Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 20 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE, MOHAMED SELF KHATIB) (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA)**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha kwa Mwaka 2003/2004 (*The Annual Report and Accounts of the* Arusha *International Conference Centre for the year* 2003/2004).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. ISSA MOHAMMED SULEIMAN (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira Kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni yake kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 294

**Ofisi za Wabunge**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikwishatoa maagizo kuwa Ofisi za Wabunge ziwe katika maeneo yaliyopo ndani ya majimbo yao na kwa kuwa Jimbo la Nanyumbu halijapatiwa Ofisi ya Mbunge hadi sasa:-

(a) Je, ni sababu gani zilizoifanya Serikali kushindwa kuweka Ofisi ya Mbunge katika jimbo hilo?

(b) Je, ni nini gharama yote ya kuipata Ofisi hiyo?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kukosekana kwa Ofisi hiyo kumechangiwa na udhaifu wa kiutendaji katika ngazi za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kuchukua nafasi hii kujibu swali la Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kulingana na maagizo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wakuu wa mikoa katika barua yake ya tarehe 24/7/2004 aliagiza kua Ofisi za Wabunge zitakuwa katika ofisi za majengo ya wakuu wa wilaya. Pia Waheshimiwa Wabunge ambao majimbo yao hayapo katika Makao Makuu ya Wilaya Ofisi zao ziwe katika majengo ya Serikali katika ofisi za Katibu Tarafa, Kata au Kijiji.

Vile vile alisisitiza kuwa Wabunge wa viti maalum wapatiwe Ofisi kwenye jengo la Serikali katika makao makuu ya Mkoa. Katika barua hiyo pia aliagiza kuwa Serikali ya Mkoa au Wilaya haikatazwi kujenga ofisi ya Mbunge iwapo hali ya fedha inawaruhusu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika kuhakikisha kuwa Waheshimiwa Wabunge wanapatiwa Ofisi, Serikali ya Mkoa wa Mtwara na ya Wilaya ya Masasi mpaka sasa zimekwisha fanya jitihada mbalimbali ili Mheshimiwa Aridi M. Uledi Mbunge wa Nanyumbu apatiwe Ofisi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara ilipatia Wilaya ya Masasi ya Masasi jumla ya shilingi 2,600,000/= kwa ajili ya kufanya ukarabati wa Ofisi ya Waheshimiwa Wabunge watatu (3) wa Wilaya ya Masasi yaani Mbunge wa Masasi, Mbunge wa Lulindi na Mbunge wa Nanyumbu. Ofisi hizo zilikarabatiwa na kuwekewa samani, lakini hadi sasa ni Ofisi moja tu ya Mbunge wa Jimbo la Masasi peke ndiyo inayotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ukarabati huo Mheshimiwa Mbunge wa Nanyumbu alitaka ajengewe ofisi katika jimbo lake la Nanyumbu na Serikali Wilayani humo ilianza kutafuta jengo la Serikali ambalo lingeweza kutumika kama Ofisi ya Mbunge. Juhudi hizo zilizaa matunda kwa kupata jengo lililokuwa linatumiwa kama ofisi ya kata ya Nanyumbu na kata hiyo ilikubali kutoa sehemu ya jengo hilo ili litumiwe na Mheshimiwa Mbunge.

Lakini Mheshimiwa Mbunge alilikataa jengo hilo kwa madai kuwa Makao Makuu ya jimbo lake yapo kwenye mji mdogo wa Mangaka na hivyo alitaka ofisi yake iwe hapo katika mojawapo ya majengo ya Chuo cha Utafiti wa kilimo – Naliendele. Katibu Tawala wa Wilaya ya Masasi aliuandikia uongozi wa Chuo hicho kuomba kupatiwa ofisi lakini mpaka sasa bado majibu hayajapatikana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga jengo la Ofisi ya kila Mbunge kwenye jimbo lake la uchaguzi kutokana na ufinyu wa Bajeti. Aidha gharama kamili za Ofisi za Wabunge inategemea zaidi vigezo yaani *standard* za ofisi za Wabunge ambavyo mpaka sasa havijatolewa. Hivyo ni vyema kujua vigezo hivyo ndipo tujue gharama yote ya ujenzi wa Ofisi ya Mbunge.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo niliyoyatoa hapo juu ni wazi kwamba kukosekana kwa Ofisi ya Mbunge wa Nanyumbu hakukuchangia na udhaifu wa kiutendaji katika ngazi yoyote ya Serikali. Kwani hii inategemea uwezo wa kifedha wa Serikali na vipaumbele vya jamii, Wilaya na Mkoa husika.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa makao makuu la Jimbo la Nanyumbu, yako Mangaka, Je, isingekuwa busara basi kwa Serikali kujenga ofisi ya Mbunge pale Mangaka kuliko kuipeleka kwenye kata Nanyumbu?

La pili, kwa kuwa pale Mangaka kuna jengo ambalo zamani lilikuwa zahanati lakini sasa haitumiki baada ya kupata kituo cha afya cha Mangaka, kwa nini basi jengo hili lisikarabatiwe likawa ofisi ya Mbunge badala ya kuliacha bila matumizi yoyote kama ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba kimsingi tunakubaliana na Mheshimiwa Uledi, kwamba kwa kuwa makao makuu ya Jimbo ni Mangaka, sasa hizi juhudi zetu sasa zinaelekezwa Makanga, kwa sababu hata kule

Nanyumbu ambapo tulishampatia jengo, alisema hapana pale sio makao makuu ya Jimbo na sisi tukakubaliana naye, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Uledi kwamba juhudi sasa ziko Mangaka, na hili jengo la zahanati ambalo wamelitaja tutakwenda kutazama kama uwezekano upo wa kulikarabati na kulifanya liwe ofisi ya Mheshimiwa Mbunge wakati fedha zinatafutwa za kujenga ofisi kamili.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo moja la nyongeza. Inayoonyesha kwamba majibu yaliyotolewa hapa kwamba kuna baadhi ya majimbo mengi nchi bado ukarabati wala kujenga ofisi, na fedha zimetolewa; Je, Serikali inakubali kabla ya uchaguzi au baada ya uchaguzi kufuatilia fedha hizi kwanza ili baadaye utaratibu unaofuatwa ufuatwe, kwa sababu fedha inaonyesha hazijatumika au zimetumika mahali pengine, mnaweze mkafuatilia hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imekuwa inatoa fedha na kuzipeleka kwa makatibu tawala wa mikoa kwa ajili ya kukarabati ofisi za Wabunge na kununua thamani. Sasa hoja ya Mheshimiwa Mbunge inasema kuna baadhi ya mikoa pesa hizo hazijanunua thamani wala hazijakarabati ofisi yoyote ya Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafuatilia usahihi wa jambo hili. *(Makofi)*

Na. 295

**Hospitali ya Dareda**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2002/2003 Serikali ilikubali kimsingi kuifanya hospitali ya Dareda kuwa hospitali Teule ya Mkoa na kupeleka bajeti ya mishahara na matumizi mengine yaani – OC; na kwa kuwa, kilichokuwa kimebakia ni Ofisi ya RAS Manyara kuweka Mkataba na hospitali hiyo ya Dareda (Jimbo Katoliki Mbulu) ambalo liko tayari kwa kusudi hilo:-

(a) Je, kwa nini Ofisi ya *RAS* Manyara haijakamilisha mkataba huo wakati vikao husika *(RCC)* vilishakubali uamuzi huo wa Serikali?

(b) Kama yupo mtu yeyote anayetatanisha utendaji wa Serikali kuhusiana na jambo hilo. Je, kwa nini asiwajibishwe ipasavyo ili kulinda hadhi ya utendaji wa Serikali?

(c) Je, kuchukua muda mrefu katika utekelezaji wa shughuli ya Serikali, hakuonyeshi hali ya kujali zaidi maslahi binafsi kuliko utumishi wa umma?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (k.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Katibu Tawala, Mkoa wa Manyara haina taarifa kwamba mwaka 2002/2003 Serikali ilikubali kimsingi kuifanya hospitali ya Dareda kuwa hospitali teule ya Mkoa na kupeleka bajeti ya Mishahara na matumizi mengine yaani *Other Charges* kwa msingi kwamba ni hospitali teule ya Mkoa. Aidha, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara haijawahi kupata maelekezo kutoka Serikali kuu juu ya kuwekeana mkataba na hospitali ya Dareda kama Hospitali teule ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kikao cha Kamati ya ushauri cha Mkoa ambacho Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe kilifanyika tarehe 23 Machi, 2004 na kuhudhuriwa na Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, katika kikao hicho suala la Hospitali ya Dareda lilizungumzwa katika agenda ya mengineyo baada ya mjumbe mmoja kutaka kufahamu kama ni kweli hospitali ya Dareda imefanywa kuwa Hospitali ya mkoa wa Manyara. Mazungumzo hayo yalipewa agenda Muhitasali Na. MNR/RCC/13/07: chini ya Mengineyo. Katika kulipa umuhimu suala hili, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilitaka kupata taarifa zaidi kuhusu Hospitali ya Dareda na iliundwa timu ya wataalam kuchambua namna mkoa utakavyoweza kupata huduma za hospitali ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya wataalam hao ilibainisha njia tatu zifuatazo;

- Kujenga Hospital ya Mkoa.

- Hospitali ya Wilaya ya Babati kutoa huduma zitolewazo na Hospitali ya Mkoa.

- Kuifanya Hospitali ya Dareda kuwa Hospitali teule ya Mkoa wa Manyara.

Baada ya majadiliano ya kina uamuzi wa kikao (*RCC*) katika suala hili haukuwa kuifanya hospitali ya Dareda kuwa hospitali teule ya mkoa bali iliamuliwa Hospitali mpya ya mkoa ijengewa. Aidha, katika agenda ya awali ya mkutano huu kikao kilishapitisha mradi wa ujenzi wa hospitali ya mkoa awamu ya kwanza kwenye bajeti yake ya mwaka 2004/2005, ambapo ulitenga Shs.200, 000,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kikao cha Kamati ya ushauri ya mkoa kilitenga kiasi cha Shs 200,000,000/= ili kuanza mradi wa ujenzi wa awamu ya kwanza wa Hospitali ya mkoa kwenye bajeti yake ya mwaka 2004/2005 Bunge liliidhinisha kiasi cha Shs 100,000,000/= tu ambazo zilitumika kwenye ujenzi wa boma la mkoa ambalo ni kipaumbele kwa wakati huu kwani Mkoa ulianzishwa bila ya kuwa na Ofisi mbadala ambazo zingeweza kutumika ili kutoa nafasi kwa mipango mingine ya maendeleo bila ya

kipingamizi. Ili kuonyesha nia ya ujenzi wa hospitali ya mkoa, katika mwaka fedha 2005/2006 kiasi cha Shs 100,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana nia ya baadhi ya wananchi ya kuitaka kuifanya Hospitali ya Dareda kuwa Hospitali teule ya mkoa ilikuwepo jambo hili ni zuri tu na Serikali inaipongeza. Hata hivyo, kutokana na msimamo huu wa mkoa na kwa mantiki iliyojitokeza katika majibu niliyoyatoa utaona kwamba hospitali ya Dareda haijafanywa kuwa hospitali teule ya mkoa na hakuna mtu katika ofisi ya katibu tawala wa mkoa wa Manyara anayetatanisha utendaji katika Serikali kwa maslahi binafsi. *(Makofi)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu haya ya Serikali ambayo kwa kweli hayaridhishi, hayaridhishi kwa sababu yanapingana yenyewe kwa yenyewe.

Je, Serikali inafahamu kwamba inapeleka shilingi milioni 500 kwa ajili ya bajeti ya kuendesha hospitali ya Dareda kwa misingi kwamba ni hospitali teule ya mkoa?

La pili, kwa kuwa wazo la kufanya hospitali ya Dareda kuwa hospitali teule ilitokana na kutokuwa na hospitali ya mkoa kwa muda sasa wa miaka mitatu, na kwamba hiyo ingeweza kufanyika kwa muda mfupi tu hadi hapo hospitali ya mkoa itakapokuwa tayari. Kwa nini Serikali inasita kuifanya hospitali ya Dareda kuwa teule kwa muda kwa nini inasita?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba majibu niliyoyatoa hayaridhishi, yanaridhisha na ningemwomba akubaliane na mimi hivyo hivyo kwa kuwa hospitali hiyo ambayo ameizungumzia imefanya kazi nzuri sana na mimi niliwahi nilipokuwa Waziri wa Afya ya kutembelea ile sehemu ya hospitali.

Mheshim iwa Spika, nataka kutoa pongezi maalumu kwa viongozi wa hospitali wa misheni kwa kazi nzuri walioifanyia wananchi wa mkoa wa Manyara na Babati na hospitali kama hizo ziko nyingi nchi hii na zinafanya kazi na Serikali inatoa pesa kama kusaidia hospitali kutoa huduma kwa wananchi, sio 500 milioni kuna hospitali zingine Serikali inatoa zaidi ya 500 milioni.

Kwa hiyo nataka nikuhakikishie jibu ni hilo ni sahihi, lakini la pili ni kwamba hospitali hiyo iliamuliwa kutoa huduma za hospitali za mkoa za Manyara kwa miaka mingi. Suala la mkoa wa Manyara umeanza juzi ni kama miaka miwili iliyopita, hospitali ile ilikuwa imetoa huduma kama sehemu ya hospitali ya mkoa wa Arusha ili hospitali iweze kuwa hospitali ya mkoa sifa zifuatazo lazima ziwepo.

(i) Hospitali hiyo iwe na madaktari wa kutosha, mabingwa wasiopungua wanne katika fani ya upasuaji, fani ya watoto, fani ya maradhi ya kina mama na uzazi, fani ya magonjwa ya moyo, figo, kifua na fani ya daktari wa meno na *geologia*, *ultrasound*, maabara, *authologia* na kadhalika na wauguzi wasiopungua 20.

Vigezo hivi ndivyo vinawezesha Wizara ya Afya kutoa kibali cha kuanzishwa kwa hospitali ya mkoa. Lakini wakati huo huo hospitali hiyo pia lazima iwe na vitanda ambavyo havipungui 200.

(ii) Lazima Hospitali hiyo iwe karibu na makao makuu ya mkoa kiutawala, sasa kama sifa hizo hazipo mimi ninaomba ndugu yangu alijue hilo kwa sababu kazi aliyoifanya ni nzuri na hospitali ile ni nzuri Serikali itaendelea kutoa ruzuku na kutoa huduma kwa wananchi. Swali nilivyolijibu ni sahihi kabisa ndilo jibu la Serikali, na kama ana mawazo mengine tuonane tutapashana habari namna ya kuisaidia hospitali ya Dareda. *(Makofi)*

Na. 296

**Utekelezaji wa Barabara kwa Nguvu za Wananchi**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wilayani Same wamejitoa mhanga kuchimba barabara zao zote za milimani kwa nguvu zao wenyewe; na kwa kuwa, idadi kubwa ya wananchi hao 75% wanaishi katika ukanda wa milimani; na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais alifanya ziara wilayani Same na kusafiri katika barabara ya Makanya – Suji/Gonjanza iliyochimbwa na wananchi hao, na alifurahishwa na juhudi za wananchi katika kuchimba barabara zao wenyewe na kwa kuwa, aliahidi kuwa barabara hiyo itengenezwe ili iweze kupitika majira yote na kwa kuwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilituma mkandarasi kuifanyia tathmini barabara hiyo kwa lengo la kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa na kwa kiwango gani?

(b) Je, baada ya matengenezo hayo, itakuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Same au itapandishwa daraja kuwa barabara ya Mkoa ili kuweka kumbukumbu ya ziara ya Mheshimiwa Rais katika milima ya Same?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Makanya – Suji yenye urefu wa kilometa 20 ni barabara ya wilaya na hivyo iko chini ya usimamizi wa Halmashauri ya wilaya ya Same.

Barabara hii inaunganisha tambarare ya Same Magharibi na Kata ya Suji ambayo ipo milimiani. Mheshimiwa Rais alipotembelea wilaya ya Same tarehe 02/02/2002 alipita kwenye barabara hiyo wakati akielekea kata ya Suji na kujionea mwenyewe mchango mkubwa wa wananchi waliojitolea kujenga barabara hiyo katika maeneo ya milimani na aliguswa sana na hali mbaya ya barabara hiyo. Kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Rais aliahidi kutoa msaada wa kuboresha barabara hiyo ili kuwatia moyo wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Halmashauri ya Wilaya ya Same iliwasilisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mchanganuo wa gharama za matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe ambayo ilifikia Sh. 150,000,000,000.

Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Ujenzi tulitoa fedha hizo na kwa sasa barabara hiyo iko katika hatua za mwisho za kukalimilisha matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe.

Aidha, kuhusu kuipandisha daraja barabara hiyo kuwa barabara ya mkoa ili ihudumiwe na *TANROADS*, namshauri Mheshimiwa Mbunge kulipitisha suala hili katika bodi ya barabara ya mkoa ambayo iko katika nafasi nzuri zaidi ya kuweza kuona umuhimu wa barabara hiyo kupandishwa daraja na kuwa ya mkoa.

Hata hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge akubali ukweli kuwa hata hivyo namwomba Mheshimiwa Mbunge akubali ukweli kuwa hata *TANROADS* haijaweza kuzihudumia barabara zote za mtandao ulio chini ya usimamizi wake vizuri kama ipasavyo kutokana na ufinyu wa Bajeti.Kupitia Bunge lako Tukufu naomba Mheshimiwa Mbunge afikishe salamu zangu za pongezi kwa wananchi wa jimbo la Same Magharibi na kwake mwenyewe binafsi kwa moyo wao wa kujitolea katika juhudi za kuhudumia

barabara zao wenyewe na hivyo kuwa mfano wa kuigwa na wananchi wengine hapa nchini.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Kwanza nishukuru kwa majibu ya Serikali, lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Same niishukuru Serikali kwa kutoa msaada wa milioni 150 kwa ajili ya matengezo ya barabara ile. Pamoja na majibu haya nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Waziri amesema barabara ile imetengenezwa kwa kiwango cha changarawe, tayari walishaanza matengenezo ya barabara ile lakini ni kwa kiwango cha udongo, ningeomba Serikali ikaangalie pesa yake kama imetumika vizuri. Walishaanza kutengeneza kwa kiwango cha udongo. Je, hayo ni matumizi sahihi ya fedha ya Serikali iliyokusudiwa na kupotosha ahadi ya Rais kwa wananchi?

(ii) Kwa kuwa wananchi kabla barabara hii haijapatiwa msaada walikuwa wamekusanya kifusi au moramu kwa ajili ya kulipea barabara yao yenye thamani ya shilingi milioni moja na mkandarasi akaja akatumia kile kifusi kwa ajili ya matengenezo ya hiyo barabara. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kumwambia mkandarasi aweze kuwarejeshea wananchi fedha yao ambayo walichangia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza pongezi za wananchi wa Same Magharibi kuhusu msaada wa Serikali tumezipokea kwa furaha kubwa na tutazidi kushirikiana nao kwa mengine mengi kuliko hili. Sasa kuhusu hoja zake mbili nataka kuzijibu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwamba Serikali imetoa shilingi milioni 150, kwa ajili ya kutengeneza ile barabara, Mheshimiwa Mbunge anasema lakini matengenezo yale hayafanani na ile gharama ya zile pesa na ameomba Serikali tufuatiliea.

Nataka kusema tu kwamba Serikali inakwenda ngazi mbalimbali kuanzia huku katika ngazi ya Serikali kuu mpaka ngazi za kata huko, kwa hiyo ningependa kuwaomba madiwani wa eneo husika wa Halmashauri ya Same kwa kweli na wenyewe wawe na uchungu wa hizi pesa ambazo Serikali imewapa wafuatilie wenzetu wazungu wanaita *value for money* yaani je kazi ile inafanana na thamani ya zile pesa? Naomba madiwani nadhani wananisikiliza huko Same wafuatilie vile vile na ile moramu.

Sasa kama mkandarasi alichukua moramu ya wananchi, vile vile madiwani wambane kwamba ainunue maana yeye amepata pesa milioni 150 ainunue ile moramu ambayo wananchi walikuwa wametengeneza. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge na Naibu Spika, tusaidiane sisi Wizara na Halmashauri ya Wilaya ya Same kupitia Madiwani wake kukagua hii kazi na kama ni hafifu tumbane basi atengeneze kitu kamilifu.

**NAIBU SPIKA:** Swali hili linalofuata la 297 halijapata majibu Serikalini, kwa hiyo litaulizwa siku zijazo.

Na. 298

**Mwenendo wa Bei ya Pamba Katika Soko la Dunia**

**MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y. MHE. JAMES P. MUSALIKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kampuni za ununuzi wa pamba hufuatilia mwenendo wa bei ya zao hilo katika soko la dunia, kujipanga kwenye cartel na kupanga bei ya zao hilo dhidi ya wakulima na pia kwa kuwa Serikali imejiondoa katika kupanga bei ya mazao kwa mujibu wa soko huru:-

(a) Je, Serikali itawadaidiaje wakulima kufahamu mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia ili nao wajipange katika kupanga bei yao kwa kuzingatia gharama za uzalishaji na bei katika soko la dunia badala ya kuacha jukumu hilo kwa vyama vya ushirika ambavyo ama vimekufa au vina migogoro na pengine havina mwelekeo kabisa?

(b) Je, hadi kufikia wakati swali hili linavyojibiwa, bei ya pamba nyuzi katika soko la dunia ni senti ngapi za Dola za Marekani kwa ratili na ni sawa na shilingi ngapi za Tanzania kwa kilo ya pamba mbegu iuzwayo gulioni hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya Vyama vya Ushirika vinavyojishughulisha na ukusanyaji na uuzaji wa pamba vina matatizo ya kibiashara kama ilivyo kwa wafanyabiashara wengine duniani katika mfumo wa sasa wa soko huru na utandawazi ambpao bei za mazao ghafi hupanda na kushuka bila kutarajiwa hasa katika biashara ya mazao ya kilimo (*Trading in Agricultural Commodities*).

Hata hivyo hii haina maana kwamba Vyama vya Ushirika havina mwelekeo wowote. Matatizo ya kibiashara yakitokea inabidi kutafuta mbinu za kuyatatua na siyo kukata tama na ndiyo maana Serikali imeandaa Mpango Kabambe na Modenaizesheni ya Ushirika Nchini. Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo ya kibiashara yanayovikabili vyama vya ushirika na wafanyabiashara wengine kitendo cha wanunuzi wa mazao likiwemo zao la pamba kujipanga na kuunda makundi ya *Cartel* kwa lengo la kupanga bei za mazao ni kinyume cha Sheria na taratibu zinazosimamia ununuzi wa mazao chini ya mfumo wa soko huria.

Kwa hiyo, wanunuzi wa pamba vikiwemo vyama vya ushirika hawatakiwi kujipanga kwa lengo la kupanga bei kwani kufanya hivyo ni kuvunja sheria na taratibu za ununuzi wa mazao chini ya mfumo wa soko huria zinazoelekeza kuwepo kwa ushindani wa wazi kwenye maeneo ya kuuzia mazao. Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwasaidia wakulima wafahamu mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia Serikali inafanya yafuatayo:-

(i) Kujijenga uwezo kupitia Wizara ya Ushirika na Masoko ili kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko kwa kutumia teknolojia za kisasa ikiwa ni pamoja na matumizi ya mtandao wa *internet* katika kutafuta taarifa za masoko. Wizara pia inaandaa Tovuti yake ambayo pamoja na taarifa nyingine itakuwa ikihifadhi taarifa mbalimbali za masoko ya mazao yanayouzwa nje ya nchi na hivyo kuwawezesha watumiaji wa mitandao ya internet kupata taarifa hizo.

(ii) Kutoa taarifa za bei kupitia Bodi ya Pamba Tanzania kuhusu mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia kupitia kipindi cha Pamba yetu ambacho hurushwa hewani na *Radio Tanzania* kwa kutoa ufafanuzi wa matarajio ya mwenendo wa bei kwa siku zijazo na hivyo kuwaelewesha wakulima kama bei inatarajiwa kupanda au kushuka. Maelezo haya yana lengo la kumwezesha mkulima kujadiliana na wanunuzi juu ya bei ya pamba yake.

(iii) Ili kuwalinda wakulima Serikali iko tayari kuyachukulia hatua Makampuni yatakayothibitika kuwa yanajipanga kwenye *Cartel* na kupanga bei ya zao lolote kwani kufanya hivyo ni kuvunja kanuni na taratibu zilizowekwa katika biashara ya mazao yote nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuwanyang’anya leseni za kununulia mazao.

(iv) Kuhamasisha matumizi ya mbinu kinga dhidi ya maanguko ya bei ikiwa ni pamoja na kuweka bima za mazao kuhimiza kilimo cha mikataba, kuuza kwa mihadi yaani *forward sale* na kutumia mfumo wa stakabadhi za mazao katika maghala.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa bei ya pamba nyuzi ya Tanzania katika soko la kimataifa iliyokuwepo tarehe 19 Julai, 2005 yaani jana ni senti za Marekani 43 kwa ratili ya pamba nyuzi. Ukiondoa gharama za uendeshaji, kodi na ushuru mbalimbali, bei hii ni sawa na shilingi 234/= kwa kilo ya pamba mbegu daraja la kwanza hapa Tanzania. Bei za pamba hupanda na kushuka kutegemea bei ya zao hilo katika soko la dunia, kiwango cha ushindani kwenye soko, ubora wa zao na ufanisi wa mfumo wa ununuzi anaoutumia mnunuzi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha wanunuzi wa mazao likiwemo zao la pamba hujipanga na kuunda makundi ya *Cartel* la lengo la kupanga bei ni kinyume cha Sheria na taratibu zinazosimamia ununuzi wa mazao nchini chini ya mfumo wa soko huria. Kwa hiyo wananunuzi wa pamba hawatakiwa kujipanga kwa lengo la kupanga bei kwani kufanya hivyo ni kuvunja sheria na taratibu za ununuzi wa mazoa chini ya mfumo wa soko huria zinaelekeza kuwepo kwa ushindani wa wazi kwenye maeneo ya kuuzia mazao. Ili kuwalinda wakulima Serikali iko tayari kuyachukuliwa hatua makampuni yatakayodhibitika kuwa yanajipanga kwenye *Cartel* na kupanga bei ya zao lolote kwani

kufanya hivyo ni kuvunja kanuni na taratibu zilizowekwa katika biashara ya mazao yote nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuwanyang'anya leseni za kununulia mazao.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Geita, Nyangw'ale na Busanda hawana utaalamu wa *Internet* ambayo ingeweza ikawajulisha kwamba bei ya pamba imepanda kiasi gani na wanunuzi wa pamba wanapata nafasi kubwa ya kuweza kuwanyonya wananchi kwa kupunguza bei na kununua pamba kwa bei ya chini sana. Kwa mfano kampuni ya *KOPOT* mwaka jana iliweza ikawanunulia wananchi baada ya bei ya pamba kupungua iliweza kutoa stakabadhi ya wananchi. Je, Serikali inasemaje kuhusu kampuni hii ambayo imewanyonya wananchi?

Kwa kuwa wananchi wale hawana uthibitisho wa ununuzi wa pamba yao kwa sababu hawana stakabadhi. Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ambao wamenunuliwa pamba bila stakabadhi yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ernest Mabina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimetoa maelezo katika kujibu swali la msingi kwamba, hizi mbinu mpya za kutumia *internet* zinazoandaliwa nia na madhumuni yake ni kwamba ziweze kuwasaidia wakulima kupitia Wizara kama nilivyokuwa nimesema kwamba Wizara imeandaa mifumo hiyo ili wakulima waweze kuipata kupita kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini isitoshe nimeeleza hapa kwamba tunaandaa mfumo wa kuboresha ushirika nchini ambayo ni njia pekee ambayo wakulima kwa umoja wao wakiungana wanaweza wakapambana na mbinu zote chafu zinazofanyika na wafanyabiashara binafsi. Kwa hali hiyo hata katika hawa wanunuzi ambao wamewapunja hivi sasa hatuwezi tukasema kwamba Serikali itachukua hatua gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhania tu kwamba suluhisho la mwisho kwa wakulima wetu kuepukana na kupunjwa ni kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika ili waweze wakawa na nguvu ya pamoja na hatimaye kutumia hizi mbinu mpya ambazo nimezieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka tu nitoe wito kwa wakulima wote na wananchi wote nchini kwamba, ili waweze wakatumia hii mitandao mipya ambayo imeanzishwa pamoja na kuepukana na kupunjwa na wafanyabiashara binafsi waweze wakajiunga katika Vyama vya Ushirika waweze kuwa na ile *collective bargain*. Lakini vivyo hivyo ningependa tu kwamba kwa wale ambao wanawabaini wale wanaowapunja watoe taarifa kwa vyombo vinavyohusika Serikalini ili waweze wakachukuliwa hatua hapo hapo bila kusubiri muda mrefu. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anavyotoa majibu, ukweli ni kwamba kuna kero katika taratibu nzima ya ununuzi wa pamba na kwamba wakulima wameanza kukata tama. Pia kwa kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya ukuzaji na kusimamia zao la pamba ya mwaka 2001 tuliyotunga hapa Bungeni ilitakiwa mpaka sasa mkulima wa zao la pamba awe analindwa kikamilifu.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba Wizara imekawia mno katika kuitumia Bodi ya Pamba kusimamia bei ya pamba ili wananchi wasipunjwe katika maeneo hayo hayo wanapouzia na kununulia pamba, kwa nini Wizara imekawia pamoja na kuimarisha Vyama vya Ushirika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda tu nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwepo na kero katika ununuzi wa pamba kama alivyosema. Lakini Serikali baada ya kubaini kwamba kuna kero za namna hiyo ndio maana inachukua sasa hatua mbalimbali. Moja ya hatua ambazo inachukua na hivi sasa ni hiyo niliyoieleza na ambayo mwenyewe amekiri kwamba tunaimarisha Vyama vya Ushirika ili wakulima waweze kuwa na uelewa katika suala hili na kuweza kupambana na kero zinazowakabili.

Lakini vilevile Serikali haijachelewa hata kidogo kwamba labda imechelewa kukabiliana na tatizo la kukabiliana na tatizo la kutatua kero hii. Serikali inasimamia kikamilifu katika suala la kuwalinda wakulima na ndio maana tumesema kwamba taratibu zilizowekwa katika mfumo wa soko huria zinataka wakulima waweze kuwa macho na wanunuzi ambao wanawapa kero hawa wakulima na hatimaye kutoa taarifa kwa Serikali yoyote kuchukua hatua. Kwa hiyo Serikali mara zote iko pale kuweza kuwasaidia wakulima na kuondoa kero zozote ambazo zinawakabili na hatua zote hizi zinazochukuliwa na Serikali ni katika mchakato huu wa kuondoa kero ambazo zinawakabili wakulima.

Na. 299

**Dawa za Kurefusha Maisha kwa Waathirika wa UKIMWI.**

**MHE. LEONARD M. SHANGO (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilijiwekea lengo la kuwasaidia watu walioathirika na ugonjwa wa Ukimwi kwa kuwapatia dawa za kurefusha maisha kwa mwaka wa kwanza kusaidia Mkoa wa Dar es Salaam wagonjwa 10320, hospitali za rufaa 3600, Hospitali za Mikoa

14,640, Hospitali za Wilaya 11160 na hospitali za mashirika ya Dini na hospitali binafsi 4320.

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika kutekeleza lengo lake hilo zuri?

(b) Je, wagonjwa wote wanapatiwa dawa hizo na kama siyo wote wanaopewa dawa hizo ni kwa sababu gani?

(c) Kati ya wagonjwa husika je, ni watoto wangapi na watu wazima wangapi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutoa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa Ukimwi hatua zifuatazo zimechukuliwa. Dawa za kupunguza makali ya Ukimwi *(ARVs)* zimetolewa katika vituo 96 vya hospitali za Serikali, mashirika ya dini na binafsi. Mpaka sasa Serikali imeshanunua dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 10 ambazo zitatoshereza wagonjwa 21,000/=. Mpaka kufikia Desemba mwaka huu wa 2005 jumla ya wagonjwa 44,000 wanatarajiwa kunufaika na mpango huu. Lengo la mpango huu ni kuwafikia wagonjwa 500,000 katika kipindi cha miaka 5.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wagonjwa wanaopatiwa dawa ni wale tu ambao wametimiza vigezo vya kitaalam kama vilivyoainishwa katika mwongozo wa kitaifa wa kutoa dawa hizo. Vigezo hivyo ni pamoja na mgonjwa kuthibitishwa kuwa na upungufu mkubwa wa chembechembe hai nyeupe za damu ambazo husaidia kinga dhidi ya maradhi mwilini.

Mgonjwa anapothibitishwa kuwa na *CD4 count* kwa kiwango cha 200 au chini yake hupatiwa dawa. Aidha kigezo kingine ni wakati mgonjwa anakuwa na dalili za UKIMWI zilizofikia kiwango cha daraja la tatu kulingana na mwongozo wa Shirika la Afya Duniani. Katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga Tshs. 20 bilioni kwa ajili ya kununua dawa ili kuwezesha kuongeza idadi ya wagonjwa wanaohitaji dawa katika mpango huu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya wagonjwa 21,000 wanaopata dawa inakadiriwa kuwa watoto wapato 4,240 (asilimia ishirini) wananufaika na dawa hizi. Waliobaki ni watu wazima.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa waathirika kujitangaza kisheria na kwa kujenga mazingira ya kujitangaza ili kupunguza kasi ya maambukizi?

Je, Serikali inawatambua na kuwasadia waganga wa kienyeji ambao sasa wanasaidia sana katika janga hili?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Leonard Shango kama ifuatavyo:-

Kuna sheria ambazo zilitungwa kuambukiza mtu yoyote magonjwa yoyote ya zinaa pamoja na UKIMWI na kwa kweli hata ukitunga Sheria ni juu ya watu kufuata maadili kwa sababu kuvunja Sheria ni kuvunja Sheria watu wengi wametungiwa Sheria wasiue, wanauwa. Lakini bado Serikali inalifuatilia sana swali hili na kwa kweli Watanzania wengi sasa wameelimika na wanajua athari ya ugonjwa huu na ni kutokana hili tu ndio tunaweza kuwafikishia Watanzania wengi ujumbe huu kwamba, kama wewe ni mgonjwa usimuue mwenzako ni dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu na wengi wamefanya hivyo. Sasa kama mtu hafuati hayo, hata ukimuhubiria namna gani ukimweka ndani utamuua bado ana imani kwamba kitendo chake kile ni sahihi. Kwa hiyo, ninaungana na Mheshimiwa Leonard Shango kwamba kwa kweli Sheria inatakiwa itungwe, lakini Sheria zipo zitaimarishwa.

Katika swali la nyongeza la pili, waganga wa jadi, siyo waganga wa kienyeji ni waganga wa jadi wamefanya kazi nzuri sana katika Taifa hili. Ndio sababu Serikali imewatambua na ndio sababu tunakitengo cha dawa asilia kule Mhimbili na bado sehemu nyingi wanafanya kazi na dawa hizi ambazo waligundua zimeweza kutambulika na nyingine zimepelekwa Ulaya zinafanyiwa kazi. Kwa hiyo Serikali inawatambua na wanafanya kazi na bado wananchi wengi wanakwenda kwa waganga wa jadi na bila waganga wa jadi nchi hii ingepata shida kubwa sana katika nyanja ya matibabu. Kwa hivyo tunawatambua. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu na maelekezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba Serikali ikubaliane na mimi kwamba pamoja na madawa hayo ya kurefusha maisha. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inawapa lishe kwa sababu chakula nacho kilicho bora ni sehemu ya matibabu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA AFYA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Ndugu yangu maarufu Mheshimiwa Lucas Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua hilo na ndio maana wagonjwa wanaopata dawa katika hospitali na hii naizungumzia katika Hospitali yetu ya Jeshi na ni matumaini yangu ni hospitali zote. Lakini suala la ubora wa chakula ni suala la familia, ni kweli kila mtu achukue jukumu la kusaidia Serikali, maana tukiacha kuwa Serikali ndio

ilishe wagonjwa ipeleka chakula, dawa haitawezekana. Kwa hivyo Mheshimiwa Lucas Selelii nakuomba uisadie Serikali, najua wewe ni Mbunge shupavu sana na uwaeleze wananchi wako upande wa *Chief* kule kwamba suala hili ni jukumu la watu na ni jukumu la kila Mtanzania walishe wagonjwa na vyakula hivyo siyo ghali, kuna matunda, kuna vyakula ambavyo tunalima karanga na kila kitu.

Kwa hivyo hili ni suala la familia lakini Serikali itahakikisha kwamba dawa zinapatikana, ndio sababu nimesema lengo la Serikali hadi kufikia Desemba itakuwa imeshawahudumia asilimia 88 ya lengo kwa kuhudumia wagonjwa 50.

Na. 300

**Ujenzi wa Barabara Kupitia TANAPA**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikwisha kutoa ahadi ya kutengeneza barabara ya Chubi-Itaswi-Mauno-Kinyasi-Majengo; badala ya barabara ya Chubi-Itaswi-Kisaki kupitia Shirika la Hifadhi ya Wanyama Pori *TANAPA;*

(a) Kwa kuwa, ahadi hiyo imechelewa kutekelezwa kwa takriban miaka sita. Je, Serikali inaweza kuwaambia wananchi sababu za kuchelewa kutekelezwa kwa kazi hiyo; na kwamba sasa barabara hiyo itatengenezwa lini kwa manufaa ya wananchi hao ambao ni wadau wa karibu wa Hifadhi ya mbuga ya Tarangire chini ya *TANAPA?*

(b) Je, hata Serikali husema uongo, na kama haisemi uongo, mradi huo utaanza lini?

(c) Je, wananchi wa maeneo hayo hawana haki ya kusaidiwa kwa kutengenezewa barabara hiyo muhimu kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalidi Suru Mbunge wa Kondoa Kaskazini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Ni kweli kuwa Wizara yangu ilitoa ahadi ya kusaidia kukarabati barabara ya Chubi-Itaswi-Kisaki kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa *(Tanzania National Parks – TANAPA). TANAPA* haijatekeleza ahadi hiyo kutokana na kazi hiyo kuhitaji ushirikiano wa karibu kati yake na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Mwaka 2003, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini *TANAPA* akiongozwa na Menejimenti ya *TANAPA* na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa walipata fursa ya kutembelea eneo hilo. Kwa pamoja ilikubalika kuwa kazi ya kuinua tuta kwenye eneo la udongo wa mfinyanzi umbali wa karibu kilometa tano itakagharimu fedha nyingi ambapo *TANAPA* pekee haiwezi kumudu gharama hizo.

Baada ya ziara hiyo ilikubalika kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwa kutumia wataalam wake watafute njia nyingine itakayokwepa sehemu hiyo, lengo ikiwa kupunguza gharama za ujenzi na hatimaye wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuupa umuhimu wa juu mradi huu, *TANAPA* ilishauri kuwa ni muhimu kwanza kufanya tathmini ya kitaalamu kwenye eneo lote inapopita barabara hiyo ili kubaini yafuatayo:

- Urefu wa barabara;
- Kazi inayohitajika kufanyika;
- Mchanganuo wa gharama za mradi ; na
- Mitambo itakayohitajika kwa ajili ya kazi

Aidha, ilikubalika kuwa baada ya tathimini wadau wakutane kuweka mipango ya utekelezaji ili kutoa fursa kwa wadau wote wa mradi kushiriki kwenye utekelezaji.

Mpaka sasa, *TANAPA* bado wanasubiri utekelezaji wa maelekezo yaliyokuwa yameamuliwa na kukubalika na pande zote, baada ya ziara ya mwaka 2003.

(b) Serikali haisemi uwongo kwani ni mwezi uliopita tu Halmashauri imetoa taarifa ya tathmini ya kitalaam. Inabidi tathmini hii iangaliwe na *TANAPA* na baadae wadau wakutane kama makubaliano yalivyoelekeza.

(c) Wananchi wa maeneo hayo wana haki ya kusaidiwa na *TANAPA.* Nachukua nafasi hii kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa *TANAPA* ina ushirikiano mzuri na vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa Tanzania kupatia Mpango wake wa Ujirani Mwema. Kwa mfano, *TANAPA* kwa kushirikiana na wananchi wa Pahi, ilishiriki katika kukamilisha ujenzi wa *Hostel* ya Sekondari ya Amani Abeid Karume pamoja na Zahanati ya Idindiri Wilayani Kondoa.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na bidii anazofanya za kufanisha barabara hii nina uhakika ataifanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi hao wamevumilia kwa muda mrefu sana na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ndio ilikuwa inasubiriwa itoe mchango wake. Sasa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa inachangia katika barabara hiyo milioni 27.

Je, Serikali sasa iko tayari kuanza hiyo kazi mara moja kupita *TANAPA?*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalid Suru kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kwa dhati napenda kumpongeza Mheshimiwa Khalid Suru kwa kazi nzuri ambayo anafanya kwa kufuatilia barabara hii na kuwawakilisha wananchi wa Jimbo lake vizuri sana.

Lakini niseme kwamba hii *figure* ya milioni 27 naisikia hapa, kwa sababu kwa barua ambayo nilipata kutoka Halmashauri ni kwamba gharama halisi ya makisio ya mradi ni shilingi milioni 113,150,000 na kwamba Halmashauri ilikuwa itoe milioni 5. Kwa hivyo sasa tunaelezwa kwamba milioni 27 ningependa kusema kwamba itabidi wadau wote wakutane ili kulizungumza suala hili kuangalia ni jinsi gani ambavyo tutasonga mbele.

Na. 301

**Barabara Mji wa Kigoma Ujiji**

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hali ya barabara katika Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji ni mbaya sana nay a kusikitisha kutokana na ukweli kuwa uwezo wa Halmashauri hiyo ni mdogo sana kuweza kuzihudumia kikamilifu kwa sababu ya tatizo sugu la mmomonyoko wa udongo katika eneo hilo, na kwa kuwa, kikao cha *Regional Consultative Committee* Mkoa wa Kigoma kilikwishapendekeza kuwa barabara za Lumunba Road na Kigoma – Bangwe, *Airport – Kasulu Road* na Bangwe – Berege – Ujiji ziwe ni Barabara za Mkoa na hivyo zuhudumiwe moja kwa moja na *TANROADS*.

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa mmomonyoko wa udongo ni tatizo kubwa katika Halmashauri ya Mji wa Kigoma Ujiji?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kutoihusisha *TANROADS* katika ujenzi wa barabara za Jimbo la Kigoma Mjini ni kuwanyima haki wakazi zaidi ya laki moja na nusu wa Mji wa Kigoma Ujiji?

(c) Je, Serikali imeshapokea mapendekezo hayo ya Kamati ya Mkoa *(TCC)* na imefikia uamuzi gani?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Barabara za Halmashauri ya Mji Kigoma Ujiji ni mbaya. Mji wa Kigoma, kama ilivyo miji mingine iliyo kwenye milima ama miinuko una tatizo sugu la mmomonyoko wa udongo hasa kwa maeneo ya ardhi yaliyo wazi na yaliyotifuliwa au kulimwa. Ni ukweli kuwa maji ya mvua yateremkayo kwa kazi *concentrated run off* katika milima au miinuko huleta mmomonyoko wa udongo yasipodhibitiwa.

Hivyo tatizo la mmomonyoko katika barabara hutokea pale ambapo barabara imejengwa bila kuwa na umbo la kutoa maji na haina mifereji ya kutolea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubali kuwa Barabara nyingi zinazohudumiwa na Halmashauri ya Mji Kigoma Ujiji zimeathiriwa na mmomonyoko kwa sababu ya kutokuwa na mfumo wa mifereji mikubwa ya kutolea ama kukusanya maji ya mvua yanayotiririka na kuharibu barabara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kuwa kutoihusisha *TANROADS* katika ujenzi na matengenezo ya barabara za Jimbo la Kigoma Mjini ni kuwanyima haki wakazi wa mji wa Kigoma Ujiji. Wananchi wana haki ya kutengenezewa barabara na *TANROADS* kwa barabara zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na Halmashauri kutokana na fedha za Mfuko wa Barabara zu makusanyo ya Halmashaurti yao. Siyo dhana nzuri kuwajenga Watanzania kuwa watapata haki pindi barabara zao zitakapokuwa zinanatengenezwa na *TANROADS* tu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishapokea mapendekezo ya Bodi ya Barabara ya kupandisha hadhi barabara za Wilaya zenye urefu wa kilometa 354.6 kuwa Barabara Kuu. Mapendekezo hayo yataangaliwa sambamba na mapitio ya Sheria ya Barabara *Highway Ordinance* ambayo Wizara yangu inafanyia kazi kabla ya kuwasilishwa Bungeni.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kutafuta kampuni yenye wataalam wa kutosha ambao wanaweza kuufanyia utafiti udongo huo na kutoa mapendekezo kwa wanaohusika kutengeneza barabara hizo?

(b) Kama Serikali inakubaliana na mimi ushauri wangu ni lini itafanya hivyo ili wananchi wa Kigoma Ujiji waweze kupata barabara bora? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Grace Kiwelu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri tumepokea tutauzingatia. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja tu la kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Hivi ninachokiona zile barabara au hiyo barabara iliyopo Mkoani Kigoma katika Halmashauri ya Kigoma Ujiji ni ya tangu Mjerumani na jana nilikuwa naelezea hivi kwamba Deni la Taifa sisi halituhusu. Sasa kwa kuwa hakuna miundombinu inayoelekezwa Mkoa wa Kigoma kuhusu barabara hizi. Je, haoni kwamba hilo ni tatizo la kudumu na lisilo na ufumbuzi, sasa tutapata barabara lini? Naomba jibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halimenshi Mayonga kama ifuatavyo:-

Meshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba barabara za Mkoa wa Kigoma ni za enzi ya Wajerumani. Pamoja na kwamba kuna matatizo ya barabara hizi lakini Serikali ya awamu ya tatu ambaye Mheshimiwa Halimenshi Mayonga pia ni mshiriki wake mkuu na mkereketwa imefanya kazi nzuri sana, katika kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara zinapata mafanikio makubwa ni Tanzania peke yake ambayo ina miundombinu ya barabara ya kisasa hata vijijini. Tatizo lililopo ni kwamba fedha za matengenezo ya barabara zote nchini hutolewa na na Bodi ya Mfuko wa Barabara ya Taifa kwa mgawanyo ufuatao:-

- Asilimia 67 *TANROADS*,
- Asilimia 30 TAMISEMI,
- Asilimia 3 tu Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mgao huo utakubaliana na mimi kwamba ni dhahiri kuwa fedha hizo zinazotolewa kwa ajili ya *TANROAD* na zile za Serikali za Mitaa hazikidhi mahitaji yote.

Lakini jitihada zinafanywa na ndio maana Mkoa wa Kigoma umepata kipaumbele, kivuko cha Ilagala kimefunguliwa juzi. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba Serikali haipuuzi na inazingatia umuhimu wa wananchi wa Mkoa wa Kigoma wana haki ya kupata usafiri kama mikoa mingine.

Na 302

**Huduma ya Simu – Wilaya ya Tandahimba na Miji Midogo**

**MHE. LYDIA THECLA BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mtandao wa Simu wa *TTCL* na simu za mkononi ni muhimu sana katika kurahisisha mawasiliano na maendeleo kwa ujumla wake, na kwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Tandahimba, Mtwara Vijijini ikiwemo na Mji Mdogo wa Nanyamba, Shule zilizoko mbali na Makao Makuu kama Nanyamba, Mnyambe, Kitangari na kadhalika hazipapatiwa simu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyapatia maeneo hayo simu?

(b) Je, kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kuyapatia maeneo hayo simu ifikapo mwaka 2002 na ahadi hiyo bado haijatekelezwa. Je, Serikali inatuambia nini hasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Wilaya ya Tandahimba tayari yamekwisha patiwa laini 120 za simu za kisasa na Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)*.

Kwa upande kuzingatia umuhimu wa kupeleka huduma za simu za kisasa nchini kote, Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ina mpango wa kuanzisha mfuko maalum ujulikano kama *Universal Access Fund* kwa ajili hiyo. Wadau mbalimbali watahusishwa katika kuchangia Mfuko huo. Ni mategemeo yetu kuwa mara mfuko huo utakapoanza kutumika, tatizo la ukosekanaji wa huduma za simu za kisasa vijijini itapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, tunawaomba wananchi wa maeneo yaliyobakia wasubiri hadi mpango huo utakapoanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mawasiliano ya simu katika maeneo hayo, Serikali imeyashawishi makampuni ya simu za mikononi kufikisha huduma zao katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Kampuni ya Simu *Mobitel* imeshafikisha mawasiliano katika Wilaya ya Tandahimba na maeneo ya jirani. Kampuni ya Simu ya *Vodacom* nayo inafanya tathmini katika maeneo hayo na inategemea kufikisha mawasiliano huko kabla ya mwezi Septemba 2005.

Aidha, Kampuni ya Simu *Celtel* imeshafanya tathmini kwenye maeneo hayo na itafikisha mawasiliano huko wakati wowote kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maombi ya Mheshimiwa Mbunge, makampuni hayo yatatuma wataalam ili kuona kama maeneo yote hayo yatafikiwa na mawasiliano baada ya kuwasha mitambo yao.

**MHE. LYDIA THECLA BOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina maswali mawili ya nyongeza lakini bado nianze na kutoa shukrani kwa niaba ya uongozi wa Mkoa wa Mtwara na wananchi jinsi Serikali ilivyoweza kuleta simu ya *Vodacom*, *Celtel* na *Buzz* ingawa bado zinasuasua kwa hiyo natoa pongezi kwa Serikali kusikiliza matatizo yawananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kwamba Kampuni ya *Celtel* kwa kipindi cha wiki tatu zilizopita wananchi yaani kwa maana ya wateja kadi zile za Shilingi, 5,000/= ulikuwa ukinunua haziingiaa hazikubali zinakataa. Mimi ni miongoni mwa walioteseka karibu shillingi 15,000/= lakini *Celtel* wamenyamaza kimya haikutoa tangazo sawa na wanavyofanya matangazo mengine. Je Serikali hili inalijua na kwa nini wametutesa wateja wao?

La pili, napenda kujua au kuuliza ile miji midogo ambayo mpaka sasa hivi wanapata shida kupanda kwenye miti wanatafuta kusikiliza mawasiliano kati ya Wilaya na Vijiji, watapanda juu ya miti mpaka lini? Je, isingekuwa vizuri Serikali iwaambie hawa Makampuni waongeze nguzo ili na wananchi wenyewe wasikilize simu sawa na watu wengine? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza shukrani alizozitoa Mheshimiwa Mbunge kwa Wizara na kwa Serikali tunazipokea na zinatupa moyo kwamba tuendelee kupeleka mawasiliano katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu *Celtel* kwamba kuna kadi zao zilikuwa haziingii kwenye simu, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kweli hili tatizo lilikuwepo *Celtel* walitoa maelezo na hata Waziri wa Mawasiliano mwenyewe wakati wa hotuba yake ya Bajeti alitoa vilevile tamko hapa kwenye hotuba yake ya Bajeti kwamba lilikuwa ni tatizo la muda walikuwa wanabadilisha mitambo. Walipata mitambo ya kisasa zaidi kwa hiyo walikuwa wanaiondoa ile ya zamani na kuweka mitambo mipya kwa kipindi kile cha mpito kulitoa lile tatizo tunasikitika sana kwa usumbufu ambao ulipatikana.

Lakini nia ilikuwa ni kuweka mitambo mazuri ili wateja wa *Celtel* wapate huduma iliyo bora zaidi na walisema zile kadi ambazo hazikuingia zitunze ili wakishakamilisha ile mitambo baada ye utazitumia tu. Kwa hiyo Shilingi 15,000/= hazijapotea Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miji midogo kutokupata mawasiliano wanapanda juu ya miti ili wapate mawasiliano baada ya hii mitambo kuwashwa ambayo sasa hivi inawekwa na Makampuni mbalimbali habari ya watu wa Mtwara kupanda juu ya miti ili wapate mawasiliano itakuwa historia. (*Makofi*)

Na. 303

**Mahitaji ya Shule**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** alijibu:-

(a) Je, ni shule ngapi za msingi zinazohitajika hivi sasa ili watoto wote wanaostahili waweze kwenda shule?

(b) Je, ni wanafunzi wangapi Ki-mkoa waliofaulu kuingia Kidato cha Kwanza lakini hawakupata nafasi kutokana na upungufu wa shule na madarasa?

(c) Je, ni wangapi waliofaulu kuingia kidato cha tano, lakini wanakosa nafasi; na ni wangapi waliofaulu kuingia Chuo Kikuu wakakosa nafasi?

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule yaani miaka 7-13 kwa Wilaya za Vijijini kwa mwaka huu ni milioni 5,478,778.

Kwa kuwa shule za msingi za vijijini zinatakiwa kuwa na idadi ya wanafunzi 560 kwa shule hivyo zinahitajika shule za msingi 9784 ili ziweze kuchukua watoto wote milioni 5,400,000. Hata hivyo kwa hali halisi hivi sasa zipo shule za msingi 12845 katika Wilaya za Vijijini kwa hiyo kuna shule za ziada za msingi 3061. Kwa upande wa Wilaya za mijini hivi sasa kuna watoto wenye umri wa kwenda shule milioni 1,380,504 na kwa kuwa shule za mijini zinatakiwa kila shule iwe na wanafunzi 840 zinahitajika shule za msingi 1643 kukidhi idadi ya hao watoto milioni 1,300,000. kwa hali halisi hivi ziko

shule za msingi za mijini 1415 kwa katika Wilaya za mijini kuna uhaba au upungufu wa shule 228 katika miji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika jumla ya wanafanzi 562,241 walifanya mtihani wa Darasa la VII mwaka 2004. Waliofaulu walikuwa 243,043 kati ya hao 134,963 ambao ni asilimia 55.5 waliteuliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka 2005 katika shule za Sekondari za Serikali. Kwa hiyo jumla ya wanafunzi 108,080 hawakupata nafasi ya kidato cha kwanza. Orodha ya wanafunzi waliofaulu ki-Mkoa lakini hawakupata nafasi ya kidato cha kwanza kwa kukosa nafasi katika shule za Sekondari za Serikali atapewa Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa orodha hiyo ni ndefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huo wa 2004 jumla ya wanafunzi 63,370 waliofanya mtihani wa kidato cha nne. Jumla ya wanafanzi 23,929 walifaulu katika daraja la I – III na kati yao wanafunzi 16,059 ambao ni asilimia 70.1 wameteuliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2005. Kwa hiyo jumla ya wanafunzi 6,851 hawakupata nafasi ya kidato cha tano katika shule za Sekondari. Aidha jumla ya wanafunzi 13,575 walifanya mtihani wa kidato cha sita, waliofaulu katika daraja I –III ni 12,781 sawa na asilimia 94.1 ya watahiniwa wote.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa,Serikali imewahimiza watu binafsi kujenga shule lakini kwa kuwa kipato cha Watanzania ni kama dola moja tu kwa siku kwa hiyo hawana uwezo wa kupeleka vijana wao kwenye shule hizi za *private*. Je, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa Elimu na katika njia ya kupambana na umaskini itakubali kuwalipia vijana hawa waliofaulu kwenye shule za binafsi?

Pili, kwa kuwa wananchi wameitikia wito wa kujenga shule binafsi Serikali itakuwa tayari kuwasaidia wale ambao wamejitokea kujenga shule za binafsi mitaji ili waweze kuendesha shule hizo kwa ajili ya kubana pengo hili ambalo lina upungufu?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI**:- Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed Mbunge wa kuteuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wanajenga shule za binafsi na ni kweli kwamba shule hizi zinasaidia kuchukua watoto kwa mfano katika hawa 108,000 ambao walikosa nafasi, takwimu zinaonyesha kwamba watoto waliokwenda *form one* katika shule za Sekondari za binafsi wale wote 108,000 wamechukuliwa na ziada. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba hizi shule zinafanya kazi nzuri na ndiyo maana Serikali imeanza kutoa ruzuku, hatuwezi kutoa ada kwa kila mtu aliyekwenda kwenye *private* lakini Tumeanza kutoa ruzuku katika shule za *private* zile shule ambazo si za kibiashara na siyo *Seminary*, sasa Serikali inaanza kutoa ruzuku. Mwaka huu Tumeanza

kutoa 10,000 kwa kila mtoto na huu ni mwanzo mziri kuelekea katika kufanikisha maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwapa mitaji ili shule hizi za *private* zijengwe nyingi zaidi. Kwa wale ambao wanajenga shule za private kwa mfano za walemavu au watu wenye shida mbalimbali tayari Serikal imeanza kutoa msaada wa kujenga hata madarasa. Milioni 7 kwa darasa moja, milioni 9 kwa nyumba ya mwalimu, shule za *private* zinazolenga makundi yenye shida maalum kama vile walemavu kwa hiyo ni mwanzo mzuri wa kushirikiana na Serikali na Sekta binafsi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kuna vikao viwili vya Kamati, Kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali Mwenyekiti wao Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anawatangazia kutakuwa na kikao leo saa 5:00 chumba namba 231, ghorofa ya pili *wing C.*

Pia Kamati ya Fedha na Uchumi, Makamu Mwenyekiti anawatangazia kwamba kutakuwa na Kikao leo saa 5:00 asubuhi hii chumba namba 227 Jengo la Utawala. Kwa hiyo hivyo ndivyo Vikao ambavyo vinatangazwa kwa leo. Agenda inayofuata Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006
### Ofisi ya Makamu wa Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu, baada ya kuzingatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira, sasa lijadili na kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2005/06.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutulinda na kutuwezesha kutekeleza majukumu tuliyojiwekea katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, kilichojumuisha Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 1995 na 2000 kwa mafanikio makubwa chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tatu. Kwa heshima kubwa napenda kumpongeza Rais wetu aliyeliongoza Taifa hili kwa miaka kumi na hatimaye ametufikisha tena katika kipindi kingine cha uchaguzi kwa amani, utulivu na mshikamano.

naomba tena kumpongeza Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake kwa kusimamia vizuri mikutano yote iliyofanyika ya kumtafuta mgombea nafasi ya Urais wa Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2005. Navipongeza pia Vyama vya Upinzani kwa kusimamia vizuri mikutano yote iliyozaa wagombea wa nafasi ya Urais katika Uchaguzi Mkuu unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mbunge wa Chalinze, kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza kwenye uchaguzi wa Oktoba 2005, na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa Mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza pia wote walioshinda kutoka Vyama vya Upinzani watakaogombea nafasi ya Urais na Mgombea Mwenza katika uchaguzi unaokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu Bunge hili tukufu katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, lilipoteza Waheshimiwa Wabunge wafuatao:- Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria Mbunge wa Rahaleo Zanzibar, Mheshimiwa Frank Michael Mussati Mbunge wa Kasulu Mashariki, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga Mbunge wa Kilombero na Mheshimiwa Margareth Bwana Mbunge Viti Maalum Rukwa. Misiba hii imekuwa ni pigo kubwa katika Bunge hili tukufu, katika Taifa na katika familia za marehemu. Nachukua nafasi hii kuwapa pole ndugu na jamaa wa Waheshimiwa hao. Mwenyenzi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuungana na wenzangu kuwashukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda (Mb), Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil P. Mramba (Mb), na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa hotuba zao ambazo zimeelezea mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, Hotuba hizo zimefafanua sera na mikakati ya kukuza uchumi na mwelekeo wa bajeti na hatua zinazochukuliwa na Serikali kukuza uchumi na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira ya Bunge hili chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda Mbunge wa Njombe Kusini kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kutekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi mkubwa katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita na miaka mingine tangu Kamati ianze kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais. Kamati hii pamoja na kazi zake nyingine ilitembelea miradi mbalimbali ya kupambana na umaskini na ya hifadhi ya mazingira. Kamati pia ilichambua makadirio ya mafungu 26 na 31 Ofisi ya Makamu wa Rais na kuyatolea maoni na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makamu wa Rais ana majukumu mahsusi ya kitaifa ya kumsaidia na kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya nchi kwa ujumla. Ofisi ya Makamu wa Rais pia inaratibu shughuli za Muungano, juhudi za kuondoa umaskini nchini, inasimamia utekelezaji wa sera ya mazingira, pamoja na kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) na Jumuiya za Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi na tunahitimisha kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Tatu, napenda kuungana na wenzangu kueleza mafanikio makubwa tuliyojipatia chini ya uongozi imara na shupavu wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa utaratibu kama wa mwaka jana, nitaelezea utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2004/2005, kazi muhimu zitakazotekelezwa na makadirio ya matumizi kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua sote Muungano wetu umetimiza miaka 41 tangu kuundwa. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hicho. Katika hotuba yangu nitazungumzia mafanikio katika kipindi tajwa kama ifuatavyo:-

Sheria ya Uraia, Sheria Na. 6 ya mwaka 1995 ilitungwa ambapo imefuta sheria zote zilizokuwa na utata katika utekelezaji wa masuala ya uraia katika Muungano wetu. Suala la Uhamiaji lilifanyiwa kazi kwa kutunga Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 ambayo imewezesha Watanzania kuingia au kutoka pande zote za Muungano bila vikwazo vyovyote.

Chombo cha Usalama wa Taifa kiliundwa chini ya Sheria Na. 15 ya mwaka 1996 ambayo inasimamia usalama katika pande zote za Muungano. Jitihada hii

imewezesha kuwa na Watumishi wa Usalama wa Taifa wanaotoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sheria Na. 1 ya 1995 ilitungwa ili kuboresha masuala yahusuyo sarafu na matumizi yake, fedha na mabenki. Aidha, Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Na.14 ya mwaka 1996 ilitungwa na wajumbe wa Tume wameteuliwa mwaka 2003. Tume ya Pamoja ya Fedha imefungua Ofisi zake pande zote mbili (SMT na SMZ) ili kutoa huduma kikamilifu. Watumishi katika Ofisi hizo wameajiriwa na shughuli za Ofisi zimeanza. Hadi sasa jumla ya vikao 11 vya Tume ya Pamoja ya Fedha na vikao 10 vya Sekretarieti vimekwishafanyika. Semina kwa wajumbe wa Tume na Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Asasi zinazoshughulikia masuala ya kifedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilifanyika. Semina hizi zimekuza uelewa wa watumishi wa Tume katika masuala ya kifedha. Ili kuboresha mgawanyo wa mapato, tayari mtaalaam amekwishapatikana kwa ajili ya kuchambua vigezo vya kugawana mapato. Mtaalamu huyu anatarajia kuanza kazi wakati wowote, na kutoa mapendekezo ya taratibu zitakazotumika kugawana mapato kwa Serikali zote mbili ili kuleta maendeleo kwa Taifa letu. Tume pia ilifanya mapitio ya Sheria No. 14 ya 1996 na kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo Serikalini. Tume imechambua madeni baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuweka taratibu za kulipa madeni hayo.

Hivi sasa, utaratibu wa SMZ kupata gawio la asilimia 4.5 la faida ya Benki Kuu pamoja na mikopo na misaada inayotolewa na wafadhili kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania umewekwa na unatekelezwa na Serikali. Katika kipindi hiki Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefungua akaunti Benki Kuu ambapo imeendelea kupata huduma za Benki Kuu kupitia Tawi la Benki Kuu lililofunguliwa Zanzibar.

Halikadhalika, Benki ya Dunia, *ADB*, na *UNDP* wameanza kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza Mpango wa Kupambana na Umaskini (*ZPRP*). Tatizo la Wafadhili kusitisha misaada kwa Zanzibar limepata ufumbuzi na misaada hiyo kwa sasa inapatikana. Aidha, jitihada za kupanua huduma za mikopo midogo Zanzibar zinaendelea. Tangu mradi wa *SELF* uanze Zanzibar hadi sasa Asasi 6 za kifedha zimepatiwa mikopo kwa ajili ya kuitoa kwa vikundi mbalimbali kuendeshea biashara ndogondogo.

Huduma nyingine kubwa iliyotolewa Tanzania Zanzibar ni ya Mfuko wa *TASAF*. Mafanikio makubwa yamepatikana, na kuwezesha miradi ya jamii 28 Pemba na 33 Unguja kuanzishwa na kukamilika. Miradi ya jamii ilijumuisha elimu, maji, afya na miundo mbinu ya kiuchumi. Miradi mingine iliyoanzishwa na kukamilika ni ya ujenzi kama vile ujenzi wa barabara za vijijini, mabwawa ya umwagiliaji, na kadhalika. Pemba miradi 5 na Unguja miradi 6.Utaratibu wa kutunga Sheria zinazohusu mambo ya Muungano umerekebishwa na kwamba Miswada yote inatolewa siku 21 kabla haijawasilishwa Bungeni. Hii inatoa fursa kwa Wabunge wa pande zote mbili za Muungano kuchangia maoni kuboresha Miswada hiyo.

Suala la Elimu ya Juu linaendelea kusimamiwa na kuratibiwa na Wizara ya Sayansi na Teknolojia nchini kwa kushirikisha pande zote za Muungano ambapo kituo cha utafiti wa Viumbe vya Bahari kilichopo Zanzibar kimepanua shughuli zake na kinatoa shahada mbalimbali. Aidha, kwa sasa hivi kituo kinapanuliwa ili kuhudumia Afrika Mashariki na baadaye nchi za *SADC*.

Hatua zimechukuliwa kuimarisha sekta ya Usafiri na Usafirishaji wa Anga ikiwa ni pamoja na kuboresha uwanja wa Ndege wa Zanzibar hivyo kuruhusu kutua Ndege kubwa, pia, kuruhusu mashirika ya watu binafsi kuendesha biashara ya Usafiri na Usafirishaji wa Anga. Katika kipindi hiki tumeshuhudia demokrasia ya hali ya juu ambapo idadi ya vyama vya Siasa nchini imeongezeka kutoka vyama 13 mwaka 1995 hadi 18 kwa mwaka 2005 na vinafanya shughuli zao halali bila kubughudhiwa na mtu yoyote. Aidha, chaguzi mbalimbali zimefanyika kwa amani ikiwa ni pamoja na uchaguzi wa serikali za mitaa. Katika kuimarisha Demokrasia Serikali iliandaa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambapo litaanza kutumika rasmi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Kwa upande wa masuala yasiyo ya Muungano Serikali zote mbili chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, zimejiwekea utaratibu wa kuwa na vikao vya kisekta vya mashirikiano. Wizara na Asasi zilizofanya vikao hivyo vya mashirikiano ni kama ifuatavyo; Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto (SMZ) na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto(SMT), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (SMZ) na Wizara ya Afya (SMT), Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba (SMT) na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora, Wizara ya Kilimo, Mazingira na Ushirika SMZ na Wizara ya Kilimo na Chakula (SMT), Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo (SMZ) na Wizara ya Elimu na Utamaduni (SMT), Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo (SMT) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (SMZ), n.k. Vikao hivi hufanyika angalau mara mbili kwa mwaka. Katika vikao hivi masuala mbalimbali yanayohusu Sera, kubadilishana utaalamu na wataalamu, ushiriki katika masuala ya Kitaifa na Kimataifa, utafiti, na ziara za mafunzo. Kufanyika kwa vikao hivi kumekuza ushirikiano kati ya pande hizi za Muungano katika kuandaa mikakati na programu mbalimbali kama vile Mpango wa Kupunguza Umaskini Zanzibar, Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa Tanzania Bara na Mkakati wa Kupambana na UKIMWI.

Miradi imeanzishwa Tanzania Zanzibar kama vile:- Ujenzi wa Ofisi za Bunge, Ujenzi wa Ofisi za Benki Kuu ya Tanzania na ujenzi na upanuzi wa Kituo cha Utafiti wa Viumbe vya Baharini. Ofisi nyingine zilizofungua Ofisi Tanzania Zanzibar ni Tume ya Pamoja ya Fedha, Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Tume ya Mawasiliano na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kufunguliwa kwa Ofisi hizi kumeimarisha Muungano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba mazingira ni ajenda pana na yenye umuhimu mkubwa katika kutimiza lengo kuu la Taifa la kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Kwa sababu hii, Serikali imechukua hatua mbalimbali za hifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuweka sera madhubuti za kusimamia

hifadhi ya mazingira na kupitisha sheria, mikakati, programu pamoja na miradi ya utekelezaji wa sera hizi. Aidha Bunge, kwa mara ya kwanza, mwaka jana, limepitisha Sheria ya Mazingira ambayo imeweka mfumo wa kisheria wa hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Shughuli nyingi za uhamasishaji wa umma kuhusu hifadhi ya mazingira zimeendeshwa na katika kufanya hivi, taasisi zisizo za Serikali, sekta binafsi na wananchi katika vikundi mbali mbali wameshirikishwa na wameendelea kuonesha ari ya kushirikiana na Serikali katika jukumu hili pana na muhimu la hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali wa kuipa dhana ya mazingira hadhi ya kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ulikuwa ni uamuzi muhimu sana na umewezesha mafanikio makubwa katika usimamizi wa Mazingira nchini. Sera ya Taifa ya Mazingira ilipitishwa mwaka 1997 na kuwa nguzo muhimu katika juhudi za serikali za kupambana na uharibifu wa mazingira. Hii ilifuatiwa na mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira uliopitishwa mwaka 2002 na kama nilivyosema awali, Sheria ya Mazingira ilipitishwa na Bunge hili tukufu Novemba mwaka jana. Mifumo na misingi hii muhimu imeweza kuleta mafanikio mbalimbali yafuatayo:

Kuwa na miongozo mbalimbali ya kusaidia wananchi ikiwa ni pamoja na wawekezaji katika kufanya shughuli zao za kujiendeleza kiuchumi bila kuharibu mazingira. Miongozo hiyo ni pamoja na; miongozo ya tathmini ya athari kwa mazingira (*EIA guidelines);* miongozo ya kujumuisha (*mainstream*) suala la mazingira katika mipango ya maendeleo ya kisekta; miongozo ya kuainisha uhusiano wa mazingira na umasikini na kuingiza masuala ya mazingira katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); miongozo ya kushiriki katika miradi ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi; miongozo ya matumizi salama ya baiotekinolojia ya kisasa; na miongozo ya utaratibu wa kupeana taarifa juu ya biashara ya kimataifa ya kemikali hatari na madawa ya kuulia wadudu. Serikali pia imeandaa mikakati na miongozo ya kuhifadhi na kusimamia maeneo mbalimbali, kwa mfano mkakati wa uwiano wa kuhifadhi maeneo ya pwani na bahari, miongozo ya ufugaji endelevu wa samaki katika mwambao wa pwani na miongozo ya utalii endelevu katika maeneo ya pwani. Aidha, miongozo ya usimamizi wa taka za hospitali imeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya; na nyenzo za kiuchumi kwa ajili ya usimamizi wa hifadhi ya mazingira nchini pia zimeandaliwa.

Chini ya Mkataba wa Bioanuwai, Serikali imetekeleza miradi mikubwa ya kupambana na matatizo ya mazingira ikiwa ni pamoja na mradi wa kupambana na tatizo la mazingira katika eneo la Ziwa Victoria. Chini ya mradi huu, tangu mwaka 1997, mafanikio yafuatayo yamepatikana: Asilimia 90 ya magugumaji yaliyokuwa kero kwa wananchi na mazingira ya Ziwa Victoria, yamedhibitiwa kwa kushirikiana na wananchi; Miradi midogo midogo 76 inayohusu visima vya maji safi, zahanati, uvuvi na ujenzi wa madarasa imetekelezwa. Zaidi ya Vikundi 500 vya wananchi vimeanzishwa ili kusimamia maendeleo, usalama na usafi wa mialo na mazingira kwa ujumla; na wakulima waishio katika maeneo yanayozunguka ziwa hasa katika wilaya za Magu na Tarime wamepewa ujuzi wa kuvuna maji na kuzuia mmomonyoko wa udongo na hivyo kuinua uzalishaji wa mazao na kipato. Aidha, Miche ya miti milioni kumi (10,000,000)

imepandwa katika Mkoa wa Mara. Vilevile, Programu ya Hifadhi ya Ziwa Tanganyika imeendelea kutekelezwa ambapo mkataba wa usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika wa mwaka 2003 unaozihusu pia nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Zambia, uliridhiwa na Tanzania mwaka 2004.

Mkataba wa Vienna unaohusu kulinda Tabaka la Hewa ya Ozoni angani na wa mwaka 1985 na Itifaki yake ya *Montreal* inayohusu kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni, ya mwaka 1987 uliendelea kutekelezwa. Mafanikio ni pamoja na: kupatiwa msaada wa mitambo mipya isiyotumia kemikali zinazoharibu ukanda wa Ozoni katika viwanda vya *Ply Foam* na *Pan Africa Enterprises* vya Dar es Salaam na Mwanza vinavyotengeneza bidhaa za sponji na kiwanda cha *Mansoor* Daya kinachotengeneza madawa ya kupuliza *aerosols* kilichopo Dar es Salaam. Aidha, makampuni mengine 20 yamepata msaada wa mitambo ya kunasa na kurejeleza kemikali za *Chlorofluorocarbons (CFCs)* zilizoko kwenye mitungi ya majokofu na viyoyozi. Mafunzo kwa mafundi mchundo 30 na wadau wengine yamefanyika juu ya njia bora za kusafisha, kuhifadhi na kurejesha kemikali hizi. Mitambo hii imewezesha Tanzania kupunguza matumizi ya kemikali hizo kwa kiasi cha asilimia sitini.

Utekelezaji wa Mkataba wa *Basel* ambao unahusu udhibiti wa utupaji wa taka za sumu na usafirishaji wake baina ya nchi na nchi (1989) ulileta mafanikio yafuatayo; Kituo cha Tekinolojia na Uendeshaji Endelevu wa viwanda (*CPCT*) kilianzishwa mwaka 1995 ili kusaidia viwanda na sekta nyingine kutekeleza dhana ya uzalishaji bora yenye lengo la kuongeza tija, ufanisi na kupunguza uchafuzi wa mazingira. Kituo hiki, kimetoa mafunzo kwa wataalamu takriban 100 juu ya mbinu za uzalishaji bora katika viwanda 47 vya Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Mwanza, Jiji la Tanga, Jiji la Arusha, Manispaa za Morogoro, Moshi, na Unguja na mji wa Pemba.

Aidha, utekelezaji wa Mkataba wa *Stockholm* unaohusu udhibiti wa kemikali hatari zinazochukua muda mrefu kuoza (*Persistant Organic Pollutants)* uliwezesha utambuzi wa tani 1,200 za kemikali chakavu za kilimo ambazo zitasafirishwa kwenda nje ya nchi ili kuangamizwa kwa kutumia tekinolojia mahsusi kwa taka za aina hii. Mikakati ya kudhibiti madhara ya kemikali hizi imeandaliwa;

Chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, *(UNCCD),* wa mwaka 1997, juhudi za kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame hasa katika maeneo kame zimehusisha serikali kuu, serikali za mitaa na vikundi vya kijamii. Kupitia miradi mbalimbali na kwa kuhusisha vikundi vya kijamii zaidi ya 20, serikali imeweza kusaidia katika shughuli zifuatazo: juhudi za kupambana na uchomaji moto ovyo; ukataji miti kiholela; na upatikanaji wa nishati jadidifu za biogas na jua. Shughuli hizi zilitekelezwa katika maeneo ya Iyumbu (Dodoma), Uluguru (Morogoro), Bonde la Chipite (Masasi) na Bonde la Usangu; na wilaya 13 za Mikoa ya Mwanza, Singida na Shinyanga. Aidha, Miti zaidi ya 380,000,000 imepandwa katika mikoa ishirini (20) ya Tanzania bara. Idadi hii ni asilimia tisini na sita (96%) ya lengo lililowekwa katika mikoa yote tangu mwaka 2000. Kutokana na madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi kwa Tanzania, chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*UNFCCC*) wa mwaka 1992 na Itifaki ya Kyoto ya mwaka 1997, Serikali imeanisha sekta za kipaumbele, mikakati ya kukabiliana na madhara ya

mabadiliko ya tabianchi; na tekinolojia zinazotakiwa kutumika katika sekta mbali mbali kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 1997, programu ya mazingira na maliasili yenye lengo la kukuza ushiriki wa wananchi katika shughuli za usimamizi wa hifadhi ya mazingira, kujenga uwezo wa serikali za mitaa, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kupanga na kutekeleza shughuli za hifadhi ya mazingira imeendelea kutekelezwa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara na hifadhi ya akiba ya Ugalla; kujenga zaidi ya kilometa 300 za barabara katika hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara; kukarabati barabara kuu ya watalii *(main tourist viewing road circuit)* katika hifadhi ya Manyara; kujenga kituo cha habari kwa Setelaiti *(GIS Center)* katika hifadhi ya Taifa ya Tarangire; kujenga vituo viwili vya kutoa maelezo kwa wageni (*visitors centers*) katika hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara; na kukarabati Mitambo ya uchapishaji ya *TANAPA* Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa msaada wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(GEF),* imeweza kutekeleza miradi mbalimbali ya mazingira na kupambana na umaskini kupitia vikundi vya jamii katika nchi nzima, ikiwa ni pamoja na Zanzibar. Zaidi ya vikundi 54 vimesaidiwa ambapo jumla ya shillingi zaidi ya bilioni moja na milioni mia nne zimetumika. Maeneo ya kipaumbele katika miradi hii midogo midogo ni; ujenzi wa visima vya maji hasa katika maeneo kame; upandaji miti; upatikanaji wa nishati mbadala; kilimo cha umwagiliaji; na usafi wa mazingira mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukuza weledi na elimu ya mazingira, Serikali imeendesha mafunzo mbalimbali na kusambaza taarifa kwa wadau kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira. Kwa mfano, taarifa kuhusu dhana ya uzalishaji bora viwandani; taarifa kuhusu utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya mazingira; taarifa kuhusu miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia; na kukuza weledi kuhusu uhusiano wa mazingira na umaskini.

Taarifa nyingine zinazohusu mazingira ni pamoja na taarifa ya hali ya mazingira ya pwani na uwezo wa mito iliyopo Mwanza (Mabubi na Nyashishi) na Kagera (Ngono) katika uchujaji wa uchafu katika bonde la Ziwa Victoria. Vile vile elimu imetolewa kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla ili kukuza ufahamu kuhusu umuhimu wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) katika kupunguza athari za shughuli za maendeleo katika mazingira na afya za viumbe hai ili kuleta maendeleo endelevu. Kutokana na elimu hii miradi mingi imefanyiwa TAM na hasa imehusisha sekta za uchimbaji madini, ujenzi wa madampo ya taka, viwanda vya minofu ya samaki, ufuaji umeme, shughuli za kilimo, ujenzi wa machinjio, ujenzi wa barabara, ujenzi wa mahoteli na vivutio vya kitalii, viwanda vya nguo na bohari za madawa. Aidha, kitabu cha mafunzo ya TAM kinacholenga kukuza weledi kwa watumishi wa ngazi ya halmashauri na kuongeza elimu ya uratibu na uanishaji wa masuala ya mazingira katika mipango ya halmashauri za wilaya, miji na manispaa imeandaliwa. Vile vile mafunzo ya majaribio kwa matumizi ya kitabu hiki *(Pilot EIA Training)* yamefanyika kwa halmashauri za Rufiji na Bagamoyo, na Manispaa ya Ilala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji na mwamko wa wananchi na taasisi katika hifadhi ya mazingira umeedelea kukua kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, serikali inaadhimisha siku ya mazingira duniani kila mwaka ambapo pia shule, vijiji na vikundi mbalimbali vya jamii hushiriki kikamilifu kwenye mashindano ya kuhifadhi mazingira. Mashindano ya miji na manispaa mbalimbali katika usafi wa mazingira hufanyika wakati wa maadhimisho ya siku hii. Aidha, Tuzo ya Rais ya ubora wa utunzaji mazingira katika uchimbaji madini iliyoanzishwa na Mhe. Rais mwaka 2000 imeendelea kutolewa kwa wawekezaji wakubwa na wadogo katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo sugu la taka za aina mbali mbali, serikali kwa ushirikiano na Shirika la Viwanda la Umoja wa Mataifa (*UNIDO*), imeanzisha kituo cha majaribio cha kurejeleza taka za plastiki na taka za aina nyingine jijini Dar es Salaam. Mafanikio ya kituo hicho cha majaribio yataiwezesha serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, kusambaza vituo hivyo kote nchini ili kurejeleza taka zitokanazo na plastiki hasa chupa na mifuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria mpya ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 Baraza limepewa majukumu ya kusimamia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kupitia na kudhibiti tathmini ya athari kwa mazingira, kuratibu utafiti pamoja na kuhakikisha ushirikishwaji wa jamii katika maamuzi yanayohusu usimamizi na hifadhi ya mazingira. Sheria inalipa Baraza kwa kushirikiana na sekta zote, mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala ya mazingira na kuwachukulia hatua za kisheria wanaoharibu au kuchafua mazingira. Kutokana na hilo, serikali itahakikisha Baraza linapewa nyenzo ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha awamu ya Tatu Baraza lilitoa mchango wa kitaalamu katika kuandaa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na uandaaji wa Sheria ya Mazingira. Aidha, katika kipindi hicho Baraza lilijishughulisha na elimu kwa umma ambayo imeongeza weledi wa wananchi katika suala zima la hifadhi ya mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingra, Baraza lilitoa ushauri kwa viwanda mbalimbali kuhusu udhibiti wa uchafuzi katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Arusha na Mwanza. Kwa upande wa Dar es Salaam uchafuzi sugu wa Kiwanda cha Saruji Wazo ulipunguzwa. Katika kipindi hicho, Baraza lilisimamia miradi mbalimbali ya mazingira. Baadhi ya miradi hiyo, ni mradi wa Bioanuwai wa Afrika Mashariki, mradi wa Hifadhi ya Pwani na Bahari (*TCMP*) na mradi wa kuhifadhi mazingira nyeti ya vyura wa Kihansi (*LKEMP*).Aidha Baraza liliendelea, kusimamia na kutekeleza majukumu yanayohusiana na mchakato wa Tathmini ya Athari kwenye Mazingira *(TAM)* hususan katika nyanja za kuelimisha wadau juu ya umuhimu wa *TAM*. Elimu hii imetolewa kwa wawekezaji na wananchi kwa ujumla na imekusudia kukuza ufahamu kuhusu umuhimu wa TAM katika kupunguza athari za shughuli za maendeleo katika mazingira na afya za viumbe hai na kuleta maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume na miaka ya nyuma, miradi mingi iliyoanzishwa katika kipindi hicho ilifanyiwa *TAM;* miradi iliyofanyiwa TAM inahusu: uchimbaji madini, ujenzi wa madampo ya taka, viwanda vya minofu ya samaki, ufuaji umeme, shughuli za kilimo, ujenzi wa machinjio, ujenzi wa barabara, ujenzi wa mahoteli, na vivutio vya kitalii, viwanda vya nguo na bohari za madawa. Ushauri wa kitaalam katika hatua za awali za mchakato wa *TAM (Screening and Scoping level)* uliotolewa kwa wawekezaji katika maeneo mbalimbali ya uchumi ni pamoja na: ufugaji wa kamba na chaza, ujenzi wa ghati Mafia na umeme wa gesi Mtwara. Aidha Baraza lilifanya mapitio (*review*) ya taarifa za *TAM* zaidi ya 150 na kutoa ushauri wa kuziboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza limetengeneza rasimu ya kitabu cha mafunzo ya TAM. Kitabu hiki kinalenga kukuza weledi kwa watumishi wa ngazi ya halmashauri na kuongoza masuala ya mazingira katika mipango ya halmashauri za wilaya, miji na manispaa.

Aidha Baraza liliendelea na utayarishaji wa miongozo ya *TAM* ya sekta kwa kushirikiana na sekta husika *(Sectoral Envirnmental Guidelines).* Kwa mfano sekta ya barabara, rasimu yake imekamilika. Kwa sekta za kilimo na mifugo rasimu ya mwongozo imo katika hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mojawapo ya utekelezaji wa mkakati wa uwiano wa kuhifadhi na kusimamia maeneo ya pwani na Bahari pamoja na wa kupambana na umaskini; Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya za Bagamoyo, Pangani na Mkuranga limefanikiwa kutayarisha Mpango wa uwiano wa uhifadhi wa maeneo ya pwani na bahari na kuanza kuutekeleza. Vile vile, Baraza kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi limekamilisha uandaaji wa mwongozo wa ufugaji endelevu wa viumbe bahari (*aquaculture*) katika mwambao wa pwani na kusambaza miongozo hiyo kwa wadau; na limeshirikiana na sekta husika kutayarisha mwongozo wa utalii endelevu katika maeneo ya pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza lilifanya tafiti kadhaa na kusambaza taarifa mbalimbali zinazohusu mazingira kwa ujumla. Taarifa muhimu ambazo zimetolewa kwa kipindi hiki ni pamoja na Hali ya Mazingira ya Pwani na Uwezo wa Mito ya Mabubi (Mwanza) Ngono (Kagera) na Nyashishi (Mwanza) katika uchujaji wa uchafu katika bonde la Ziwa Victoria. Elimu ya mazingira katika ngazi mbalimbali iliendelea kutolewa kwa nia ya kukuza weledi wa mazingira.

Aidha, kongamano la kwanza la kitaifa la kisayansi kuhusu mahusiano kati ya uhifadhi wa mazingira, kilimo endelevu na kupambana na umaskini lilifanyika kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza liliwahamasisha wananchi katika maeneo oevu kuanza kutayarisha mikakati ya kuhifadhi maliasili katika maeneo hayo. Hatua za awali za kutayarisha mikakati ya kuhifadhi maeneo oevu ya Kitaji (Musoma) Rubana (Bunda),

Nyashishi (Misungwi/Mwanza) Simiyu (Magu) na Mabubi (Geita) zimepiga hatua ya kuridhisha. Pia mashindano ya kuhifadhi mazingira kwa shule, vijiji na vikundi vya mwambao wa Ziwa Victoria, Pwani ya Bahari ya Hindi na kwingineko nchini yaliandaliwa ili kushirikisha wananchi wengi zaidi katika shughuli za kutunza mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tumesikia mafanikio ya sekta mbalimbali kwenye hotuba za Mawaziri walionitangulia yaliyowezesha uchumi wa Taifa kukua kufikia asilimia 6.7 mwaka 2004 kutoka asilimia 4.7 mwaka 2000, na asilimia 3.6 mwaka 1995. Hii ni historia kwa nchi yetu kufikia kiwango hiki na ni dalili ya kuendelea kuimarika kwa uchumi wetu. Aidha, kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita uchumi unaonekana kukua mara mbili kwa wastani. Ina maana kwamba tukiendelea kwa kasi hiyo, kipindi cha miaka 10 ijayo uchumi wa Taifa utakuwa umekua kwa wastani wa asilimia 13 ambayo ingetuwezesha kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliungana na Jumuiya ya Kimataifa mwaka 1995 kule Copenhagen katika kuweka upya dhamira ya kuutokomeza umaskini nchini na duniani kote.

Hali kadhalika, katika Mkutano wa Millennia uliofanyika *New York* 2000, Tanzania iliungana na Mataifa yote ya ulimwengu katika kutilia mkazo dhamira ya kuutokomeza umaskini kwa nusu ifikapo mwaka 2015, na kuundoa kabisa ifikapo mwaka 2025.

Maamuzi hayo yalifanyika kufuatia dosari zilizojitokeza katika kipindi cha marekebisho ya uchumi ambapo mkazo uliwekwa katika kuweka misingi ya kukua kwa uchumi bila kuzingatia haja ya kuwashirikisha wadau wote katika ukuaji wa uchumi (ambayo yalizaa mikakati mbalimbali ya kupambana na umaskini kuanzia mwaka 1995). Mambo ya msingi yaliyobainishwa katika vita dhidi ya umaskini ni pamoja na:-

Kukuza uchumi unaoshirikisha watu wengi (kuzingatia shughuli zinazofanywa na wadau mbalimbali kama vile wakulima wadogo, wafanya biashara wadogo, viwanda vidogo na vya kati na kadhalika.):

(i) Kuendeleza huduma muhimu za kijamii na kiuchumi;

(ii) Kuweka mazingira mazuri ya umilikaji wa uchumi yanayovutia wawekezaji;

(iii) Kuwa na usimamizi mzuri wa hifadhi ya mazingira kwa maendeleo endelevu;

(iv) Kuimarisha miundo mbinu hasa barabara na mawasiliano;

(v) Utawala bora (vita dhidi ya rushwa, demokrasia, uwazi, uwajibikaji, na ushirikishwaji wa wadau); na

(vi) Kuwa na Mfumo imara wa ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka kumi ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzishwa kwa Idara ya Kuondoa Umaskini katika Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 1995. Lengo kuu la kuanzisha Idara hii ni kuratibu na kusimamia jitihada za kupunguza umaskini, ili kuleta mafanikio kwa haraka zaidi.

(ii) Kuandaliwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo inayolenga kuwa na jamii ya Kitanzania iliyoondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025.

(iii) Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau wengine mwaka 1998 iliandaa Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Kuondoa Umaskini, kwa lengo la kupunguza umaskini uliokithiri kwa nusu ifikapo mwaka 2010 na kuuondoa kabisa ifikapo mwaka 2025. Aidha, juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuleta maendeleo ziliimarisha misingi ya ukuaji wa uchumi na kujenga imani kwa wafadhali na hivyo kufanikiwa kusamehewa baadhi ya madeni yake. Chini ya mpango wa msamaha wa madeni, Mkakati wa Kupunguza Umaskini *(Poverty Reduction Strategy - PRS)* uliandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali, ukilenga kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliandaa Mpango wa Kupunguza Umaskini *(ZPRP)* kama hatua ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (Vision 2020).

(iv) Jitihada pia zilifanyika kuandaa Mkakati wa Misaada wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2002 *(Tanzania Assistance Strategy – TAS)* unaolenga kuboresha usimamizi wa misaada ili kuelekeza misaada ya wafadhili katika maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Mafanikio ya mkakati wa misaada yamewezesha kuanza maandalizi ya hatua ya juu zaidi ya kuandaa mkakati wa pamoja wa wafadhili *(Joint Assistance Strategy).*

(v) Mpango wa ufuatiliaji wa jitihada za kupambana na Umaskini *(Poverty Monitoring Master Plan)* uliandaliwa mwaka 2001. Lengo ni kupima mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini, kubaini mapungufu na kuchukua hatua za makusudi kuharakisha kasi ya kuondoa umaskini. Kupitia mfumo wa ufuatiliaji *(poverty monitoring system)* uchambuzi na tafiti mbalimbali umefanyika na kuonesha kuwa:-

Idadi ya watu wanaoishi katika umaskini imepungua kutoka asilimia 38.6 ya mwaka 1991/92 na kufikia asilimia 35.3 mwaka 2000/01 na idadi ya wanaoishi katika umaskini uliokithiri imepungua kutoka asilimia 21.6 katika mwaka 1991/92 na kufikia asilimia 18.7 katika mwaka 2000/01, kama inavyoonyesha katika utafiti wa Mapato na Matumizi ya *Kaya (Household Budget Survey).*

(vi) Aidha, bajeti ya Serikali ni nyenzo muhimu katika juhudi za Serikali za kupambana na umaskini. Mafanikio ya kukua kwa uchumi yamechangia kuboresha bajeti ya serikali yenye lengo la kuongeza ufanisi katika sekta za kipaumbele. Kiasi cha fedha zilizotolewa katika sekta za kipaumbele ili kupiga vita umaskini, kiliongezeka kila mwaka kuanzia mwaka 2001, na kutuwezesha kufikia malengo tuliyojiwekea.

(vii) Taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Kuondoa Umaskini (*PRSP*), za kila mwaka (*Annual Progress Reports)* ziliandaliwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2000. Ripoti hizi zimetoa maelezo ya kina ya utekelezaji katika sekta za kipaumbele zilizoainishwa ambazo ni: kilimo, elimu ya msingi, barabara za vijijini, maji safi na salama, afya, na sheria. Pia zimetoa maelezo ya kina ya utekelezaji wa mambo ya jumla yanayogusa sekta zote ikiwemo: mkakati wa maendeleo vijijini, mazingira, mapambano dhidi ya UKIMWI, jinsia, utawala bora, ukuzaji wa ajira, uboreshaji wa serikali za mitaa na maendeleo ya rasilimali watu. Aidha, bajeti ya Serikali ilitoa upendeleo kwa shughuli za kupambana na umaskini katika sekta za kipaumbele ziliainishwa. Ripoti hizi zinapatikana katika tovuti ya Taifa ya *http://www.tanzania.go.tz* na ya Ofisi ya Makamu wa Rais *www.povertymonitoring.go.tz.*

(viii) Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu *(Poverty and Human Development Report–PHDR)* ya mwaka 2002 na 2003 ziliandaliwa. Ripoti ya mwaka 2002 ilichapishwa kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu. Ripoti hizi huchambua kwa kina hali ya umaskini nchini, tofauti za kijiografia, uhusiano kati ya masuala ya kimataifa na ya kitaifa na hatari mbalimbali zinazoweza kuwakabili watu na kusababisha umaskini (*vulnerability*).

(ix) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) uliandaliwa na kupitishwa na Serikali mwezi Februari 2005. Huu ni mpango wa awamu ya pili wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU/PRSP) ulioandaliwa mwaka 2000 chini ya mpango wa msamaha wa madeni kwa nchi maskini sana duniani. Lengo kubwa la kufanya mapitio lilikuwa kubaini mapungufu na kuboresha Mkakati ili uweze kuleta mafanikio zaidi kwa wananchi na kuhakikisha kuwa uchumi unaendelea kukua kwa kasi zaidi, na hivyo kuiwezesha Tanzania kufikia malengo yaliyobainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kasi ya kupunguza umaskini, Serikali ilibuni miradi na programu zilizozingatia jinsia na UKIMWI, kuunga mkono nguvu za wananchi katika kupambana na umaskini. Miradi na programu nyingi zimeanzishwa kama vile: Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(Tanzania Social Action Fund - TASAF),* Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo (Small Entrepreneurs Loan Facility – SELF), Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato *(National Income Generation Programme - NIGP)*, na Mpango wa Kurasilimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) n.k. Dhana ya MKURABITA au *Property and Business Formalization Programme – (PBFP)* ni ushirikishwaji wa Watanzania walio wengi katika mfumo wa kitaifa wa umilikaji mali na uendeshaji biashara kama njia mojawapo ya kupiga vita umaskini na hivyo kuboresha maisha. Mipango ya programu hizi inazingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika MKUKUTA na kudhihirishwa zaidi katika mipango ya ki-sekta kama vile marekebisho ya sheria za ardhi, biashara, viwango, uboreshaji wa mazingira, usawa wa jinsia, kuinua ubora wa maisha ya watu na hivyo kujipatia maendeleo ya jamii yaliyo endelevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) kama moja ya mikakati yake ya kuondoa umaskini na kuchangia kufikiwa kwa malengo ya Mkakati wa Kuondoa Umaskini uliobuniwa mwaka 2000. Lengo lake kuu lilikuwa kushughulikia mahitaji ya wananchi waishio vjjijini na pembezoni mwa miji ili kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii. Msingi mkubwa wa mafanikio katika Mradi huu umekuwa ni wananchi wenyewe ambao kwa njia shirikishi jamii wamekuwa wabunifu, wapangaji, watekelezaji na wasimamizi wa utekelezaji wa miradi waliyoianzisha. Halmashauri za Wilaya zimekuwa zikitoa msaada wa kiufundi kwa wananchi ili watekeleze miradi yao kwa viwango vinavyokubalika na sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwake, *TASAF* imewasaidia wananchi kutekeleza miradi ambayo imechangia kupunguza pengo katika utoaji wa huduma za jamii kama elimu, afya, maji na kuwasaidia wananchi kuinua kipato chao. Jumla ya miradi 1704 imetekelezwa tangu kuanzishwa kwa mfuko huu. Miradi hiyo imewezesha upatikanaji wa miundombinu ambayo inachangia kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii kwa wananchi waishio vijijini. Mafanikio haya ni kama yafuatayo:-

(i) Miradi ya huduma za Jamii imeongeza na/au kuboresha madarasa 2,586, ofisi za walimu 468, nyumba za walimu 335, maabara za shule za sekondari 18, majengo ya utawala katika shule za sekondari 26, mabweni ya wanafunzi 13, vyoo vya wanafunzi 951; zahanati 312, nyumba za watumishi wa zahanati 922, vyoo 613, vichomea taka 304; mifumo ya maji 70, visima 559; barabara 5 za urefu wa kilomita 85, masoko 4; mifumo midogo ya umwagiliaji 2 na ofisi 1 ya kijiji.

(ii) Miradi ya ujenzi imeongeza/ imeboresha barabara za vijijini 204, hifadhi ya mazingira (misitu) 29, masoko 16, vituo vya mabasi 3, miundombinu ya umwagiliaji maji 11 na daraja 1 la watembea kwa miguu.

(iii) Miradi ya makundi maalum imetoa huduma kwa yatima 1,262, wajane 875, wazee 472 na watoto chini ya miaka mitano 57 kupitia miradi ya uzalishaji mapato katika wilaya 4 za majaribio. Vilevile, uhamasishaji juu ya kudhibiti UKIMWI umetolewa kwa watu 30,015.

(iv) Pia, mafunzo juu ya kusimamia uendeshaji wa miradi yametolewa kwa watu 22,230 na wengine 732 wamepewa mafunzo katika fani mbalimbali katika ngazi ya wilaya na taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu iliyopatikana na mafunzo yaliyotolewa kwa walengwa kupitia *TASAF* vimechangia kuondoa umaskini kama ifuatavyo:

(i) Katika sekta ya elimu, msongamano wa wanafunzi katika madarasa umepungua na wanafunzi wamepata mazingira mazuri ya kusomea. Aidha, walimu wamepata mahali pazuri pa kuishi na kuwapunguzia usumbufu wa kuishi mbali na shule na hivyo kuwa na nafasi ya kufanya kazi kwa ufanisi. Yote haya yanachangia kuboresha kiwango cha elimu nchini.

(ii) Katika sekta ya afya, ujenzi wa zahanati umerahisisha upatikanaji wa huduma za afya karibu zaidi na wananchi hasa huduma kwa wanawake na watoto.

(iii) Katika sekta ya maji, miundo mbinu iliyowekwa imepunguza muda wa upatikanaji wa maji na hivyo kuwaondolea usumbufu wanawake. Kwa njia hiyo, muda unaotumika katika shughuli zingine za uzalishaji umeongezeka, magonjwa ya kuambukiza kama kuhara na kipindupindu yamepungua katika jamii zilizopata huduma hii.

(iv) Ujenzi wa barabara vijijini umechangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la kipato cha wakazi wa maeneo ambayo barabara hizo zinapita. Wananchi wanaweza kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko yaliyo nje ya maeneo yao na hata wafanyabiashara kutoka nje wanakwenda kununua mazao katika vijiji hivyo. Aidha, wananchi wana uwezo wa kufuata huduma nyingine kama za matibabu katika sehemu zingine ambazo kabla ya hapo hawakuwa na uwezo wa kuzifikia.

(v) Miundombinu ya kiuchumi na miradi ya umwagiliaji inachangia kukua kwa kipato, kuboresha lishe na kupunguza tatizo la ukosefu wa chakula kwa wananchi. Kwa njia ya kilimo cha umwagiliaji, kiwango cha uzalishaji wa mazao kimeongezeka kutokana na wananchi husika kuwa na uwezo wa kulima bila kuwa na wasiwasi wa kukosekana kwa mvua.

(vi) Mafunzo yaliyotolewa yamejenga uwezo mkubwa kwa wananchi vijijini kusimamia maendeleo yao wenyewe. Baadhi ya wale waliopata mafunzo hayo wamepata ujuzi mkubwa ambao umewawezesha kufanya kazi ambazo hawakuwa na uwezo wa kuzifanya kabla kama uhasibu na wengine wamechaguliwa kuwa viongozi wa vijiji na madiwani.

(vii) Huduma kwa makundi maalum imesaidia kuanzisha miradi ambayo imepunguza kwa kiwango kikubwa makali ya ugumu wa maisha kwa kuongeza kipato na kuboresha lishe. Makundi hayo ni ya wazee, wajane, watoto yatima na walemavu. Stadi zinazotolewa kwa walengwa wa makundi haya zinawawezesha kukidhi mahitaji muhimu katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu, kwa kutambua tatizo la ajira nchini ilianzisha Mradi wa *SELF* ili kuongeza ajira na kipato kwa wananchi. Mwaka 1998/99 Serikali ilipata mkopo wa dola za Marekani 10.7 milioni kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na kuanzisha mradi wa *Small Entrepreneurs Loan Facility – SELF* kwa ajili ya kutoa mikopo midogo midogo yenye masharti nafuu. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2000 chini ya Usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Mradi ulianza kutekelezwa katika mikoa 6 ambayo ilibainika kuwa nyuma kimaendeleo, kama

sehemu ya majaribio. Mikoa hii ni Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida na mikoa yote Tanzania Zanzibar. Aidha ili kuongeza huduma na kasi ya utoaji mikopo, mwaka 2004 mradi ulipanua eneo kwa kuongeza mikoa mingine nane:- Ruvuma, Iringa, Mbeya, Mwanza, Mara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Pamoja na mikoa ya awali jumla ya mikoa inayotekeleza mradi wa *SELF* ni 14.

Hadi kufikia mwezi wa Juni 2005, *SELF* ilikwishatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.635 kwa Asasi za kifedha zipatazo 93. Kati ya fedha hizo, takriban asilimia 84 zimetolewa kwa Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*), na sehemu iliyobaki zilitolewa kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, mikopo hii imewafikia walengwa wapatao 25,515 ambao kati ya hao asilimia 62 ni wanawake. Inakadiriwa vilevile kuwa watu wapatao 97,325 wamenufaika na mikopo hii. Kazi zinazofanyika za kuongeza vipato ni pamoja na biashara ndogondogo kama vile mama lishe, vioski, maduka madogo madogo, ushonaji, ufumaji, kilimo, na ufugaji. Kwa ujumla urejeshaji wa mikopo hii upo katika kiwango cha asilimia 95.

Tathmini zilizofanyika zimedhihirisha kwamba mradi wa *SELF* umeanza kupata mafanikio ya kupunguza umaskini kutokana na mikopo inayotolewa kwa wananchi. Asilimia kubwa ya walengwa, (zaidi ya 70 %) walidhihirisha kuwa kipato chao kimeongezeka kutokana na biashara mbalimbali wanazofanya. Mikopo iliyoelekezwa katika kilimo inasaidia kupunguza tatizo la ajira vijijini na kuwa na uhakika wa chakula kwa familia kutokana na kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini zilizofanyika kuhusu mafunzo ya walegwa pamoja na watendaji wa Asasi za kifedha zinazoshirikiana na Mradi wa *SELF* kuhusu mbinu bora za utendaji na kuwepo kwa misingi endelevu ya kujiendesha kibiashara hasa katika Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*), yameanza kuonyesha mafanikio. Utunzaji wa kumbukumbu, vitabu mbalimbali vya fedha pamoja na taarifa mbalimbali zimekuwa na ubora kutokana na mafunzo waliopatiwa watendaji wa Asasi.

Mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa hasa wafanya biashara wadogo yamekuwa na manufaa makubwa. Walengwa wameanza kutambua kuwa biashara ni ushindani, ubunifu, ubora wa bidhaa, pamoja na umahiri wa kuitangaza. Kumekuwa na ongezeko la wafanyabiashara wadogo wadogo katika maonesho mbamblimbali ya kibiashara, na hivyo wameweza kuuza bidhaa zao na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato – *NIGP* ilianza kutekelezwa mwaka 1994. Programu ililenga kutekeleza miradi mbalimbali iliyo katika sekta za kilimo, miundo mbinu na biashara ndogo ndogo inayolenga katika kuongeza kipato cha mwananchi na hasa wanawake, vijana na walemavu. *NIGP* ilipanga kutekeleza jumla ya miradi kati ya 20-30. Hadi kufikia Machi 2002, jumla ya miradi 26 ilikwishatekelezwa. Kati ya hiyo miradi 18 ilikamilika kama ilivyopangwa. Miradi 8 iliyobaki inategemea kukamilishwa katika kipindi kijacho kama tutafanikiwa kupata fedha. Miradi yote hiyo ipo katika mikoa ya Mwanza, Pwani, Arusha, Manyara, Dodoma, Pemba, Unguja na Dar es Salaam.

Katika kipindi hicho cha utekelezaji wa miradi, *NIGP* imepata mafanikio makubwa, kwa kusaidia wananchi kupitia miradi hiyo iliyopelekea kuongeza kipato, kuongeza ajira, kuboresha utaalamu na kujenga uwezo wa wananchi hasa wanawake na vijana na kuboresha mazingira ya jumuiya katika makazi mbalimbali ya mijini na vijijini. Aidha, *NIGP* ilifanikiwa kuboresha uwezo wa Asasi za kifedha 30 ambazo zilifanyiwa mafunzo ya kitaalamu ili ziweze kutoa huduma bora za mikopo kwa wananchi. Jumla ya Asasi 12 za kifedha sasa zinaendelea kutoa huduma bora za mikopo ya maendeleo kwa wananchi katika mikoa mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu na inaendesha shughuli zake mtambuka kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa. Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kutambua hilo imejenga mazingira muafaka kwa mashirika haya kuendesha shughuli zao nchini. Naamini Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kuwa wengi tumeshuhudia mafanikio na mabadiliko makubwa katika sekta hii nchini. Aidha, kumekuwako na mahusiano mazuri kati ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kati ya *NGOs* wenyewe na kati ya *NGOs* na wadau wengine. Umuhimu wa sekta hii umezidi kudhihirika kutokana na hatua za makusudi za Serikali za kuwashirikisha *NGOs* kama wadau katika michakato mbali mbali ya kijamii na kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tumeshuhudia pia mafanikio makubwa katika sekta hii ya *NGOs* ambayo yametokana na jitihada za Serikali za kushirikisha na kutoa mwanya kama wadau wenza kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo. Mafaniko hayo ni pamoja na:

(i) Sera ya Taifa ya *NGOs* ambayo ni mara ya kwanza kuwa nayo nchini, ilipitishwa na Serikali mwezi Novemba 2001. Mchakato wa Sera hii ulishirikisha wadau wote na hivyo kuongeza umilikaji wake. Sera hii ambayo ni mwongozo wa kitaifa wa utendaji na uendeshaji shughuli za *NGOs* nchini inahimiza mahusiano mazuri kati ya Serikali na *NGOs* na mazingira muafaka kwa *NGOs* kuendesha shughuli zao.

(ii) Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 ambayo ni mahsusi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliandaliwa, kupitishwa na Serikali na kuanza kutumika kwa usajili wa *NGOs*. Lengo kubwa la Sheria hii ni kupunguza urasimu katika usajili wa *NGOs* nchini kwa kuweka ngazi za usajili katika Wilaya, Mkoa na Taifa. Aidha, inalenga kuweka utaratibu wa kutambua mchango wa sekta ya *NGOs* katika Pato la Taifa.

(iii) Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* na Baraza la Taifa la *NGOs* viliundwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 20 -21 Mei, 2004. Vyombo hivi vikuu ambavyo vinafanya kazi chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 vinaunganisha wawakilishi wa Serikali na *NGOs* katika utendaji kazi wao. Aidha, Baraza la Taifa la *NGOs* ni chombo huru ambacho kinaunganisha *NGOs* zote nchini.

(iv) Uratibu wa *NGOs* umeendelea kufanyika kwa kushirikisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, sekta ya kiraia, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Dhana ya uratibu imejikita hasa katika kuhakikisha na kuhimiza wadau wote kuimarisha mahusiano na mawasiliano mazuri ili kujenga umoja thabiti na kuunganisha nguvu zao katika kutekeleza malengo tuliyojiwekea. Ndio maana Serikali yetu imekuwa ikihimiza upashanaji habari na utoaji taarifa baina ya *NGOs* wenyewe, kati ya Serikali na *NGOs*, kati ya *NGOs* na Sekta binafsi na pia mawasiliano kwa sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha bajeti kilichopita, Serikali zote mbili kwa kupitia vikao mbalimbali iliendelea kuvitafutia ufumbuzi vikwazo mbalimbali vilivyojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Hii ni pamoja na kujadili suala la mafuta, gesi asilia na madini mengine ili kufanikisha utekelezaji wake kwa pande zote za Muungano hasa katika kugawana mapato yatokanayo na rasilimali hizo.

Aidha, ilionekana kwamba ni muhimu kwa pande zote za Muungano kushirikiana katika suala la uvuvi katika Bahari Kuu ili kulinda na kutumia rasilimali zilizopo katika kina kirefu cha Bahari Kuu kwa pamoja na kwa manufaa ya Taifa letu. Katika kujadili masuala ya hapo juu Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda kamati ya Makatibu Wakuu ambao walifanya vikao sita ambapo taarifa ya kamati hiyo iliwakilishwa kwa Serikali mbili mnamo Machi, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni kuwa na Muungano imara chini ya Serikali mbili. Katika kuhakikisha kuwa sera hiyo inatekelezwa, suala la kuratibu na kufuatilia maamuzi mbalimbali yanayohusu Muungano linazingatiwa. Aidha, kipaumbele kitakuwa kuhakikisha kuwa maamuzi ya Serikali yanatekelezwa ili kudumisha Muungano wetu kwa kufanya mawasiliano na Wadau wote kwenye maeneo ambayo ni ya Muungano na yasiyo ya Muungano, kutoa elimu kuhusu Muungano na kuweka mikakati ya ushirikiano kwa maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jeshi la Polisi linaendelea kuhakikisha usalama wa raia na mali zao. Aidha, Jeshi la Wananchi wa Tanzania linaendelea kutoa ulinzi wa kutosha katika mipaka yetu na kufanya shughuli nyingine kama kushirikiana na wananchi katika jitihada za kudumisha amani Nchini, kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya sherehe mbalimbali za Kitaifa zikiwemo sikukuu za Muungano kila mwaka kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mambo yasiyo ya Muungano chini ya utaratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara sita na Taasisi mbalimbali zilikutana na kufanya vikao nane vyenye lengo la kukuza Sekta husika ikiwa ni pamoja na kubadilishana sera, wataalam, kupata mafunzo ya pamoja, na kushirikiana katika kuiwakilisha Tanzania katika masuala ya Kimataifa. Mambo haya yamesaidia kwa kiasi kikubwa kushirikiana kwa karibu zaidi watumishi wa serikali zetu. Kwa mfano; Wizara ya Vijana, Ajira, Wanawake na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara

ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo zimeshirikiana katika shughuli mbalimbali kama vile mbio za Mwenge wa Uhuru na mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2005. Mchakato wa kuandaa Baraza la Vijana Tanzania (BAVITA) umeshirikisha pande zote mbili za Muungano. Aidha, baadhi ya wajumbe wa Baraza hili wanatoka katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mazingira katika kipindi cha 2004/2005 ulilenga katika masuala yafuatayo:- kukamilisha Sheria ya Mazingira; kutekeleza Mikataba na Itifaki za kimataifa zinazohusu mazingira; na kuendelea kuandaa na kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya mazingira.

Aidha, malengo mengine katika kipindi hicho yalikuwa kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kunufaika na Mfuko wa Mazingira Duniani (*GEF*); na kukuza weledi na ushirikishwaji wa wananchi na Taasisi mbalimbali katika masuala yote ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako tukufu kuhusu maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Mazingira. Muswada huu uliwasilishwa na kujadiliwa Bungeni katika kikao cha 17 na kupitishwa na Bunge tukufu tarehe11 Novemba mwaka jana na kuwa Sheria. Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza maandalizi ya kanuni, miongozo na taratibu ili kuwezesha kuanza utekelezaji wa sheria hii. Sheria imeweka bayana majukumu na wajibu wa kila sekta katika kila ngazi ya utendaji kuanzia ngazi ya kitaifa hadi ngazi ya kijiji na inaonesha majukumu ya wadau mbalimbali. Sheria pia inatamka mambo muhimu ikiwemo kuteuliwa kwa waratibu na washauri wa mazingira kwenye ngazi ya serikali za mitaa, mikoa na wizara; suala la tathmini ya athari kwa mazingira, kuweka viwango vya usafi wa mazingira kitaifa; na elimu ya mazingira na ushirikishwaji wa umma.

Kazi ya kutafsiri Sheria hii kwa lugha ya Kiswahili imeanza, ili kuhakikisha kuwa watu wengi wanaisoma na kuielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, inayotekelezwa na nchi za Afrika ya Mashariki yaani Kenya, Tanzania na Uganda kwa kushirikiana. Programu hii inalenga kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria na inatoa kipaumbele katika kuimarisha shughuli endelevu za uvuvi, kudhibiti uchafuzi wa maji na utupaji taka za majumbani na viwandani, kuhifadhi ardhi, misitu, vyanzo vya maji na maeneo owevu na kudhibiti magugu maji. Programu pia inatekeleza miradi midogo midogo kwa kushirikiana na wananchi, inayolenga kuboresha hali yao ya maisha na kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria katika sekta za afya, elimu, maji na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa gugumaji katika Bonde la Ziwa Victoria uliendelea katika kipindi cha 2004/2005. Mbawakavu wapatao milioni 29 walizalishwa

na kusambazwa katika Ziwa Victoria na maeneo korofi (*hot spots).* Program imeendelea kudhibiti gugumaji kwa karibu asilimia 90 na mialo zaidi ya 500 haina gugumaji. Vituo viwili zaidi vya kuzalishia mbawakavu vimejengwa *Rubafu Bay* (Bukoba Vijijini) na *Nyakaliro Bay* (Sengerema) na kufanya vituo vya kuzalishia mbawakavu kufikia jumla ya 14. Hii ni asilimia mia moja ya lengo la Programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chote cha mwaka 2004/2005, Progamu iliendelea na tafiti mbalimbali kuhusu uchafuzi wa maji ya Ziwa na utupaji taka za majumbani na viwandani. Tafiti hizi zinaonesha kuwa maji ya Ziwa Victoria yamechafuka kandokando ya Ziwa, hasa yale yaliyo karibu na miji na viwanda, kama vile Jiji la Mwanza, Miji ya Musoma, Bukoba, na kadhalika.

Ili kupunguza uchafuzi huu, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuendelea kuvishirikisha viwanda kutekeleza mbinu za uzalishaji. Viwanda hivi vimeendelea kushirikiana na Programu katika kupunguza uchafuzi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha uvuvi endelevu katika Ziwa Victoria, nchi za Kenya, Tanzania na Uganda kwa kushirikiana zimekusanya takwimu za bioanuwai ya samaki katika Ziwa. Takwimu hizi zitatumika katika utayarishaji wa atlasi inayoonesha mahali samaki wapatikanapo katika Ziwa Victoria. Utayarishaji wa atlasi hizi umeshaanza na unafanywa na nchi zote tatu. Pia, mradi ulifanya sensa *(Frame Survey)* ya tatu ya wavuvi na zana za kuvulia samaki kwa kushirikiana na Kenya na Uganda. Takwimu za sensa hii zinatayarishwa na zitaziwezesha nchi hizi kuweka mikakati ya uvuvi endelevu na makadirio ya uvunaji wa samaki katika Ziwa Victoria. Vile vile mradi uliendelea kutoa ushauri kwa baadhi ya vijiji vya Mkoa wa Mara kuhusu kuhifadhi misitu hasa misitu ya asili ili kupunguza kasi ya kutoweka kwa misitu. Aidha kwa kushauri na kushirikisha, wananchi wamepanda miche ya miti milioni 2.5 na kusambazwa katika wilaya za Tarime, Musoma na Bunda. Vikundi vinavyojihusisha na uoteshaji na upandaji miti vimeongezeka kutoka 11 mwaka 2003/04 hadi 26 mwaka 2004/05. Miche ya miti imesambazwa mashuleni, na katika taasisi na watu binafsi. Aidha, mradi umesaidia utekelezaji wa miradi midogo midogo minne (4) katika sekta za elimu na afya. Miradi mingine 3 imeanzishwa katika sekta za elimu na afya katika wilaya za Muleba (1) na Tarime (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kilimo endelevu na matumizi bora ya ardhi, wakulima 242 katika vijiji vya Chamugasa, Mayega, Lamadi na Lukungu wilaya ya Magu wamepatiwa mafunzo. Pia wakulima 11 katika lindimaji la Kalemela Wilayani Magu wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha makinga maji kwenye miteremko. Makinga maji yenye urefu wa kilometa 3.4 yalitengenezwa katika lindimaji hili. Aidha wakulima 10 wamepata mafunzo ya uvunaji maji ya mvua. Programu hii kwa kushirikiana na serikali za Wilaya za Karagwe, Sengerema na Bunda zimetayarisha mkakati wa pamoja wa kuanzisha shughuli za Mradi katika wilaya hizo. Program pia imechapisha vijitabu viwili cha "Mbinu za Kuzuia Mmomonyoko wa Udongo Shambani kwa Wakulima Wadogo Wadogo" na kingine cha "Matumizi Sahihi ya Madawa ya Kilimo" na nakala 4,000 zimesambazwa kwa walengwa. Tangu 1997 tafiti mbali mbali za kisayansi zimefanyika. Matokeo ya tafiti hizi yamechapishwa katika taarifa za kibiolojia ya viumbe katika Bonde la Ziwa Victoria katika jarida la *Tanzania Journal of Science*

nakala 200 za jarida hili zimesambazwa kwa wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Bunge. Katika jitihada za kuhifadhi na kuendeleza matumizi bora ya maeneo owevu, mradi uliendelea kuyakarabati kwa kuwashirikisha wananchi wa kijiji cha Nyatwali kwa kupanda miti 26,000. Aidha, wasusi 28 kutoka vijiji vinne vinavyozunguka eneo owevu la Simiyu wamepatiwa mafunzo ya kutengeneza viti na meza kwa kutumia rasilimali za maeneo hayo. Katika kipindi hiki pia Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa ziara ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kutembelea maeneo ya mradi wa Ziwa Victoria katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Wabunge walipata fursa ya kuona shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Kwanza ya Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria ambayo inagharimiwa na Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia (*IDA*) na Mfuko wa Mazingira (*GEF*) itamalizika tarehe 31 Desemba, 2005. Katika kutekeleza shughuli za mwaka 2004/2005, mradi umetumia shilingi bilioni 1.8. Pamoja na mafanikio mengi na mazuri yaliyopatikana katika miaka minane ya utekelezaji wa Programu hii, matatizo ya hifadhi ya mazingira ya Ziwa Victoria na bonde lake, bado hayajamalizika na ni makubwa. Hivyo serikali kwa kushirikiana na Uganda na Kenya imeona umuhimu wa kuandaa programu ya muda mrefu wa miaka 10 hadi 15. Programu inayoandaliwa italenga katika masuala ya utafiti wa kisayansi ya mazingira, uchumi na usimamizi wa maliasili katika bonde la Ziwa Victoria. Maandalizi ya Awamu ya Pili ya Programu hii yanaendelea na yatakamilika Juni 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Bunge hili tukufu limeridhia Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika. Lengo la Mkataba huo ni kuziwezesha nchi zinazolizunguka ikiwemo Tanzania, kuhakikisha kwamba panakuwepo na hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai ya ziwa katika misingi ya uwiano na usimamizi wa ushirikiano. Mkataba huu unazihusisha nchi za Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Aidha mwaka jana nililieleza Bunge hili Tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kufanya majadiliano na wafadhili mbalimbali walioonyesha nia ya kugharimia shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu kwenye ziwa na bonde lake. Katika kutekeleza hilo, Serikali imesaini makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika ya mkopo wa shilingi bilioni 8.1 kwa utekelezaji wa mradi wa miaka mitano wa uwiano wa Ziwa Tanganyika. Pia ujumbe wa Mfuko wa Nchi za *Nordic (Nordic Development Fund)* ulitembelea mkoa wa Kigoma mwezi wa Septemba mwaka jana kwa lengo la kupata maelezo zaidi ya maandalizi ya mradi wa majitaka ya Halmashauri ya Mji wa Kigoma/Ujiji. Hadi sasa *NDF* imethibitisha kutenga *Euro* milioni 6 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Aidha, kikao cha kwanza cha kamati ya kitaifa ya uendeshaji, kimefanyika mjini Dar es Salaam kufanya maamuzi kuhusu maandalizi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazingira ya Ziwa na bonde lake. Kutokana na uchelewashwaji wa kupata fedha kutoka kwa wafadhili, miradi haikutekelezwa kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako tukufu mwaka jana, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Kituo cha Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira Tanzania (*CPCT*) inasimamia mradi wa usafi wa mazingira kwa ajili ya

maendeleo endelevu ya viwanda ambao ulianza mwezi Desemba 1999. Mradi huu una madhumuni ya kujenga uwezo wa viwanda na wadau wengine nchini katika tekinolojia na mbinu za uzalishaji bora zenye lengo la kupunguza au kuzuia uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Kituo, kikishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kilifanya uchunguzi kwa nia ya kubainisha nafasi na uwezo wa Kitaifa kuweka mkakati wa tekinolojia nadhifu (*Diagnostic Study of Opportunities and Capacities for the Creation of National Cleaner Technology Strategy*). Uchunguzi huu uligharamiwa na Idara ya Uchumi na Masuala ya Jamii ya Umoja wa Mataifa. Matokeo ya uchunguzi huo yamebainisha sekta sita za uchumi kuwa na uwezekano mkubwa wa kufaidika na utumiaji wa teknolojia nadhifu. Sekta hizo ni bidhaa za vyakula, madini, utalii, viwanda vidogo vya uzalishaji sukari, kilimo cha mboga na maua, na bidhaa za mbao. Tanzania ni miongoni mwa nchi nne za majaribio ya mradi huu; zingine ni Argentina, Nicaragua, na Vietnam. Shughuli zingine zilizofanywa na Kituo ni pamoja na:- kuandaa warsha moja kwa washiriki 40 kutoka taasisi za serikali, viwanda na vyombo vya habari juu ya uanzishwaji wa huduma ya mtandao wa tekinolojia nadhifu kwa njia ya tovuti; kuratibu usajili wa wataalamu wa tekinolojia nadhifu kwenye tovuti husika; kuainisha na kuorodhesha tekinolojia nadhifu zilizopo nchini na nchi jirani; kusajili Kituo; na kuratibu shughuli za Sekretariati inayoshughulikia masuala ya matumizi na uzalishaji endelevu barani Afrika ijulikanayo kama *African Roundtable on Sustainable Consumption and Production (ARSCP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Montreal kuhusu kuzuia matumizi ya madawa yanayomong'onyoa ukanda wa hewa ya ozoni angani. Mafunzo yaliendeshwa kwa maofisa wa idara ya forodha toka vituo vyote vya mpakani juu ya udhibiti wa biashara ya uingizaji wa vifaa vyenye kemikali aina ya *CFCs* nchini kulingana na matakwa ya Itifaki ya *Montreal*. Mradi wa miaka miwili wa kuimarisha kitengo kinachosimamia utekelezaji ikiwa ni awamu ya pili ya mradi umeandaliwa na fedha zimepatikana toka Mfuko wa Itifaki. Aidha tathimini ya kiasi cha kemikali zinazomong'onyoa ukanda wa hewa ya Ozoni ilifanyika. Matokeo yameonesha kuwa mwaka 2003 na 2004 kiasi cha tani 196.8 na 62.7 sawia kiliingizwa nchini kwa ajili ya kutumika kwenye majokofu na viyoyozi.

Aidha, mwezi Machi 2004 Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na *CPCT*, ilizindua kituo cha kusafisha na kurudufu kemikali aina ya *CFCs* zinazotumika kwenye majokofu na viyoyozi *(CFC Reclamation Centre).* Kituo hiki kitafanya kazi chini ya usimamizi wa *CPCT*. Kituo cha *CPCT* kitapokea gesi chafu toka makampuni ambayo yana mitambo ya kunasa gesi za *CFCs* na kuisafisha tayari kwa kutumika tena. Kazi hizi ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya kitaifa ya kuondosha matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa ukanda wa hewa ya Ozoni ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho ya siku ya Ozoni Duniani ambayo ni tarehe 16 Septemba kila mwaka yalifanyika Dar es Salaam tarehe 20 Septemba 2004 ambapo wadau 100 walishiriki. Wadau waliwakilisha Idara za Serikali, makampuni ya biashara na viwanda husika, wanahabari na taasisi za mafunzo na utafiti na mashirika

yasiyokuwa ya kiserikali. Maadhimisho yalifanyika kwa njia ya semina ya kukuza weledi juu ya manufaa ya ukanda wa hewa ya Ozoni, majukumu ya Taifa chini ya Itifaki na upatikanaji wa kemikali mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Bunge liliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Stockholm unaohusu udhibiti wa kemikali zinazochukua muda mrefu sana kuoza katika mazingira *(Persistent Organic Pollutants - POPs).* Madhumuni ya Mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara ya kemikali za aina hii. Rasimu ya Mpango wa Taifa wa Kutekeleza Mkataba wa Stockholm iliandaliwa na warsha ya wadau ya kujadili rasimu ya mpango ilifanyika mwezi Machi 2005. Mapendekezo na maoni yaliyotolewa na wadau yametumika katika kuboresha rasimu ya Mpango huu.

Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa kutayarisha takwimu za kemikali zinazochukua muda mrefu kuoza aina ya *Polychlorinated Biphenyls* (*PCBs*) na vifaa vinavyotumia kemikali hizo.

Mradi huu unatekelezwa katika nchi zote 14 wanachama wa Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*). Huu ni mradi wa mwaka mmoja wenye lengo la kuweka mikakati ya pamoja ya kulinda mazingira na afya ya binadamu dhidi ya athari ya kemikali hizo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, shughuli zifuatazo zilifanyika:- Uchunguzi wa mafuta ya mitambo ya kusambaza umeme inayoashiria kuwa na kemikali aina ya *PCBs* ulifanyika katika maabara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kufahamu viwango vya *PCBs*. Pia ripoti ya uchunguzi kuhusu kiasi cha mafuta yenye kemikali na vifaa vinavyotumia kemikali aina ya *PCBs* iliandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoridhia Mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa utupaji na usafirishaji wa taka sumu baina ya nchi na nchi *(The Basel Convention on the Control of Transboundary Movements of Hazardous Wastes and their Disposal)* ziliamua kuanzisha Vituo vya Kanda vya Mafunzo na Usambazaji wa Tekinolojia. Kituo kwa ajili ya nchi za Afrika zinazozungumza Kiingereza kipo Pretoria, Afrika ya Kusini. Nchi zinazohudumiwa na Kituo hiki ni 21, nazo ni:- Afrika ya Kusini; Botswana, Eritrea, Ethiopia, Gambia, Ghana, Liberia, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Rwanda, Namibia, Nigeria, Sychelles, Swaziland, Uganda, Zambia, Zimbabwe na Tanzania. Kituo hiki kipo katika hatua za awali za kusajiliwa rasmi, ambapo nchi 11 zimesaini mkataba wa kuunda Kituo hiki na zipo katika hatua mbalimbali za kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba taratibu za kuridhia Mkataba wa Kuundwa kwa Kituo hiki zimeshaanza. Mawasiliano na wadau mbalimbali yamefanyika na wamependekeza Tanzania iridhie mkataba wa kuunda kituo hiki. Kituo kitatoa mafunzo na kushughulikia upatikanaji wa tekinolojia zinazokubalika kudhibiti madhara ya taka sumu wakati wa kutibu au kutupa taka za aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Kituo cha Pretoria kilitekeleza kazi zifuatazo:- kuratibu mafunzo juu ya Itifaki ya Mkataba wa Basel inayohusu fidia kutokana na ajali au madhara yanayoweza kutokea wakati wa usafirishaji wa taka za sumu kati ya nchi na nchi na utupaji wake yaliyofanyika nchini Ethiopia ambapo jumla ya nchi 19 zinazohudumiwa na Kituo zilishiriki; kuanzisha tovuti ya kituo ambayo inaonesha shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Kituo; Kuendesha mafunzo kwa wadau mbalimbali juu ya usimamizi wa taka zenye sumu katika sekta za Afya, Viwanda na Usafiri; na kuandaa mkakati kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za Kituo. Vilevile kuendesha mafunzo juu ya kuimarisha ushirikiano na programu za kimataifa na za kikanda zinazotekelezwa chini ya mikataba mbalimbali ya mazingira; na kutoa mafunzo kuhusu uandaaji wa miradi inayoweza kuvutia uwekezaji katika tekinolojia zenye kudhibiti athari za taka zenye sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(United Nations Framework Convention on Climate Change - UNFCCC*). Mwaka jana nililiriarifu Bunge lako tukufu kuhusu mradi wa kuandaa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*National Adaptation Programme of Action – NAPA).* Katika kipindi hiki timu ya wataalamu wa *NAPA* ilifanya tathmini ya kiwango cha madhara yanayoweza kutokea na mikakati iliyopo ya kuhimili madhara hayo kwa sekta ambazo zitaathirika zaidi na mabadiliko ya tabianchi. Sekta zitakazo athirika zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na: Kilimo, Misitu, Maji na mifugo, Wanyamapori, Afya, Makazi ya watu, Utalii, Ardhi, Nishati, Maeneo ya pwani ya bahari na Viwanda. Rasimu ya ripoti ya awali ya tathmini hiyo *(Draft Preliminary Assessment Report)* imekwisha andaliwa. Ripoti hii imeainisha sekta hizi zilizo katika hatari ya kuathirika zaidi na mabadiliko ya tabianchi pamoja na mbinu za kukabiliana na mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nililiriafu Bunge hili kuwa Tanzania Serikali likuwa inaandaa mwongozo wa Taifa wa jinsi ya kushiriki katika miradi mbalimbali ya *Clean Development Mechanism - CDM (Clean Development Mechanism Investor's Guide).* Rasimu ya mwongozo huo imekamilika. Mwongozo huu umeainisha jinsi Tanzania itakavyoshiriki kwa hiari katika shughuli za miradi ya CDM, na utaratibu na masharti ya kufuata kwa mwekezaji yeyoye anayetaka kujishughulisha na miradi ya CDM nchini. Aidha mwongozo umebainisha vigezo vya maendeleo endelevu ambavyo ni lazima miradi ya namna hii ivikidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (*United Nations Convention to Combat Desertification - UNCCD).* Katika kipindi hiki Programu ya Taifa ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame *(National Action Programme to Combat Desertification – NAP)* iliyoandaliwa mwaka 1999, ilipitiwa upya ili ikidhi matakwa ya mikakati mingine ya kitaifa hususan Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA). Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais, kupitia mradi wa *Sub-*

*regional Support Facility in Southern Africa (SSFSA)* unaofadhiliwa na *SADC*, iliendelea kutoa msaada wa kifedha kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (*NGOs*) na vikundi vingine vya kijamii vinavyojishughulisha na shughuli za kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Katika kipindi hiki Ofisi iliweza kuandaa ripoti ya tatu ya utekelezaji wa Mkataba huu na kuiwasilisha kwenye Sekretariati ya Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki pia, Ofisi ilipata msaada wa fedha kutoka *Global Mechanism* kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kuhuisha mipango ya maendeleo katika ngazi ya wilaya na utunzaji wa taarifa zinazohusu kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Katika utekelezaji wa mradi huu, warsha ya ushirikishwaji kwa wilaya tisa toka mikoa mitatu (Singida, Mwanza na Shinyanga) inayokabiliwa na tatizo la jangwa na ukame iliandaliwa. Aidha mafunzo ya kompyuta kuhusu utunzaji wa kumbukumbu zinazohusu kuenea kwa hali ya jangwa na ukame yalifanyika kwa maafisa husika kutoka katika wilaya hizo tisa. Mradi huu pia ulinunua kompyuta kwa kila wilaya hizo ili ziweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira Duniani *Global Environment Facility* (*GEF*) hapa nchini. Katika kipindi hiki Ofisi imeendelea kupokea miradi mbalimbali kutoka kwa wananchi kwa lengo la kuichambua na kuipitisha kwa ajili ya kupatiwa ufadhili wa *GEF*. Vilevile, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuhakikisha kuwa Sera za *GEF* zinaendana na Sera za Serikali, kutoa taarifa ya mikutano mbalimbali ya *GEF* kwa wadau mbalimbali hapa nchini, kuwasilisha maoni mbalimbali ya Serikali kwa wadau wa *GEF*, na kukuza ufahamu wa *GEF* kwa Watanzania ikiwa ni pamoja na kusambaza makabrasha yahusuyo *GEF* nchini. Aidha katika kipindi hiki Ofisi ya Makamu wa Rais imeweza kuandaa kongamano la kitaifa kuhusu Mpango na Mkakati wa kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, pamoja na kujadili miongozo ya uwekezaji katika miradi ya *CDM* nchini. Katika kuboresha hali ya mazingira nchini, Mfuko huu umeendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazingira hapa nchini. Miradi hiyo ni pamoja na:- Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Programme);* Mradi wa Kuendeleza Hifadhi ya Bahari ya Mnazi Bay-Mtwara, Mradi wa *Solar Powered Ultra-violet Water Purification Systems for Rural Tanzania,* Mradi wa hifadhi ya mazingira katika bonde la mto Kagera, na Mradi wa kupunguza athari kwa mazingira zitokanazo na Utalii wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge hili tukufu kuhusu uamuzi wa Baraza la Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF Assembly)* wa kukubali kufadhili miradi ya kukabiliana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Katika kipindi cha mwaka 2004/05 Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuandaa na kuendesha warsha ya uhamasishaji kwa taasisi za kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu maeneo hayo mapya yanayofadhiliwa na Mfuko huo. Kufuatia warsha hizo mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yameitikia wito wa kuandaa miradi ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Ofisi ya Makamu wa Rais imehakiki miradi hii na kuiwasilisha kwenye Sekretariati ya Mfuko kwa ufadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu programu ya kuimarisha usimamizi wa mazingira na maliasili inayotekelezwa kwa msaada toka serikali ya Marekani kupitia shirika lake la misaada (*USAID*). Madhumuni ya programu hii ni kukuza ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za usimamizi wa hifadhi ya mazingira ili kujenga uwezo wa serikali za mitaa na vijiji, sekta binafsi, na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kupanga na kutekeleza shughuli za hifadhi na uendelezaji wa mazingira katika maeneo yao. Katika kipindi hicho, programu ilisaidia katika kukamilisha sheria ya mazingira iliyopitishwa na Bunge lako tukufu mwishoni mwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge hili tukufu kuwa programu hii inasaidia pia katika kuimarisha na kuboresha miundombinu ikiwemo matengenezo ya barabara na usambazaji wa maji katika Hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara na vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo. Vilevile katika kipindi hicho, mafunzo mbalimbali yaliendeshwa kwa wafanyakazi wa *TANAPA* na jamii zinazozunguka hifadhi za Tarangire na Manyara na Hifadhi ya Akiba ya Ugalla, juu ya ulinzi wa maliasili na kuzuia ujangili, na mafunzo ya *GIS*, namna ya kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji na uanzishwaji wa hifadhi za jamii *(Wildlife Management Areas - WMAs)*.

Mipango ya matumizi bora ya ardhi iliandaliwa kwa vijiji vya Kiteto, *Endumet*, Narakauwo na *Loiborsiret* mkoani Arusha. Aidha mradi uliendelea kufanya tafiti mbalimbali za ekolojia, sensa ya wanyama hasa tembo na simba na uchunguzi kuhusu vifo vya ndege vilivyotokea katika hifadhi ya Manyara ambapo ndege 50,000 wa aina ya flamingo na 48 wa aina ya bata maji walikufa na zaidi ya flamingo milioni tatu walihamia kwenye maziwa mengine. Shughuli nyingine ni kuimarisha vituo vya kufikia wageni *(Visitors Centres)* katika hifadhi ya Tarangire na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hicho pia, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa ziara ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira katika mikoa ya Tabora na Rukwa. Kamati ilitembelea wilaya za Sikonge, Urambo na Mpanda ambapo Waheshimiwa Wabunge walijionea uharibifu wa mazingira ya Hifadhi ya Akiba ya Ugalla na misitu inayozunguka hifadhi. Itakumbukwa kwamba mwaka jana nililiarifu Bunge hili Tukufu kuhusu ziara ya Waheshimiwa Wabunge wa kamati hiyo mkoani Tanga, Arusha na Manyara, ambapo ilitoa ushauri na mapendekezo juu ya matatizo ya uchimbaji holela wa madini mkoani Tanga.

Kutokana na maelekezo ya Kamati, Ofisi ya Makamu wa Rais imefanya uchunguzi wa kina na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kulitatua tatizo la uchimbaji holela wa madini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya programu hii iliyoanza mwaka 1987/98 inategemea kumalizika ifikapo tarehe 30 Septemba 2005. Serikali inawasiliana na Serikali ya Marekani kwa ajili ya uandaaji wa awamu ya pili ya programu kwa kipindi kingine cha miaka kumi (2005 – 2014).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki, Tanzania ilishiriki katika mkutano wa 13 wa Kamisheni ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa uliofanyika mjini New York nchini Marekani kuanzia tarehe 11 hadi 22 Aprili mwaka huu. Mkutano huo ulilenga kuhamasisha wadau katika ngazi zote za kimataifa kuandaa mikakati ya kisera kuhusu utekelezaji wa Agenda ya 21 na Mpango wa Utekelezaji wa Johannesburg kuhusu Maendeleo Endelevu Duniani. Aidha, pamoja na mambo mengine mkutano ulijadili mbinu za kuimarisha huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini, Usafi wa mazingira na Maendeleo ya makazi. Katika mkutano huo pia mawaziri wa nchi mbalimbali walikutana kujadili na kufikia makubaliano ya maamuzi ya kisera kuhusu mwelekeo wa kiutendaji katika harakati za kuimarisha huduma za maji, usafi na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa mwaka 2000 wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa anafungua mgodi wa *Geita Gold Mine*, aliagiza kuanzishwa kwa Tuzo ya Rais ya Uongozi na Ubora wa Uhifadhi wa Mazingira katika Uchimbaji Madini. Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa inaratibu mashindano ya Tuzo hiyo ambayo hutolewa kila mwaka kuanzia mwaka 2001. Kwa kipindi cha mwaka 2004/2005, jumla ya kampuni nane, zikiwemo za wachimbaji wakubwa tatu, wa kati tatu, na wachimbaji wadogo wawili waliingia katika shindano. Mshindi wa mwaka 2004/2005 alipatikana, na kukabidhiwa Tuzo
.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge hili tukufu linavyofahamu upana wa suala la mazingira ambapo sekta nyingi za watu binafsi, vikundi mbalimbali, taasisi, makampuni na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanaguswa na umuhimu wa mazingira bora. Kutokana na juhudi za serikali za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa hifadhi ya mazingira. Kwa sasa juhudi za wananchi katika hifadhi ya mazingira zinatia moyo. Katika kipindi cha mwaka jana wananchi kutoka mikoa yote ya Tanzania bara waliendelea na wito wa azimio la Dodoma la Kampeni ya Upandaji Miti ambapo kati ya jumla ya miti 94,338,614 iliyopandwa msimu wa 2003/2004, jumla ya miti 75,732,445 ilipona. Aidha vikundi mbalimbali vinavyohusika na hifadhi ya mazingira vilipatiwa huduma ya ushauri ili kuboresha azma ya uhifadhi na utunzaji mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05, pamoja na ukaguzi wa maeneo mbalimbali ya miji na viwanda ili kushauri na kuelekeza juu ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, Baraza liliandaa mipango ya utekelezaji wa mradi wa Tathmini ya Uchafuzi wa Hewa Jijini Dar es Salaam unaofadhiliwa kwa pamoja na Serikali, Wakala wa Mazingira wa Serikali ya Marekani ( *USEPA*) na Shirika la Mazingira Duniani (*UNEP*). Vile vile, maandalizi yameendelea kufanyika kwa ajili ya mradi wa kuteketeza madawa chakavu ya kilimo nchini, kwa ushirikiano na Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa (*FAO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Baraza lilifanya mapitio ya taarifa thelathini na tano (35) za tathmini ya athari kwa mazingira za miradi ya maendeleo iliyopo hapa nchini na kutoa ushauri pamoja na vibali vyenye masharti ya kuboresha mazingira. Vile vile Baraza lilipitia taarifa za ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit Reports)* za miradi kumi (10) na kuzitolea ushauri wa kitaalam

kuhusu namna ya kuboresha masuala ya mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo; na kwa kuzingatia mchakato wa TAM wa Benki ya Dunia, Baraza lilipitia Muongozo wa Jumla wa shughuli za Mazingira na za Kijamii *(Environmental and Social Assessment Framework)* wa Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani na Bahari *(Marine and Coastal Environmental Management Project – MACEMP)* na kutoa kibali chenye masharti ya kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa taifa linapata taarifa za kisayansi kuhusu usimamizi wa mazingira katika shughuli mbalimbali; Baraza liliandaa kongamano la Kitaifa la Kisayansi, kuhusu Kilimo endelevu kwa kuangalia uhusiano kati ya kilimo, mazingira na umaskini. Kongamano hili lilifanikiwa kwa kiwango cha juu. Napenda kuwashukuru serikali ya Norway, Finland na pia *UNDP* kwa msaada wa fedha waliotoa kufanikisha kongamano hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, pamoja na kuendeleza elimu ya mazingira na uhamasishaji, Baraza limeandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Mazingira na Mawasiliano ambao unalenga kukuza weledi wa wanahabari, watekelezaji wa elimu ya Mazingira na kukuza uwezo wa kufanya maamuzi yanayohusiana na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa elimu ya Mazingira na mawasiliano, Baraza limeandaa miongozo, makala za ushauri na kuelimisha jamii juu ya majukumu yao na matumizi endelevu ya rasilimali. Vile vile Baraza limeendelea kutekeleza shughuli mbali mbali za utunzaji wa mazingira katika Bonde la Kihansi na mwambao wa nchi yetu kwa kushirikiana na jamii na serikali za mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha sera na mikakati ili kujenga mazingira bora yatakayowezesha uchumi wa Taifa kukua kwa haraka na kuwanufaisha wananchi ili waondokane na umaskini. Hii ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati ya kuondoa umaskini na kuhakikisha kuwa sera zinafanyiwa mabadiliko pale inapolazimika ili zilenge kuondoa umaskini wa kipato na usio wa kipato na kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania wote. Aidha, tumeendelea kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya jitihada za kupambana na umaskini nchini ili kufahamu hali halisi ya utekelezaji, mafanikio na mapungufu na hivyo kuweza kuchukua hatua mapema za kurekebisha mapungufu pale itakapolazimika. Aidha, uelimishaji na uhamasishaji wa wananchi kuhusu jitihada mbalimbali za kupambana na umaskini umetiliwa mkazo ili kuwezesha wadau wote kufahamu sera na mikakati ya kitaifa na kujifunza mbinu mbalimbali zitakazochangia nguvu katika kuondokana na umaskini. Pamoja na jitihada hizi za kisera na ufuatiliaji, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa programu na miradi muhimu inayolenga kuongeza kasi katika jitihada za kuondokana na umaskini. Programu na miradi hii ni kama vile *TASAF*, MKURABITA, *SELF* na *NIGP*.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji mwaka uliopita (2004/05) ni kama ifuatavyo:-

Kusimamia Utekelezaji wa Mkakati wa Kuondoa Umaskini na Kuhakikisha Sera Zinafanyiwa Mabadiliko Pale Inapolazimika ili Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza, Serikali ilifanya mapitio ya Mkakati wa Awali mwaka 2004 na kuandaa Mkakati wa awamu ya pili MKUKUTA. Maeneo makuu ya kipaumbele yaliyoainishwa katika MKUKUTA ni: (i) kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; (ii) kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii; na (iii) utawala bora na uwajibikaji. Mkakati huu tofauti na MKU umeweka msisitizo mkubwa zaidi katika kukuza uchumi ili kuboresha mazingira ya kuondokana na umaskini. Pamoja na mambo mengine Mkakati unasisitiza utawala bora na uwajibikaji kwa lengo la kuangalia mifumo na michakato ya uchumi kama vile usimamizi wa rasilimali za umma, kushirikisha wananchi katika kufanya maamuzi kwa mfano kupitia michakato ya uboreshaji wa serikali za mitaa, huduma za jamii, njia kuu za uchumi na hasa kuongeza uzalishaji, njia za usafirishaji na mawasiliano, kuboresha sekta binafsi n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yanayotarajiwa yamebainishwa na kuwekewa malengo tunayoamini kuwa yakitekelezwa kwa ufanisi yatatufikisha kwenye lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo. Ikiwa kama hatua ya uboreshaji masuala mtambuka *(cross-cutting issues)* ambayo ni pamoja na jinsia, UKIMWI, ajira, mazingira, utawala bora na sheria, na makundi yanayoathirika zaidi na umaskini (mf. Wazee, wenye ulemavu, vijana, watoto n.k), yameingizwa kwenye MKUKUTA kulingana na matakwa ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuandaliwa kwa MKUKUTA kumesaidia kuboresha taratibu na mipangilio ya mgao wa fedha za serikali kwa kuhakikisha kuwa malengo yaliyobainishwa kama kipaumbele kwenye MKUKUTA na ambayo siyo, yanaingizwa kwenye mfumo wa kompyuta *(Strategic Budget Allocation – SBAS)* wa Wizara ya Fedha kwa sekta zote. Hii itarahisisha na kuhakikisha kuwa bajeti ya serikali inaelekezwa kwenye maeneo yatakayotufikisha kwenye matokeo tunayotarajia. MKUKUTA utatekelezwa kwa miaka mitano, kuanzia mwaka 2005/06 hadi 2009/10.

Kuratibu Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini ya Hali ya Umaskini Nchini

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizofanyika chini ya mfumo wa ufuatiliaji ni:- Uchambuzi wa takwimu za Savei ya Kilimo na Mifugo *(Agriculture Sample Survey 2003/04);* kufanya Savei ya UKIMWI; kuandaa ripoti za mkoa na ripoti nyingine muhimu zinazotokana na takwimu za Sensa na Savei; kufanya Savei ya masuala ya Afya na Uzazi *(Demographic and Health Survey);* na kuanza maandalizi ya Savei ya Hali ya Mapato na Matumizi ya Kaya (*HBS*) inayotarajiwa kufanyika mwaka 2005/06.

Aidha, maandalizi ya mwongozo wa mapitio ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA (2004) yamefanyika. Lengo la mapitio ya mfumo huu ni kuboresha mapungufu yatakayojitokea wakati wa utekelezaji na kufanya mfumo uende sambamba na matokeo yanayotarajiwa katika MKUKUTA. Mfumo huu unasaidia

kuonesha matokeo ya utekelezaji kwa wakati tofauti na kubaini mapungufu ili hatua za makusudi za kuboresha mapungufu zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya mapitio ya mfumo huu wa ufuatiliaji inaendelea. Tayari vikundi vya kiufundi *(Technical Working Groups)* vimekwisha kamilisha tathmini ya shughuli zao na kupendekeza mambo ya kipaumbele pamoja na marekebisho yanayohitajika ili kuboresha zaidi mfumo huu na kuufanya kukidhi mahitaji ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA. Hatua inayoendelea sasa ni maandalizi ya Mpango Kabambe wa Ufuatiliaji wa Hali ya Umaskini kwa kuzingatia uzoefu wetu wa nyuma na mapendekezo yaliyotolewa na tathmini ya ndani na nje ya mfumo huu. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Novemba 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitatu mfululizo, Serikali imekuwa ikiadhimisha Wiki ya Sera za Kuondoa Umaskini ili kutoa fursa ya kubadilishana mawazo na kuibua mijadala ya kitaifa inayosaidia kuboresha jitihada za kupambana na umaskini. Mwaka jana 2004 mwezi Novemba maadhimisho yalilenga kujadili rasimu ya mwisho ya MKUKUTA. Nafasi hiyo maalumu ilitolewa kuwezesha wadau katika ngazi ya Taifa na katika mikoa yote kufahamu maeneo ya kipaumbele ya mkakati na kutoa maoni zaidi kwa uboreshaji. Majadiliano katika ngazi ya mkoa yalisimamiwa na TAMISEMI, na kila mkoa ulipitia rasimu na kuwasilisha maoni yao Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo yalijumuishwa katika MKUKUTA.

Aidha, Ofisi iliendelea kufanya uelimishaji wa wananchi kuhusu jitihada mbalimbali za kupambana na umaskini kupitia kipindi cha redio cha TUJIKOMBOE kinachorushwa na Redio Tanzania kila wiki siku ya Jumatano saa 10.30 jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliendelea kupanua huduma ya mikopo ili kuwafikia watu wengi zaidi wenye vipato vya chini, kwa kuongeza mikoa mingine minane na kufanya jumla ya mikoa yote inayotekeleza mradi wa *SELF* kufikia 14 Tanzania Bara. Mikoa hii ni: Singida, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Lindi, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mwanza, Iringa, Mbeya, Ruvuma na mikoa yote ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ilifanyika na kudhihirisha kwamba, asasi nyingi zinahitaji mafunzo ya mbinu bora za utendaji *(Best Practices Principles)* ambazo zinakubalika ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wateja kwa misingi endelevu. Kufuatana na tathmini hii programu ya mafunzo iliandaliwa na mafunzo kutolewa. Watendaji wapatao 327 kutoka asasi mbalimbali za kifedha wakiwemo Maafisa Mikopo, Mameneja wa Mikopo, Wahasibu na Makarani walinufaika na mafunzo mwaka uliopita. Jumla ya watendaji 1163 wamekwisha faidika na mafunzo tangu mradi uanze mwaka 2000. Katika mafunzo, mradi pia unazingatia kutoa mafunzo maalumu kwa viongozi wa vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*), ili vyama viweze kujiendesha kibiashara.

Sambamba na mafunzo kwa watendaji wa Asasi, mradi wa *SELF* pia unagharamia mafunzo kwa walengwa ambao ni wafanyabiashara wadogo ili kujenga taaluma *(business skills)* ya uendeshaji wa biashara kwa faida na katika hali ya ushindani. Mafunzo hayo yanajumuisha uwekaji kumbukumbu, kupanga bei kutokana na gharama za uzalishaji, kutafuta masoko, kutangaza bidhaa n.k. Hadi Juni 2005, walengwa wapatao 692 walinufaika na mafunzo hayo mwaka jana. Idadi hii inafanya jumla ya walengwa 1,410 walionufaika na mafunzo tangu mradi uanze kufikia 1,410. Aidha, zilifanyika jitihada za kuhamasisha jamii na kushawishi asasi nyingi zaidi zijitokeze kushirikiana na mradi katika kutoa huduma ya mikopo katika maeneo ya mradi, na hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliendelea kusimamia utekelezaji wa *TASAF* kwa kuzingatia kwamba Awamu ya Kwanza ya mradi ilikuwa ikiishia Desemba 2004. Juhudi kubwa ilielekezwa kukamilisha utekelezaji wa miradi iliyokuwa imeanzishwa. Katika kipindi hicho, miradi 398 ilitekelezwa na kukamilika tayari kwa kutoa huduma kwa walengwa. Kati ya idadi hiyo, miradi ya jamii ilikuwa 222, miradi ya ujenzi ilikuwa 133 na miradi ya makundi maalum ilikuwa 42.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika jitihada za kuboresha mipango ya kuongeza kasi ya kuondokana na umaskini imeanzisha mpango utakaosaidia kurasilimisha rasilimali na biashara za wanyonge walio katika sekta isiyo rasmi. Kama Bunge lako Tukufu lilivyoelezwa wakati wa Semina ya Waheshimiwa Wabunge iliyofanyika mwezi Aprili 2005, dhana ya Mpango wa Kurasilimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) au *Property and Business Formalization Programme - PBF* ni ushirikishwaji wa Watanzania walio wengi katika mfumo wa kitaifa wa umilikaji mali na uendeshaji biashara kama njia mojawapo ya kupiga vita umaskini na hivyo kuboresha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu ni miongoni mwa mipango maalumu iliyoanzishwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza uchumi na kuondoa umaskini. Madhumuni ya MKURABITA ni kuandaa mfumo wa kitaifa wa umiliki mali na uendeshaji biashara utakaoanisha na kuboresha kanuni na taratibu zinazotumiwa na makundi mbali mbali nchini na kuwa na mfumo mmoja wa kisheria, ili walengwa waweze kuutumia mfumo huo kupata mitaji ya kugharamia shughuli zao kadri ya utashi wao, na pia wawe washiriki katika uchumi wa soko la ndani na nje ya nchi. Mpango huu utawawezesha wananchi kupata hati miliki ya mali zao kama vile ardhi, nyumba na biashara nyinginezo ambazo zitaweza kutumika kama dhamana katika kukopa fedha benki na hivyo kujiendeleza katika biashara mbalimbali, kuongeza vipato vya Watanzania na kuchangia kuendeleza uchumi wa Taifa. Aidha upatikanaji wa hati miliki utamhakikishia Mtanzania haki ya kisheria ya kumiliki mali aliyonayo bila kubugudhiwa na mtu yoyote. Walengwa mahususi wa mpango huu ni Watanzania, wanawake, wanaume na vijana wanaomiliki mali na kuendesha biashara katika sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha fedha 2004/2005, *NIGP* iliendelea kusimamia ukamilishaji wa miradi mbalimbali pamoja na kusimamia na kufuatilia Jumuiya mbalimbali za wananchi zilizokabidhiwa dhamana ya kuendeleza shughuli za miradi baada ya taratibu za ufadhili wa miradi hiyo kukamilika. Kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ya Serikali pamoja na kutokukamilika taratibu za kupata fedha zilizoahidiwa na Serikali ya Ubelgiji, *NIGP* haikuweza kutengewa fedha za maendeleo katika kipindi hicho. Kwa sababu hizo, *NIGP* haikuweza kukamilisha miradi kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 ilielekeza nguvu katika utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika misingi ya kuanza rasmi usajili wa *NGOs* chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Usajili huu umehusisha *NGOs* za Kitaifa, Kimataifa na pia utoaji wa vyeti vya ukubalifu (*certificate of compliance)* kwa *NGOs* ambazo zimesajiliwa katika Sheria nyingine nchini. Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 ndiyo Sheria pekee nchini ambayo imeweza kutoa ainisho na sifa za Shirika Lisilo la Kiserikali, hivyo ni sheria ambayo inalenga kuunganisha *NGOs* zote nchini kwa maslahi ya Watanzania wote. Napenda kusisitiza kwamba Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuunganisha nguvu na kufanya utafiti wa kina ambao utasaidia kuleta mabadiliko ya utendaji kazi wa *NGOs* ikiwa ni pamoja na kufanya mabadiliko ya Sheria hii ili kuboresha mazingira yatakayopelekea ukuaji wa sekta ya *NGOs* nchini.

Kwa misingi hiyo Serikali haitarajii kwamba kutakuwepo na mkanganyiko wa kushindwa kutambua *NGO* halisi ni ipi katika mazingira ya Kitanzania kwa kuwa vigezo halisi na sifa ambazo *NGO* inapaswa kuwa navyo vimeainishwa vizuri kwenye Sera ya Taifa ya *NGOs* ya mwaka 2001 na katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa sheria yeyote mpya sharti uendane na mpango mahsusi wa kuhakikisha kwamba wadau wanaelewa vyema taratibu na kanuni za utekelezaji wake. Kwa kutambua umuhimu huo, na hasa nia ya kuwaondolea wananchi usumbufu katika usajili, ofisi yangu ilitoa matangazo kwenye magazeti ya Kiswahili na Kiingereza na pia kufanya mahojiano kwenye Luninga katika kipindi cha 'Sema Usikike' kinachorushwa hewani kupitia *ITV.* Jitihada hizi zimesaidia sana kutoa mwanga na kuongeza weledi kwa wananchi hivyo kuwapatia fursa ya kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa usajili wa *NGOs* chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na matakwa ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002, ngazi za usajili zimegawanyika katika Wilaya, Mkoa na Kitaifa. Katika ngazi ya Wilaya na Mkoa, Maafisa Tawala (W) na Maafisa Mipango (M) waliteuliwa rasmi kuwa Wasajili Wasaidizi ili kurahisisha usajili wa *NGOs* kwa niaba ya Msajili Mkuu wa *NGOs* katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha, kwa kuwa sheria hii ni mpya katika utekelezaji wake yamegundulika maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho ya haraka ili kurahisisha utekelezaji wake kama vile kuondoa ulazima wa *NGOs* kusajili mara mbili kwa kuongeza kipengele ambacho kitazipa *NGOs* zilizosajili chini ya sheria ya *NGOs* kupewa hadhi ya kisheria (status). Maoni kuhusu maeneo hayo na mapendekezo hayo tayari yamekusanywa kwa kushirikisha wadau kupitia Baraza la Taifa la *NGOs*. Mchakato wa kukusanya maoni haya ulisimamiwa na

Baraza la Taifa la *NGOs* kwa kufanya warsha za kikanda, mkutano wa Baraza hilo ambao ulijadili na kupitisha maoni hayo ya wadau na hatimaye kuyawasilisha kwa Msajili Mkuu. Aidha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* iliyapitia maoni hayo na kuagiza utaratibu wa kufanya marekebisho ya sheria ufuatwe. Mapendekezo ya marekebisho hayo ya sheria hii yamewasilishwa katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuongeza ufanisi, Serikali imeajiri watumishi 19 kushika nafasi mbalimbali katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha, katika mwaka wa fedha 2004/05 jumla ya watumishi 26 wamethibitishwa kazini baada ya kukidhi masharti ya miundo ya kazi inayowatawala. Ili kuongeza ujuzi, jumla ya Watumishi 44 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwenye vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi. Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea na juhudi za kuwaendeleza watumishi ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, tekinolojia na kijamii yanayoendelea nchini na duniani kote kwa kuzingatia suala zima la utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zilifanyika za kuanzisha Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tanzania Zanzibar. Napenda kulialifu Bunge kuwa tumefanikiwa kupata sehemu eneo la Tunguu kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, na Kilimani kwa ajili ya makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais. Eneo la awali la Mwanakwerekwe lililokuwa limekusudiwa kujengwa majengo hayo litatumiwa kwa shughuli nyingine za Serikali kadri itakavyokubalika. Taratibu zinaendelea kufanyika ili tupatiwe maeneo hayo rasmi. Baada ya kukabidhiwa rasmi maeneo hayo maandalizi ya ujenzi yataanza na ujenzi kufanyika mara tu baada ya mkandarasi kupatikana. Kazi ya maandalizi inajumuisha gharama za michoro, kupima udongo na kumtafuta mkandarasi. Serikali imetenga fedha za ndani sh. 747,000,000/= katika mwaka wa fedha 2005/06 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo hayo Tanzania Zanzibar.

Napenda pia kuliarifu Bunge kuwa ujenzi wa jengo la kudumu la Ofisi ya Makamu wa Rais Tanzania Bara, umeanza mwezi Januari, 2005 na kazi inaendelea vizuri kwani ukaguzi wa jengo uliofanyika mwezi Juni 2005 unaonesha kuwa kazi iliyokwishafanyika ni moja ya tatu ya kazi yote. Ujenzi unatarajia kumalizika katika kipindi cha wiki 78, yaani kabla ya mwaka wa fedha 2006/07 kuanza. Fedha zilizotengwa katika mwaka 2004/05 zimetumika kumlipa mkandarasi kugharamia ujenzi huu kama vile kulipa mafundi, gharama za kununua vifaa vya ujenzi, kuchora njia za umeme n.k.

Aidha, Serikali ilinunua jengo la Ofisi ya Kudumu ya Kituo cha Uzalishaji Bora Tanzania (kituo kinachodhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na viwanda) kama hatua ya utekelezaji wa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Wafadhili wa Kituo ambao ni Serikali ya Norway. Katika makubaliano hayo Serikali ya Tanzania inatakiwa kutoa jengo la Ofisi kama mchango wa Serikali ili Serikali ya Norway iendelee kusaidia Kituo katika miradi yake. Kupatikana kwa jengo hilo kutasaidia sana kukwepa usumbumbu unaotokana na upangishaji wa ofisi na pia itapunguza gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la UKIMWI limeendelea na litaendelea kutiliwa mkazo. Mwaka 2004/05 Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na *TACAIDS* imeendesha semina mbili kwa watumishi wote pamoja na wale wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kuwakumbusha athari za UKIMWI, utaratibu wa kupima UKIMWI na namna ya kujikinga na maambukizo na tiba.

Aidha, timu ya wataalam iliyoteuliwa na *TACAIDS* ilifanya savei kutambua uenezi wa UKIMWI kwa watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Utafiti huo ulifanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana kati ya wataalam na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, wadau wengine na Viongozi. Aidha, mtindo wa dodoso *(Questionnaire)* pia ulitumika. Ripoti ya savei hiyo ipo katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji. Ripoti hii itatoa mapendekezo yatakayochangia jitihada za kupambana na UKIMWI na hasa katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la ushirikishwaji wa wafanyakazi, Baraza la Wafanyakazi limefanya vikao mara mbili yaani mwezi wa Septemba 2004 lilikutana Arusha na mwezi Aprili 2005 lilikutana Tanga. Katika vikao hivyo wajumbe wa Baraza walijadili masuala yanayohusiana na maslahi ya watumishi yakiwemo sheria mpya ya ajira Na. 8 ya mwaka 2002, Nyaraka mbalimbali zinazohusu maendeleo ya Watumishi, kanuni na taratibu za fedha na manunuzi. Aidha, katika kikao kilichofanyika Mkoani Tanga, pamoja na masuala mengine, wajumbe wa Baraza walijadili na kuipitisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2005/2006 kama mojawapo ya kazi za Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea na majukumu yake ya kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya Kiserikali, kuratibu na kusimamia shughuli zote za Muungano, masuala ya mazingira, kupambana na umaskini, na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/06, Serikali itaweka mkazo katika shughuli kubwa zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kushughulikia masuala ya Muungano kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kero mbalimbali zilizoainishwa katika Kamati ya Shellukindo. Aidha, suala la kukuza uchumi na kupunguza umaskini, na uboreshaji wa mazingira kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vitapewa kipaumbele. Juhudi hizi zitajumuisha:-

(i) Kufanya utafiti kwa kutumia tekinolojia ya kisasa kwa masuala ya Muungano na mambo ambayo siyo ya Muungano na kutoa mapendekezo;

(ii) Kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya serikali kutokana na mikutano mbalimbali mashirikiano;

(iii) Kutoa elimu kwa Umma juu ya umuhimu wa Muungano wetu kupitia vipindi vya Redio na Televisheni, na kuandaa vijarida vya Muungano na kuvisambaza

kwa Wadau kwa lengo la kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya muungano na kukuza ushirikiano katika kuleta maendeleo ya wote.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, Sheria ya Mazingira imeanza kutumika tangu Julai mosi 2005. Katika kipindi cha 2005/2006 malengo yatakuwa:- kukamilisha kanuni zake, kujenga uwezo wa wadau ili waweze kuisimamia ipasavyo na kukuza weledi kwa wananchi ili waielewe na kuitekeleza sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 mradi wa Ziwa Victoria unatarajia kutumia jumla ya shilingi bilioni 1.7 katika kutekeleza kazi zifuatazo;

(a) Kuendelea kudhibiti magugumaji kwa kuzalisha na kusambaza mbawakavu wapatao milioni 42 katika Ziwa Victoria, Maziwa madogo madogo *(Sattelite lakes),* mito, mabwawa na kwenye maeneo korofi *(hot spots)* na kufuatilia matukio ya magugumaji. Aidha, Mradi utaendelea na mkakati wa kudhibiti magugumaji katika Mto Kagera kwa kuzishirikisha nchi za Rwanda na Burundi na kufanya utafiti wa kina katika mto huu ili kubaini sababu zinazofanya mbawakavu kushindwa kushamiri katika eneo hili.

(b) Kutoa mbinu bora za uvuvi, kuimarisha ulinzi dhidi ya uvuvi haramu na kuhifadhi mazalio ya samaki katika bonde la Ziwa Victoria kwa kushirikisha wananchi na vikundi vya ulinzi wa rasilimali *(Beach Management Units).* Aidha, Mradi utaimarisha ufugaji bora wa samaki katika mabwawa katika kanda ya Ziwa ikiwa pamoja ni na kusambaza kwa wafugaji vifaranga vilivyo bora zaidi.

(c) Kuendelea na utafiti kuhusu ubora wa maji katika vituo 126 vilivyojengwa katika Bonde la Ziwa Victoria na katika maeneo yaliyo karibu na makazi ya watu ili kubaini uchafuzi utokao katika maeneo haya.

(d) Kuimarisha na kufuatilia utekelezaji wa *Cleaner Production* katika viwanda 12 vinavyotekeleza program hii ili kubaini punguzo katika viwango vya uchafu unaoingia Ziwani kutokana na shughuli za viwanda hivi.

(e) Kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhifadhi misitu asilia, ardhi owevu na kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kukuza miche ya miti ipatayo milioni 1.6 na kuisambaza kwa wakulima.

(f) Kuendeleza ukarabati wa maeneo owevu kwa kushirikiana na vijiji na wilaya kama ilivyo katika mipango ya matumizi bora ya maeneo haya

(management plans) ya vijiji na wilaya husika na kuvijengea uwezo wa matumizi bora ya maeneo haya.

(g) Kukamilisha miradi midogo midogo 14 inayoendelea na kuhamasisha vijiji na wilaya husika kupanda miti ipatayo 50,000 kwenye maeneo ya miradi midogo midogo iliyokwishaanzishwa ili kuboresha mazingira katika maeneo husika.

(h) Kuendelea kugharamia mafunzo ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya shahada ya Uzamili (*Masters*) na Falsafa (*Ph.D.*).

(i) Kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wadau wote wa Kanda ya Ziwa Victoria juu ya hifadhi ya mazingira ya Ziwa kwa njia ya redio, luninga, warsha, magazeti, vijarida na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya programu hii yatakuwa kuajiri watumishi na wataalamu wa miradi; kununua vifaa vya miradi; kutoa mafunzo kwa wataalamu wa serikali za mitaa na vijiji; na kukuza weledi kuhusu masuala ya mazingira ya ziwa na bonde lake. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea na juhudi zake za kufanya majadiliano na wafadhili wengine walioonyesha nia ya kugharimia shughuli mbalimbali za utekelezaji wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/06 Kituo cha Tekinolojia na Maendeleo endelevu kitaajiri wataalam mbalimbali. Warsha juu ya mafanikio ya utekelezaji wa mbinu za uzalishaji bora na semina ya kukuza ufahamu wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu kwa wadau mbalimbali zitafanyika. Pia Kituo kitaendelea kuratibu shughuli za Sekretariati ya *African Roundtable on Sustainable Consumption and Production*; na kufanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati *(Cleaner Production Assessments)* viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatekeleza mradi wa kujenga uwezo na kupiga vita umaskini kupitia utekelezaji wa pamoja wa Mikataba ya kimataifa ya Mazingira *(Multilateral Environmental Agreements – MEAs).* Mikataba itakayohusika na mradi huu ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame, Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mkataba wa kuhifadhi Bioanuwai. Mradi huu umetokana na utekelezaji wa mpango wa mazingira wa *NEPAD* na unafadhiliwa kwa pamoja kupitia serikali za Norway na Ubelgiji. Katika utekelezaji wa mradi huu kamati ya kitaifa ya kuratibu utekelezaji wake imeundwa na kuanza kufanya kazi. Utekelezaji wa mradi huu utakuwa wa miaka mitatu na utakwenda sambamba na uwezeshaji wa kifedha kwa *NGOs* na asasi mbalimbali zinazoshughulika na kupiga vita umaskini na utunzaji wa mazingira, katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na mikataba ya kimataifa ya mazingira iliyotajwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*NAPA*) utakamilishwa. Mpango utaainisha maeneo ya kipaumbele, na miradi

ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi itaandaliwa na kuwasilishwa kwa wafadhili kwa ajili ya kupatiwa fedha. Uhamasishaji kwa njia ya warsha mbalimbali kwa ajili ya kukuza weledi utaendelea kuhusu miradi ya *CDM* na Mkataba kwa ujumla; na maandalizi ya Ripoti ya pili ya kitaifa *(Second Initial National Communication)* kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi yataanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame, mradi wa kuimarisha uwezo wa serikali katika kupambana na hali ya kuenea kwa jangwa na ukame nchini utatekelezwa. Mradi huu unalenga kuimarisha uwezo wa serikali hususan kupitia serikali za mitaa ili mipango inayotekelezwa katika ngazi za Wilaya iweze pia kulenga katika tatizo hili la kuenea kwa hali ya jangwa na ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005/06, uboreshaji wa miundombinu katika hifadhi na maeneo yanayozunguka hifadhi za Tarangire na Manyara utaendelea. Pia vijiji vinavyozunguka hifadhi za Tarangire, Manyara na Hifadhi ya Akiba ya Ugalla vitasaidiwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, na kuanzisha hifadhi za jamii (*WMAs*). Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendesha warsha kwa wataalamu kutoka sekta husika, serikali za mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara na watumiaji wa kemikali mbalimbali watahamasishwa kupunguza uingizaji na utumiaji wa kemikali zinazomong'onyoa ukanda wa ozoni na kuingiza kwa wingi kemikali mbadala. Mafunzo kwa mafundi mchundo na maafisa forodha yatatolewa. Pia mashirika na makampuni yaliyopewa vifaa vya kusafisha na kurudufu kemikali aina ya *CFCs* watahimizwa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa gesi hii. Vifaa vya kutambua kemikali hizi kwenye mitungi mipya ya gesi inayoingizwa nchini vitaagizwa; na uandaaji wa kanuni za kemikali zinazomong'onyoa ukanda wa hewa ya Ozoni utakamilishwa.

Aidha, warsha ya kitaifa juu ya mkakati wa kupenyeza tekinolojia nadhifu katika sekta zilizobainishwa katika uchunguzi wa mwaka 2004 itafanyika; mafunzo kwa wadau juu ya mbinu za kisasa za kuzima moto zisizotegemea gesi aina ya halons yatafanyika; na miongozo ya kusimamia matumizi ya kemikali aina ya halons inayotumika kuzimia moto kwenye maeneo nyeti *(essential uses)* kama vile kwenye ndege (*aviation*) na magari maalum ya kijeshi *(military tactical vehicles)* itaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, warsha ya Kanda ya Afrika kwa nchi za *SADC* itaandaliwa hapa nchini ili kujadili matokeo ya uchunguzi wa kemikali hizi na kuweka mikakati na mipango ya kikanda kuhusu usimamizi wake, upatikanaji wa kemikali na tekinolojia mbadala, mafunzo kwa mafundi umeme, na uboreshaji wa sheria na kanuni na utekelezaji wa mipango ya kikanda. Vilevile miradi kuhusu maeneo ya kipaumbele ya usimamizi na matumizi ya kemikali hizi itaandaliwa na kuwasilishwa kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo yatakuwa kukamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa kuundwa Kituo cha Kanda cha Mafunzo na Usambazaji wa Tekinolojia

katika utekelezaji wa Mkataba wa *Basel*. Kituo kitashughulikia mikakati ya upatikanaji wa fedha *(Resource mobilization strategy)* kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya usimamizi wa taka za sumu; mafunzo kuhusu usimamizi wa taka zenye sumu kwa maofisa wa Idara na Taasisi za Serikali na viongozi wa ngazi za juu serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo katika mwaka 2005/2006 ni kuendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za miradi iliyokwisha wasilishwa na mipya itakayoandaliwa na kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2005/2006, na baada ya maandalizi ya muda mrefu, Baraza linatarajia kuanza programu ya ukusanyaji na uteketezaji wa madawa chakavu (*ASP*) kwa mikoa yote ya Tanzania Bara hususani kuanzia mwezi Septemba 2005. Programu hii itasaidia kuboresha maeneo yaliyoathirika zaidi na madawa chakavu katika sehemu ambazo zimebainishwa. Vile vile, Baraza litaweka utaratibu wa kudhibiti uchafuzi wa mazingira kulingana na matakwa ya Sheria ya Mazingira ya 2004.

Aidha, Baraza linategemea kutekeleza mradi wa utafiti kuhusu udhibiti wa uchafuzi wa Bonde la mto Msimbazi kwa ufadhili wa mradi maalumu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kusimamia mazingira (*UNEP-GPA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2005/2006 Baraza pia linatarajia kuendelea kukamilisha uandaaji wa Mpango wa Utafiti wa Mazingira *(Environmental Research Agenda)* ikiwa kama dira ya utafiti wa mazingira hapa nchini. Mpango huo unazingatia maeneo ya kipaumbele katika nyanja mbalimbali za hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na maeneo ya mikataba ya mazingira ambayo serikali yetu imeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupambana na kasi ya umaskini Baraza linatarajia kutoa mafunzo kwa wasusi wanaoishi mwambao mwa Ziwa Victoria ili waweze kutengeneza bidhaa nzuri zaidi ambazo zinaweza kutoa ushindani katika soko la nje ya nchi. Shughuli hii ya kutoa mafunzo imeshaanza kutoa matunda wilayani Magu kwani kipato cha wasusi kimepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza litaendelea kuziwezesha wilaya zilizomo mwambao wa Ziwa Victoria kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuhifadhi maeneo owevu. Mikakati hiyo imekwisharidhiwa na wanavijiji vitano vinavyozunguka maingilio ya mto Simiyu wilaya ya Magu. Aidha katika kipindi hiki cha 2005/2006 Baraza linatarajia kuendelea kuwahamashisha wanavijiji kutengeneza mikakati hiyo na kuridhiwa na vijiji kadhaa vya Wilaya za Musoma, Geita, Bunda, Bukoba, Misungwi na Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza litaendelea kushirikiana na wananchi wa mwambao wa Bahari ya Hindi katika shughuli za kuhifadhi mazingira ya maeneo ya pwani. Aidha wananchi wa wilaya ya Kilwa, Lindi, Mtwara na Tanga watashirikishwa katika kuandaa mipango ya uwiano wa kuhifadhi maeneo ya pwani katika wilaya zao na

kuanza kuitekeleza. Aidha Baraza litaendelea na mpango wa Tuzo ya Hifadhi ya Mazingira ya maeneo ya pwani (*Coastal Environmental Award Scheme)* kwa lengo la kuwahamasisha wananchi wazidi kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zitakazofanyika ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa MKUKUTA; kufanya mapitio ya Mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA (2004) ili uende sambamba na malengo ya MKUKUTA; kutafsiri MKUKUTA kwa lugha rahisi (Kiingereza na Kiswahili) na uchapishaji wa vijarida na vipeperushi kwa uelimishaji zaidi; na kuratibu jitihada za kuelimisha na kuhamasisha jamii kama vile usambazaji wa taarifa mbalimbali, na utumiaji wa mbinu shirikishi ili kujenga ufahamu wa wananchi katika kuuchukia na kuupiga vita umaskini. Kazi nyingine zitakazopewa kipaumbele katika jitihada za kuongeza kasi ya kupunguza umaskini ni utekelezaji wa mfuko wa *TASAF*-II, MKURABITA, *SELF* na *NIGP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mafanikio ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mradi wa *TASAF* katika wilaya 40 za Tanzania Bara na visiwa vya Pemba na Unguja kwa upande wa Zanzíbar, Serikali iliamua kuwa na awamu ya pili ya *TASAF* ambayo itatekelezwa katika Halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2005 hadi 2009. Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Dunia iliridhia na kupitisha Mradi wa awamu ya pili ya *TASAF* tarehe 30 Novemba 2004. Mkataba kati ya Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulisainiwa tarehe 19 Januari 2005. Awamu hii ilizinduliwa tarehe 23 Mei 2005 kule Magu, Mwanza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamín W. Mkapa.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006, *TASAF* itajihusisha na utekelezaji wa Awamu ya Pili. Kazi zitakazofanyika ni utoaji wa mafunzo kuhusu taratibu za utekelezaji katika ngazi zote kuanzia taifa hadi vijijini, uwekaji wa mifumo ya ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi kwa wananchi wenyewe kuainisha vipaumbele na kutengeneza mipango kazi itakayoongoza utekelezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine itakayopewa uzito mkubwa katika mwaka wa fedha unaokuja ni kuendelea kutekeleza MKURABITA. Hii itajumuisha kukamilisha kazi zifuatazo: ushirikishwaji wa wananchi katika kutambua kero zao na kutafuta ufumbuzi katika maeneo mbalimbali, ili kuweka taratibu na kanuni zitakazosaidia katika umilikaji mali na kutumia mali hizo katika kufanya biashara; kuendelea kuboresha jitihada za usimamizi wa sheria za umilikimali, biashara, ajira, na kodi ili kulinda mali za wananchi zisipotee; kuboresha Taarifa ya Tathmini inayoandaliwa; na kuandaa Mpango wa Maboresho *(Reform Design).*

Aidha, uelimishaji na uhamasishaji utafanyika kwa wananchi kuhusu dhana nzima ya MKURABITA na umuhimu wake katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini ili sote tushiriki katika utekelezaji wake ambao utasaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha maisha ya watu na kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kupanua huduma ya mikopo kwa kutoa mikopo kwa asasi za kifedha mikoa yote 14 inayotekeleza mradi wa *SELF*. Utoaji wa mafunzo kwa watendaji wa asasi za kifedha na wakopaji wa mikopo hiyo utapewa kipaumbele ili kuboresha utoaji wa mikopo na kuongeza ufanisi katika kutumia mikopo hiyo ambayo itasaidia kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Mkazo utawekwa pia katika uelimishaji na uhamasishaji wa jamii ili kuongeza ari katika kufanya kazi mbalimbali za kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendeleza shughuli za *NIGP* za kukamilisha na kupanua miradi minane inayolenga kuongeza vipato vya wananchi. Aidha utaratibu unaendelea wa kuandaa utekelezaji wa miradi mipya katika mikoa ya Pwani na Kigoma ambayo itatekelezwa kwa kutumia fedha zilizoahidiwa kutolewa na Serikali ya Ubelgiji. Jitihada zinaendelea kufanyika kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.8 *(Euro 2,169* milioni) kilichoahidiwa na Serikali ya Ubelgiji, kwa utekelezaji katika kipindi cha miaka mitano.

Aidha, Serikali pia imetenga fedha za ndani kiasi cha shilingi 210 milioni kwa ajili ya kuendeleza miradi iliyoonyesha mafanikio makubwa katika kupunguza umaskini. Juhudi za kuboresha miradi ya *NIGP* ni sehemu ya utekelezaji wa MKUKUTA.

Mweshimiwa Spika, katika kipindi cha kwa mwaka wa fedha 2005/2006 Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya kuratibu, kusimamia, ufuatiliaji na kuweka mazingira bora ya kazi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza kazi zao. Msingi mkubwa ni kuhimiza utekelezaji thabiti wa Sera ya Taifa ya *NGOs* na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002.

Serikali itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Sheria hii, kwa kushirikiana na Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs*, Baraza la Taifa la *NGOs* na Wasajili Wasaidizi wa *NGOs* ili kubaini maeneo yenye kuhitaji kufanyiwa utafiti wa kina kwa nia ya kuhakikisha kwamba wadau wanaielewa na kuitekeleza vyema sheria hii.

Aidha, jitihada zitafanyika hasa katika kuimarisha mahusiano mazuri kati ya Serikali na sekta ya *NGOs*, sekta ya *NGOs* wenyewe, sekta ya *NGOs* na kiraia na wadau wengine ili kuleta na kuimarisha mshikamano wetu katika kukabili changamoto za mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mwelekeo utakuwa hasa kuhimiza kila sekta kutekeleza majukumu yake kikamilifu, kubadilishana taarifa na kuunganisha nguvu inapohitajika ili kupata mafanikio ya pamoja. Serikali ina nia ya kuimarisha ufuatiliaji wa shughuli za *NGOs*, hivyo msukumo utakuwa hasa kubuni mkakati utakaosaidia kuimarisha mpango madhubuti wa utunzaji wa kumbukumbu za orodha ya *NGOs* na shughuli zao kote nchini, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa utoaji wa taarifa ya kazi na taarifa ya fedha ya mwaka ya mashirika hayo.

Lengo hasa ni kuiwezesha Serikali na wadau wote kwa ujumla kubaini na kutambua kiwango cha mchango wa *NGOs* katika pato la taifa na uchumi kwa ujumla. Aidha, wananchi, wahisani na wadau wengine wataweza kupata fursa ya kuona taarifa za kazi za *NGOs* na mahesabu kupitia kwa Msajili wa *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi zitaendelea kufanyika kuboresha mazingira ya kazi ili kuongeza ufanisi. Hii itajumuisha: kuwaendeleza watumishi ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, tekinolojia na kijamii yanayoendelea nchini na duniani kote kwa kuzingatia suala zima la utandawazi; kuendelea kupambana na ugonjwa wa hatari wa UKIMWI na mkazo utakuwa katika kuboresha utekelezaji wa mpango wa kuthibiti UKIMWI wa Ofisi ya Makamu wa Rais unaolenga kupambana na UKIMWI katika maeneo ya kazi kama vile kukwepa maambukizi mapya na kutoa dawa za kuongeza kinga ya mwili ili kuongeza muda wa kuishi.

Jitihada pia zitafanyika kusimamia utekelezaji wa *OPRAS* kulingana na taratibu zilizotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Aidha, shughuli nyingine zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Tanzania Bara pamoja na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais na makazi ya Makamu Zanzibar. Kiasi cha sh. 747,000,000/= kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais na Makazi ya Makamu wa Rais Zanzibar, na sh. 1,200,000,000/= kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake thabiti na maelekezo yake yaliyoiwezesha Ofisi yetu kutekeleza vizuri majukumu yake.

Namshukuru Mheshimiwa Pius Msemkwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania, Mheshimiwa Juma J. Akukweti Naibu Spika kwa kuongoza Bunge hili tukufu. Pia nawashukuru wenyeviti Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Eliachim Simpasa kwa kuongoza Bunge hili Tukufu.

Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu Mwandamizi, Bwana Raphael Mollel; na Katibu Mkuu, Bibi Mary Mushi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Wakurugenzi na wafanyakazi wote kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao ipasavyo katika kipindi kilichopita. Namshukuru pia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapa maelezo haya kwa unadhifu wa hali ya juu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wahisani mbalimbali ambao wamekubali na wameendelea kusaidia Serikali ya Tanzania kugharamia miradi mbalimbali katika kuratibu utekelezaji wa mikakati ya kupambana na umaskini, usimamizi na hifadhi ya mazingira, na kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Wahisani hao ni pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo (*UNDP*), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Misaada na Maendeleo la Sweden (*SIDA*),

Shirika la Misaada na Maendeleo la Norway (*NORAD*), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Serikali ya Denmark, Serikali ya Japan, Uholanzi, Finland, Ireland, Shirika la Maendeleo la Uingereza (*DFID*), Shirika la Maendeleo *la* Marekani *(USAID*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda *(UNIDO),* Shirika la Maendeleo la Uswisi (*SDC*), Mfuko wa Mazingira wa Dunia – *GEF*", Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (*UNEP*), *International Development Agency* (*IDA*), *Organization of the Petroleum Exporting Countries (OPEC),* Shirika la *OXFAM*, *FAO*, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, sekta mbalimbali, sekta binafsi na wananchi wote. Tunawashukuru wote kwa kuchangia kwa hali na mali juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kupunguza umaskini ili kuleta maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

**Fungu 26 - Makamu wa Rais**

Katika mwaka huu wa fedha 2005/2006 kiasi cha shilingi bilioni moja, millioni mia saba tisini na sita, laki nane ishirini na tisa elfu na mia nane (1,796,829,800/=) kinaombwa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida Ofisi ya Makamu wa Rais *(Private Office).*

Kati ya fedha hizi shilingi milioni mia moja tisini na moja, laki nane ishirini na tisa elfu, na mia nane (191,829,800/=) ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi, na shilingi bilioni moja, milioni mia sita na tano (1,605,000,000/=) kwa ajili ya matumizi mengine ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba kiasi cha shilingi bilioni ishirini na tisa, milioni mia tisa thelathini na tatu, laki tano hamsini na tano elfu, na mia tano (29,933,555,500/=) kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi milioni mia tatu tisini na tatu, arobaini na tano elfu na mia tano (393,045,500/=) ni mishahara ya watumishi Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi milioni mia nne na tisa ishirini na tano elfu (409,025,000/=) ni ruzuku ya mishahara *NEMC*.

Shilingi bilioni ishirini na nne, milioni hamsini na moja, laki nane na mia nne (24,051,800,400/=) ni kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Shilingi milioni mia mbili sitini na sita, laki mbili hamsini na tano na mia saba (266,255,700) ni ruzuku ya matumizi ya kawaida *NEMC*, na Shilingi bilioni nne, milioni mia nane kumi na tatu, laki nne ishirini na nane elfu na mia tisa (4,813,428,900/=) ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha shilingi bilioni ishirini na saba, milioni mia nane thelathini na nane, laki laki nane thelathini na moja elfu, na mia mbili (27, 838,831,200/=) kinaombwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kati ya fedha hizi, fedha za ndani ni shilingi bilioni moja na milioni mia sita sabini na mbili (1,672,000,000/=) na fedha za nje ni shilingi bilioni ishirini na sita milioni mia moja sitini na sita, laki nane thelathini na moja elfu na mia mbili (26,166,831,200/=) ndicho kinachoombwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mwakilishi wa Kamati. Ningependa kutoa taarifa ambayo ningepaswa kuitoa mapema kwamba leo humu ndani ya Bunge kama mnavyoona Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo. Kwa hiyo, amemteua Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, kuwa Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Bunge hapa ndani. Kwa hiyo, tunaombwa tumpe ushirikiano, ndiyo Kaimu leo. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, sasa namwita Mwakilishi wa Kamati -Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman.

**MHE. ISSA MOHAMMED SULEIMAN (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA -MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu Na.81(1) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2004, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa Fedha uliopita wa 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni ya Kamati yangu, ningependa kutumia fursa hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati yangu kutoa salaam za rambirambi kwa familia na wananchi wote wa Jimbo la Kilombero kwa msiba wa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga aliyefariki dunia tarehe 2 Juni, 2005. Pia, tunatoa pole kwa familia na wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kuondokewa na Mbunge wao Marehemu Margareth Bwana aliyefariki dunia tarehe 23 Juni, 2005. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa

kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais kwa Chama hicho na Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Mgombea mwenza. Pia, nampongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume, Rais wa Zanzibar kwa kuteuliwa na CCM kugombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM. Nawapongeza na Wagombea wengine wa Urais walioteuliwa na Vyama vyao kuwania nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Maliasili na Mazingira imeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni 101(1) ya Toleo la 2004 na ningependa kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan R. Khatib Makamu Mwenyekiti na wafuatao ni Wajumbe wa Kamati:- Mheshimiwa Bahati A. Abeid, Mheshimiwa Aziza S. Ali, Mheshimiwa Shaib A. Ameir, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Sharifa M. Khamis, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa Ernest G. Mabina na Mheshimiwa Mariam S. Mfaki. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Mathew T. Ole-Timan, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Mohamed R. Soud. Mheshimiwa Esha H. Stima, Mheshimiwa Martha M. Wejja na mimi Mheshimiwa Issa M. Suleiman. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati yangu ikipitia na kuchambua Taarifa za Ofisi ya Makamu wa Rais zilizowasilishwa kwenye Kamati Dar es Salaam tarehe 31 Mei, 2005, masuala yaliyojadiliwa ni haya yafuatavyo:-

(i) Dira na Mwelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Rais;

(ii) Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais;

(iii) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2004/2005;

(iv) Maelezo kuhusu mapato na matumizi kwa kipindi kilichopita (2004/2005);

(v) Mafanikio na matatizo ya utekelezaji katika kipindi kilichopita (2004/2005);

(iv) Kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa (2005/2006;

(vi) Maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati; na

(vii) Maombi ya fedha za matumizi katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ni kuona kuwa Tanzania inaondokana na umaskini uliokithiri, mazingira bora, Muungano imara na kuona kuwa kuna ushiriki makini katika maendeleo ya Asasi zisizokuwa za Kiserikali yaani *NGO's.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata bahati ya kutembelea na kuona shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kamati imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Makamu wa Rais inavyotekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa juhudi walizozionyesha katika kutekeleza takriban maagizo yote yaliyotolewa na Kamati kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais iliweza kukusanya mapato ya Tshs.11,126,844/= hadi Aprili, 2005 kutoka Makadirio ya Tshs.1,243,756/= ukilinganisha na makusanyo ya Tshs.1,129,638/= kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Mapato haya yametokana na kodi ya pango, kuokoa upotevu wa fedha na mapato mchanganyiko. Kuhusu matumizi ya kawaida mwaka 2004/2005 hadi mwezi Aprili, 2005, Ofisi ya Makamu wa Rais ilitumia asilimia 73.45 ya fedha zote walizotengewa. Fedha za maendeleo waliyokadiria kwa mwaka 2004/2005 ni Tshs.11,043,071,400/= na fedha waliyopewa na kutumia hadi Aprili, 2005 ni Tshs.7,897,468,095/= tu. Kamati imeridhika na utekelezaji wa agizo lake la kutoa mchanganuo wa fedha za maendeleo ambazo zimetolewa na matumizi yake.

Hata hivyo, Kamati imeona kuwa fedha kwenye maeneo muhimu kama Kituo cha Mradi wa Usafi wa Mazingira katika uzalishaji viwandani yaani *Cleaner Production Centre of Tanzania (CPCT), National Income Generation Progromme (NIGP),* Mpango wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria *(Lake Environmental Management Programm*e *(LVEMP))* na *Participatory Environmental Resources* hakuna fedha iliyotolewa na Serikali hadi Aprili, 2005. Huu ni upungufu kwa upande wa Serikali kwani miradi hii ina umuhimu wa pekee katika kuhifadhi mazingira na kuongeza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005 ilipata nafasi ya kutembelea miradi inayotekelezwa na Taasisi mbalimbali chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Miradi mingi inafanyika kwa ustadi na mafanikio makubwa. Nchi yetu inao wataalamu wengi na waliobobea katika fani zao. Tunapenda kuwapongeza wataalamu wote katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambao wamefanikisha miradi mbalimbali katika Ofisi hii.

(i) Sheria Mama ya Mazingira ilipitishwa na Bunge lako Tukufu. Taarifa ambayo tumeipata ni kuwa Sheria hiyo imepata kibali cha Rais na kwamba maandalizi ya kanuni mbalimbali yanaendelea. Sheria hii ni muhimu sana kwa nchi yetu wakati huu ambapo nchi yetu imo katika mabadiliko makubwa ya kiuchumi; ikisimamiwa vizuri itawezesha nchi yetu kuepukana na madhara makubwa ya uharibifu wa kimazingira

ambayo nchi nyingi hata zilizoendelea nayapata hivi sasa. Elimu ya kutosha kuhusu sheria hii itolewe kwa wananchi kabla na wakati wa kuitekeleza.

(ii) Mikataba mbalimbali ya Kimataifa imeridhiwa na Bunge lako katika kipindi hiki, baadhi yake maandalizi ya utekelezaji yameendelea kufanyika; mfano, Mkataba wa Stockhom ambao unatoa ushauri kuhusu udhibiti wa kemikali zinazochukua muda mrefu sana kuoza na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabia nchini umeendelea kutekelezwa na taarifa ya utekelezaji wa Mkataba huo imekwishaandaliwa na itawasilishwa kwenye Sekretarieti ya Mkataba. Pia, Mkataba wa usimamizi endelevu wa Hifadhi ya Ziwa Tanganyika uliridhiwa na Bunge lako Tukufu katika kipindi hiki.

(iii) Kuratibu utekelezaji wa miradi na programu za hifadhi ya mazingira mfano:-

- Mradi wa kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya mazingira ya Manyara; Tarangire na Ugalla *(PERM);*

- Vijiji vya Narakauwo, Loiborsirel katika Wilaya ya Simanjiro vimetengenezewa mpango wa matumizi bora ya ardhi;

- Kituo cha mradi wa usafi wa mazingira katika uzalishaji viwandani; *Cleaner Production Centre* ya Tanzania *(CPCT)* kiliendelea kufuatilia na kuhamasisha juu ya dhana ya uzalishaji bora katika viwanda vya Miji ya Arusha, Tanga na Mwanza;

- Kamati ilitembelea viwanda ambavyo vinafanya shughuli za kurejeleza mifuko na vitu vya *plastic.* Kwa bahati nzuri vipo viwanda vingi ambavyo vimeanza kufanya kazi ya kurejeleza mifuko/bidhaa chakavu za *plastic.* Hivyo watu wengi wameanza kunufaika kutokana na kukusanya mifuko/bidhaa chakavu za *plastic* na kuuza viwandani;

- Viwanda vimetueleza kuwa *plastic* zile nyembamba kabisa haziwezi kurejelezeka. Hivyo, Serikali haina budi kupiga marufuku aina hii ya *plastic.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji wa mkakati wa hifadhi ya mazingira ya maeneo ya Pwani, katika Wilaya ya Pangani, Bagamoyo na Mkuranga chini ya mradi unaoitwa *Integrated Coastal Management Plan (ICM).* Kamati ilitembelea baadhi ya maeneo haya na kuona namna wananchi wanavyoshirikishwa kupanda mikoko ili kuzuia mmomonyoko wa fukwe za bahari. Wananchi pia wamehamasishwa kuhusu ufugaji wa samaki, ukulima wa mwani na nyuki badala ya uvuvi haramu.

Mafunzo maalum yametolewa kwa wananchi katika Vijiji vya mwambao mwa Ziwa Victoria katika Wilaya ya Magu kuhusu uhifadhi wa Ziwa hilo. Mipango ya

kutekeleza mradi wa kudhibiti uchafu wa bonde la mto Msimbazi unaendelea kufanyika. Shughuli mbalimbali za tathmini ya athari kwa mazingira *(EIA)* zimeendelea kufanyika katika hatua mbalimbali. Habari za mazingira na uhamasishaji wananchi kuhusu hifadhi za mazingira zimeendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali ya jamii.

Katika kipindi hiki Serikali imekamilisha Mpango wa Awamu ya Pili wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini (MKUKUTA). Mpango huu umeshirikisha wadau wote, Serikali, *NGO's,* Taasisi, mbalimbali zikiwemo za kidini na wananchi. MKUKUTA umehusishwa kikamilifu katika bajeti ya Serikali katika Sekta zote zikiwemo Halmshauri zote za Wilaya na Miji kuanzia mwaka huu wa fedha 2005/2006. Wananchi wakiuelewa vizuri na kutekeleza kwa kushirikiana na Serikali kwa juhudi na maarifa, hapana shaka mpango huu utafanikiwa. Ni muhimu Watanzania wote tuuelewe vizuri na kuukubali. Changamoto hapa ni kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na sekta zote ziendelee kuelimisha wananchi katika maeneo yao kuhusu dhana ya MKUKUTA.

(ii) *TASAF* ni sehemu pia ya MKUKUTA. Katika kipindi hiki tumeshuhudia kuanzishwa kwa *TASAF* awamu ya pili, ambayo itahusika nchi nzima. Dhana ya *TASAF* ni ushirikishi wa wananchi katika kujiletea maendeleo. Fedha iliyotolewa si nyingi sana, lakini pale ambapo wananchi wanaweka nguvu zao katika kutekeleza miradi ambayo *TASAF* wanahusika nayo basi maendeleo yao yatakuwa makubwa na ya haraka zaidi. *TASAF* ichukue jukumu la kujifunza kutokana na kasoro za awamu ya kwanza ili zisijitokeze katika awamu hii ya pili. Waheshimiwa Wabunge waelewe vizuri kuhusu dhana ya *TASAF* ya "Mfuko wa Taifa wa Kijiji." Wananchi waelimishwe kuhusu utaratibu huu ili waweze kutumia fursa hii kujiletea maendeleo ya haraka katika Vijiji vyao na kuondoa umaskini katika ngazi hii.

(iii) Mradi mwingine chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambao pia unatekelezwa, mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini ni *SELF*. Katika kipindi hiki mradi huu upo kwenye Mikoa kumi na nne tu. Kamati inashauri kuwa mradi huu uenezwe nchi nzima.

(iv) Kama ambavyo tumeona katika utoaji wa fedha katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais *NIGP* haikupewa fedha yoyote katika mwaka wa fedha 2004/2005. Katika shughuli nzima ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Taasisi hii ni muhimu sana katika uongezaji wa ajira na kipato kwa wananchi. Hivyo Serikali iipe kipaumbele Taasisi hii, hasa wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha mwaka 2004/2005 kumekuwepo uhusiano mzuri kati ya *NGO's* na Serikali na hivyo kuundwa kwa Baraza la *NGO's*. Kamati inaamini kuwa uhusiano huu ukiimarishwa Tanzania itapata mafanikio makubwa hasa katika kutekeleza MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masuala ya Muungano, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha ile Kamati Maalum ya Fedha chini ya usimamizi wa Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge imeundwa. Kamati inaitaka Serikali

kuhakikisha kuwa Kamati hii maalum inawezeshwa kisheria ili ifanye kazi ambayo ilikusudiwa hasa wakati huu ambapo yapo mabadiliko mengi yanayoendelea hapa nchini na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya mwaka wa Fedha 2005/2006 umeandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yanayotarajiwa kufikiwa katika utekelezaji wa mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini (MKUKUTA). Aidha, makadirio hayo yamezingatia pia maelekezo na mwongozo wa kutayarisha mpango kati wa mfumo wa bajeti *(Medium – Term Expenditure Framework Budget – MTEF)* kwa mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2007/2008 uliotolewa na Serikali Mwezi Januari, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais, itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa ratiba na kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Kitaifa na Kimataifa za Makamu wa Rais;

(ii) Kuratibu utoaji na ulipaji wa huduma zote muhimu kwa Makamu wa Rais na familia yake;

(iii) Kusimamia malipo ya ahadi za Makamu wa Rais katika kusaidia miradi ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 – Ofisi ya Makamu wa Rais, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kufanya mapitio ya Mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA na kuendeleza kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za mpango wa kuondoa maskini (*Poverty Monitory Master Plan);*

- Kutafsiri MKUKUTA kwa lugha rahisi/Kiingereza na Kiswahili na kuchapisha vijarida na vipeperushi;

- Kuendelea kujenga uwezo wa Idara katika kuratibu na kufuatilia jitihada za kupambana na umaskini;

- Kuendelea kutoa mafunzo kwa Watendaji wa Asasi za Fedha, hususan *SACCOS*, kadri ya mahitaji ili kuleta ufanisi zaidi na usimamizi mzuri wa mikopo;
- Kupanua shughuli za Mfuko wa *TASAF II* ili zienee nchi nzima; na

- Kuratibu jitihada za usambazaji taarifa mbalimbali uhamasishaji na uelimishaji umma ili kujenga ufahamu wa wananchi katika kuuchukia na kuupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya kazi zifuatazo:-

- Kuendelea na uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira;

- Kukamilisha mkakati wa mpango wa Taifa wa Bionuwai;

- Kuandaa taratibu, kanuni, miongozo ya utekelezaji wa Sheria ya Mazingira; na

- Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamzi wa Mazingira *(NEMC)* litaendelea kushiriki katika michakato ya Kitaifa, kuwianisha masuala ya mazingira katika MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masuala ya Muungano, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya kazi zifuatazo:-

- Kuandaa vijarida vya Muungano na kuvisambaza kwa wadau;

- Kufanya utafiti kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa msuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali; na

- Kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya Serikali kutokana na Mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGO's).* Kamati ilielezwa kuwa Kitengo cha *NGO's* kimepanga kutekeleza malengo yake kwa kuzingatia mpango mkakati *(strategic plan)* na Ofisi ya Makamu wa Rais kama ifuatavyo:-

- Kuweka mpango wa ushirikiano katika utendaji kazi kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la *NGO's;*

- Kutembelea, kuratibu na kutathmini shughuli za *NGO's* Mikoani; na

- Kutoa mafunzo ya kuongeza uwezo wa utendaji kazi kwa watumishi wa Kitengo cha *NGO's.*

Mheshimiwa Spika, kwa Sekta ya Utawala na Utumishi Kamati ilielezwa kuwa:-

- Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea na juhudi za kuwaendeleza Watumishi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na teknolojia;

- Suala la kudhibiti UKIMWI litaendelea kutiliwa mkazo; na

- Ofisi itaendeleza kazi ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam pamoja na Jengo la Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia na kuchambua kwa makini Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais, yafuatayo ni maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi wa kutoa mikopo midogo midogo *(Small Entrepreneurs Loan Facility – SELF)* umeweza kutoa mafunzo kwa Watendaji mbalimbali wa Asasi za Fedha, Kamati yangu inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais kusambaza mradi wa *SELF* nchi nzima. Wananchi wahamasishwe kuanzisha *SACCOS, SACCAS*, ili *SELF* itoa mtaji kwa taasisi hizo pale ambapo *NGO's* nyingine zinazojihusisha na utoaji na usimamizi wa mikopo hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria ya Mazingira imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais, Kamati yangu inaitaka Serikali kuendelea na utayarishaji wa kanuni kwa kushirikisha wadau mbalimbali na kutoa elimu kuhusu sheria hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* limepewa majukumu makubwa ya kusimamia na kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kupitia na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, pamoja na kuhakikisha ushirikishwaji wa jamii katika maamuzi yanayohusu usimamizi na hifadhi ya mazingira. Kamati inaiagiza Serikali kuhakikisha kuwa Bajeti inayopewa *NEMC* inalingana na uzito wa kazi iliyopewa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya kazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika masuala ya Muungano kwa mwaka huu wa 2005/2006 ni kuandaa vijarida vya Muungano na kuvisambaza kwa wadau. Kamati yangu inapendekeza kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais wafanye Semina, Mikutano ya kuelimisha wananchi umuhimu wa Muungano pamoja na kuwaelezea jinsi wanavyotatua kero mbalimbali na kutaka maoni yao katika kuboresha Muungano. *(Makofi)*

Mheeshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea na kujionea ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam. Kamati inasisitiza kuwa ujenzi wa Ofisi hiyo umalizike kufuatana na ratiba ya kukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa usajili wa *NGO's* umeanza kufanyika katika Mikoa yote Tanzania, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kusimamia Baraza la Taifa la *NGO's* ili likamilishe haraka kanuni za maadili ya *NGO's.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeelezwa kuwa eneo lingine la Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais limepatikana huko Zanzibar. Tunashauri kuwa

taratibu za makabidhiano ya eneo hilo ziharakishwe baina ya Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania, ili ujenzi huo uanze haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inapongeza mafanikio ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa *TASAF*. Kwa kuwa awamu ya pili ya *TASAF* imaenza Julai, mwaka huu 2005, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Wilaya ambazo hazijafaidika na awamu ya kwanza ya mradi wa *TASAF*. Serikali ihakikishe kasoro za awamu ya kwanza zinaondolewa na kwamba wananchi waelezwe vizuri kuhusu utaratibu wa awamu ya pili hususan kuhusu mfuko wa Taifa wa Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya MKUKUTA ielezwe vizuri kwa wananchi ili kila mwananchi aione nafasi yake katika kutekeleza MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina Kamati inakubaliana na Mpango wa Maendeleo pamoja na Makadirio ya Bajeti ya Makamu wa Rais – Fungu 26 na Ofisi ya Makamu wa Rais – Fungu 31. Hivyo Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na likubali kupitisha fedha zinazoombwa, Fungu 26 – Tshs.1,796,826,800/= kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Fungu 31 - Tshs.29,933,555,500/= kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii. Kwa niaba ya Wanakamati wenzangu ninapenda kuwashukuru Mheshimiwa Arcado Ntagazwa - Mbunge na Waziri wa Nchi, Mazingira na Muungano na Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo - Mbunge na Waziri wa Nchi, Kuondoa Umaskini na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Katibu Mkuu Mwandamizi - Bwana Raphael Mollel, Katibu Mkuu - Bibi Mary Moshi na wataalam na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais ambao wamefanya kazi nzuri na Kamati hii kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kuiongoza Kamati hii. Michango yao wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii pia kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge - Ndugu Damian Foka na Makatibu wake Wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Frank Mbumi na Michael Kadebe kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu Shughuli zote za Kamati. Pia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuhudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii. Kwa namna ya pekee tunamshukuru sana Ndugu Sam A. Manamba aliyekuwa Katibu wa Kamati hii hadi kustaafu kwake mwezi wa Aprili, 2005. Tunamtakia afya na mafanikio mema katika maisha hayo ya ustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuikubali hoja, nawashukuru pia Wapigakura wangu wa Jimbo la Magomeni kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha taarifa hii na ninaamini wataifanya kazi hiyo ili niwasilishe taarifa kwenye Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB (k.n.y. MHE. ALI SAID JUMA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI - OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA NA KUONDOA UMASKINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Ali Said Juma, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii, ningependa kuwasilisha maoni yake kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 43(5)(b)(c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Kamati nzima ya Uongozi ya Kambi hiyo kwa juhudi na kazi wanazozifanya ili tushiriki vizuri hapa Bungeni. Pia, nawapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Maokola-Majogo na wataalam wao kwa kuleta hapa Bungeni bajeti yao ya kuliomba Bunge kutoa idhini ya kupata TShs.29,933,550,500/= kwa nia ya kutekeleza na kusimamia mipango iliyopangwa chini ya Ofisi hii kwa kipindi cha fedha mwaka 2005/2006.

Aidha, napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini kwa ujasiri mkubwa anaouonyesha katika kuiongoza Kamati hii. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya mazingira ni pana sana, sio kupanda miti tu, kusafisha mitaro na kuondoa takataka, bali inagusa sana kilimo, uvuvi, hifadhi ya misitu, ufugaji, matumizi ya ardhi, madawa ya kilimo, uzalishaji wa mifugo, usalama wa hewa tuivutayo na kadhalika. Dhana ya mazingira ili kuwa na manufaa na mafanikio kwa wananchi wote, kufahamu takwimu na taarifa baina ya kada mbalimbali kwenye kaya, jamii na hata nchi, ni muhimu sana. Hivyo, ufahamu wa nini kinafanyika na kwanini kinafanyika kabla ya kutafuta suluhisho la matumizi endelevu ya mazingira ndio njia ya pekee ya kutumia kwa makini raslimali yetu ndogo tuliyonayo.

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja uondoke. Soma ya mwisho. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB (k.n.y. MHE. ALI SAID JUMA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI - OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA NA KUONDOA UMASKINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikija sasa katika suala la kuondoa umaskini, katika hali ya kawaida kwa nchi yetu ya Tanzania ambayo zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wake wanapata riziki zao za kila siku kupitia kwenye mazao yao ya kilimo. Hivyo basi, mtu yeyote anayetaka kwa dhati kuondoa umaskini, suala la kuinua na kuleta mapinduzi katika kilimo toka cha asili na kuwa cha kisasa ni jambo la muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusemapo kilimo cha kisasa ni vyema tukaweka mkazo mkubwa katika suala la umwagiliaji maji. Tunaelewa kuwa *National Irrigation Master Plan* iliyotayarishwa na Serikali kwa kushirikiana na *JICA* mwaka 2001/2002 inaonesha

kuwa hekta milioni 29.4 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Lakini kati ya hizo hekta 227,886 tu ndizo zinazotumika kwa umwagiliaji kwa sasa. Hii ni sehemu ndogo ya jumla ya eneo hilo na hivyo Serikali lazima iongeze nguvu hata kama ni kuwahamasisha wawekezaji kwenye kilimo waingie ubia na wananchi kwa maeneo hayo, maeneo yapimwe, yawe na hatimiliki na miundombinu ya kuruhusu wawekezaji kwenye kilimo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu zilizotolewa na *National Irrigation Master Plan* inaonyesha kuwa kama zikilimwa hekari 405,000 tu chini ya kilimo cha umwagiliaji zinaweza kuifanya nchi yetu ijitosheleze kwa mchele kwa ngazi ya Taifa na ziada kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uhubiri kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo kwa maendeleo ya Taifa letu uwe na thamani. Serikali lazima iwe na utashi wa kweli kwa kukifanya kilimo kuwa na manufaa kwa wakulima wenyewe na kwa uchumi wa Taifa. Tunaamini kuwa eneo hili likishapewa kipaumbele mambo mengine yanayozuka hivi sasa kama vile MKUKUTA na MKURABITA yasingekuwa na haja ya kubuniwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na wananchi wengi tunaona mpango huu wa MKUKUTA unaweza kuwa kama mchezo wa kuigiza iwapo hautatilia mkazo teknolojia ya kisasa katika uzalishaji na hasa kuongeza uzalishaji mashambani. Kama mpango wenyewe ni wa kuondoa umaskini tunadhani ingekuwa bora kama sehemu kubwa ya mpango huo ingetengwa kama mtaji wa uanzishwaji wa Benki ya Kilimo kitu ambacho kitaifanya Sekta nzima ya Kilimo kuwa hai na uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo katika maeneo mbalimbali hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu, tulitegemea kuwa uanzishwaji wa viwanda vya samaki mwambao mwa bahari yetu ungesaidia kuwapatia wananchi waishio maeneo hayo kuwa na ajira ya kudumu na hivyo kuongeza mzunguko wa fedha katika jamii nzima ziishizo Mwambao. Mbona viwanda vya aina hiyo vimesaidia sana Kanda ya Ziwa. Tatizo lingine la wazi ni Serikali inaposhindwa kwa makusudi kulinda soko la ndani, kutoa ruzuku kwa wakulima na kuimarisha viwanda vya ndani. Aidha, kuruhusu ubinafsishaji wa viwanda badala ya kuviachia kufanya kazi na kutoa huduma na badala yake vinabadilika na kuwa maghala ya bidhaa toka nje ya nchi. Hii ni hatari kwa nchi na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kama itapata ridhaa ya Watanzania na inaomba Watanzania iwape kura zao, itarekebisha mapungufu ya wazi yaliyomo kwenye MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, sura ya saba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mchango na mgawanyo wa mapato ya Jamhuri ya Muungano inasema hivi, nanukuu "Serikali ya Jamhuri itatunza akaunti maalum itakayoitwa akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya pamoja kwa mujibu wa sheria iliyotungwa

na Bunge kwa madhumuni ya shughuli za Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano."

Kambi ya Upinzani, kwa mujibu wa kifungu hiki inamwomba Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mambo ya Muungano atupe maelezo, yaani Serikali zipi zinatakiwa zichangie Mfuko huu wa pamoja wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano? Sisi tunaona kuna Serikali mbili zinazotakiwa kuchangia kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati alipokuwa akifanya majumuisho ya Wizara yake Waziri wa Fedha alisema kuwa asilimia 4.5 ya misaada hupewa Zanzibar na wapo watu wanaonung'unika kwamba kiwango hicho ni kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Ma-Rais wetu walipoungana walielewa wazi kuwa Bara ni kubwa katika kila hali na Zanzibar ni ndogo katika kila hali. Hivyo hivyo, Luxembourg ni ndogo katika kila hali kulinganisha na Ufaransa na nchi nyingine za Ulaya. Lakini ina haki sawa na nchi hizo bila kujali udogo wake au ukubwa wa wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, udogo wa nchi hautoi sababu ya kuinyima nchi haki yake ya msingi. Hapa ni kuangalia *spirit* ya Muungano, tukianza kuzungumzia udogo na ukubwa Rwanda na Burundi wataogopa kuungana na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuona umuhimu wa umoja, lakini hata Bunge lako Tukufu limekataa kuanza kuunganisha nchi za Afrika Mashariki kisiasa. Hivyo, ni dhahiri kuwa nchi zinapoungana inatakiwa maslahi ya kila mmoja yalindwe na hapa yote yametokea kwa sababu Tume ya Pamoja ya Fedha imechelewa kuundwa. Hivyo, hata ile 4.5 inayolalamikiwa haina usahihi wowote kwani haijibu masuala yote ya mapato na matumizi ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, tunangoja maelezo ya Tume ya Mheshimiwa Shellukindo ili tupate ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi hii ya Makamu wa Rais imeomba TShs.29,333,555,500/=. Mimi kwa niaba ya Kambi ya Upinzani sina utata nazo naomba Bunge liidhinishe wapewe kwa matumaini kwamba watafanya kazi kwa mashirikiano ya pamoja Wizara mbili hizi kurekebisha kasoro zote nilizozitoa katika hotuba hii, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge ninao wachangiaji hapa wako nane na sina uhakika kama watakwisha. Lakini tumepanga vile vile kama tunavyofanya siku zote, wachangiaji ambao wamechangia mara moja tu ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ambaye ataanza kuchangia atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor

Juma Khamis. Halafu waliochangia mara mbili tu ni Mheshimiwa Jenista Mhagama naye atafuatiwa na Mheshimiwa Leonard Shango na Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi.

Waliochangia mara tatu, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. Hao kama nafasi itakuwepo wote watakuwa wamemalizika. Sasa namwita Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie katika hotuba hii ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani sasa hivi, mimi labda nianze kwa kuunga mkono hii hoja. Nimekuwa nikisikia hapa kuna baadhi ya watu wanaitwa Askari wa Miavuli. Ni kweli Askari wa Miavuli ni Askari hodari sana lakini mimi nawaona Askari wa Miguu ni hodari zaidi kwa sababu wanakabiliana na adui uso kwa uso. Hawa kaka zangu wawili kwa kipindi hiki walioongoza Ofisi hii wamekuwa Askari wa Miguu shupavu sana. *(Makofi)*

Mimi nasema kazi walizozifanya ni kubwa, hakuna Mtanzania ambaye hakuona manufaa yaliyoletwa na *TASAF* na *TASAF* imefanya kazi bila ya kuona inafanya kazi wapi, huyu ni nani na huyu ni nani ili iwatumikie wananchi. Napenda nichukue fursa hii kushukuru sana Mfuko huu ambao katika Jimbo langu umechangia Shilingi milioni 48 kusambaza maji kutoka sehemu ya Fundo kwenda Uvinje na naamini hapo mbele kwa sababu awamu nyingine imeanza, tutapata msaada zaidi ili tumalize kazi iliyopo ya kusambaza maji katika Jimbo la Gando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na fikra kidogo kwamba kutaja mambo ya Muungano ni kitu labda Waingereza wanasema *very delicate,* yaani kwa nini unagusa hicho kitu?! Hapana! Lazima tuguse kwa sababu Muungano si *delicated issue* ni *national issue*. Sisi kama Watanzania tunapaswa kusema pale ambapo tunahisi ama mtu mmoja au kikundi fulani cha watu kinapohisi kuwa eneo hili mbona kuna tatizo. Ni vizuri tuseme basi ili watu wanaohusika waweze kuleta marekebisho kwa ajili ya kuimarisha Muungano wetu.

Mimi nasema katika hatua hii na katika wakati huu ambao tunao kuna mtu anafikiria labda kuna mwingine hapendi Muungano au hautaki kufikiria hivyo basi ni uhaini kwa sababu Muungano huwezi kuuvunja tena kwa hatua uliofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhana hii ya kuondoa umaskini ambayo imekuwa inatoka katika kila kinywa cha Mtanzania. Lakini mimi nina mashaka na utekelezaji wa hii dhana yenyewe. Tunawaona vijana wanaojituma kujihangaisha acha tuwape jina tutakalo, wengine wanawaita Machinga, wengine wanawaita jina lolote. Mimi niseme ni vijana wanaotafuta riziki. Inawezekana mara nyingine labda wanavunja sheria au taratibu kwa kukaa mahali wasiporuhusiwa, lakini namna tunavyokabiliana nao mimi nahisi hatutumii uungwana. Vijana hawa mali nyingine ni zao, mali nyingine wanakopa, wanakwenda kwa Askari sijui ni wa Baraza la Mji au Askari gani wanawavamia,

wanawapiga, wanawachukulia bidhaa zao wanawaharibia; hivi kweli tunawasaidia kuondoa umaskini au tunawaumiza?

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingine hata mantiki huioni kwa sababu unapomwondoa mtu mahali anapopata soko ukienda ukam-*damp* katika eneo ambalo hata watu hawaendi hakuelewi. Anakuona unamharibia maisha yake na anakuona wewe ni adui tu. Kwa vile mimi ningeomba Serikali katika hili wawe waangalifu sana katika kuwahamishia watu au vijana kwenye maeneo ambayo hawataweza kufanya biashara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea tumeambiwa hapa kuhusu Tume ya Haki ya Binadamu. Inawezekana mimi niko nyuma kidogo katika kuelewa habari za karibuni sana. Lakini sina hakika sana kuwa hii Tume ya Haki za Binadamu ya Jamhuri ya Muungano inafanya kazi moja kwa moja Zanzibar kwa sababu nilisikia wakisema kuwa lazima iundwe sheria na ikiwezekana iundwe Tume yenyewe huko Zanzibar. Sasa ni vizuri Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake atueleze kulikoni juu ya jambo hili. Ni kweli hii Tume yetu ya Jamhuri ya Muungano inafanya kazi moja kwa moja au hilo suala la kutungiwa sheria kule kwetu lazima lifanyike kwanza. Huu ni utata ambao ninao naomba atusaidie.

Tatu, katika suala la muhimu la nchi ni Usalama wa Taifa. Mimi nisiseme Usalama wa Taifa kwa maana ya Askari wa Usalama tu, lakini nauchukua Usalama wa Taifa *as a broad issue* ambayo inahusisha vikosi na mambo mengine mengi. Hapo mimi utata wangu ni wa Kikatiba kwa sababu unapotoa fursa kwa baadhi ya vitu vinaweza vikatumika vibaya, watu wanaotekeleza sasa hivi pengine wana nia nzuri, lakini huwezi kujua baadaye ulimwengu utakuwaje.

Kule kwetu kuna vikosi vya *KMKM, KVZ, JKU* na vingine. Mara nyingine vikosi hivi vinafanya kazi ya Askari Polisi. Sasa inapotokea hiyo watu wanaanza kujiuliza; Je, Polisi wameshindwa, wamekasimiwa madaraka na kama wamekasimiwa, wamekasimiwa na nani kwa sababu mwenye mamlaka ya usalama wa nchi ni Amiri Jeshi Mkuu. Je, kama amekasimu, ni *formal, informal* au vipi? Ni vitu ambavyo wanavizungumza watu, ni vizuri vikatolewa ufafanuzi ili hizi nong'onong'o zikamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Tume za Uchaguzi. Katika nchi yetu Tume mbili za Uchaguzi, Tume ya *NEC* na Tume ya *ZEC* ambazo sio tu ni Tume mbalimbali, lakini hata sheria ni mbalimbali. Kwa kadri ninavyoangalia mimi katika masuala ya uchaguzi, hii moja inakuwa *agent* ya nyingine. Hii *ZEC* inafanya kazi ya *NEC* mara nyingine. Sasa kama inapotokea hivyo; je, wanapaswa kutumia sheria gani? Ni vizuri tukaelezwa kwa sababu hayo ni mambo ambayo watu wanayauliza. Mimi sisemi kuwa wasifanye kazi, wafanye kazi na wanafanya kazi nzuri mara nyingine, lakini kisheria wanapaswa kutumia sheria gani? Kama wanafanya kazi ya *NEC;* je, *NEC* tayari wameshafanya *screening* hata ya majina? Mbona *ZEC* hawajafanya? Tunasemaje kwa hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la misaada, limezungumzwa sasa hivi hapa. Hapa pana tatizo kidogo. Mimi naona pana tatizo kidogo la ufahamu labda. Ni vizuri tukasaidiwa ili sisi wengine tukaelewa na walioko nje nyumba hii wakaelewa. Waziri amesema hapa kuwa kuna gawio hili la asilimia 4.5 ya misaada na mikopo na amechanganya na faida ya Benki Kuu. Sasa sijui kama na hili la pili la faida ya Benki Kuu pia linaingia hapa. Kama linaingia hapa, basi mimi nafikiri gawio kidogo ni tofauti na ilivyosemwa jana kwa sababu Benki Kuu imeundwa kutokana na Muungano wa nchi mbili na kwa maana hiyo ukigawa moja ukampa 4.5 kwa sababu tu unasema asilimia ya watu wake ni ndogo bila ya kuangalia, kwa hiyo, ni nchi yenyewe ndiyo inabidi iunde Tume za Mheshimiwa Shellukindo, kesho itakuja Tume ya Mheshimiwa Majogo, keshokutwa ya nani, manung'uniko yataendelea kuwapo.

Watu wanasema kuwa suala la asilimia 4.5 ni dogo kwa sababu *is almost* unatoa haki ya Mkoa mmoja tu katika Mikoa 25 ya Tanzania. *Logic* yake sisi wengine tunaifahamu, hivyo kuwa tunapewa haki ya Mkoa. Sasa kama ni Mkoa, basi tuambiwe maana yake watoto wa Mjini wanasema isijekuwa tunauziwa mbuzi kwenye gunia. Katika ulimwengu wa leo ni vizuri tukaelezana vizuri kwa sababu ni tatizo hili. Pia, namwomba Mheshimiwa Waziri kama anasema hii 4.5 pia ni gawio la Benki Kuu, basi atuambie atakapo-*sum-up* angalau katika kipindi hiki cha miaka miwili kwa hii 4.5 Zanzibar imepata gawio kiasi gani la faida ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la mazingira, nchi yetu hapa wanahitaji au Serikali zinahitaji kujitutumua kidogo katika hili. Inawezekana ndani tunaweza kudhibiti labda ndani ya nchi kavu lakini bado tuna matatizo baharini. Kule Pemba mwaka 2003 kulitokea balaa la maradhi katika Jimbo la Micheweni na *samples* zilichukuliwa zikaletwa Wizara ya Afya Dar es Salaam. Mimi nilikuwa miongoni mwa watu waliotumwa kwenda Wizara ya Afya kufuatilia kulikoni. Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya alisema kwa taarifa alizonazo yeye ni kuwa katika eneo lile vyakula vinavyotumiwa na watu vilikuwa na madini ambayo hayatakiwi yaweko ndani ya mwili wa binadamu na hiyo ilionekana ndani ya vyakula vilivyoko pale.

Sasa mimi nina wasiwasi isije ikawa labda zinapita meli zinamwaga vitu ambavyo sumu zake zinasambaa. Sasa mimi ningeomba tu-*invest* kidogo katika hili Serikali ijaribu kufanya doria za makusudi kabisa katika bahari ili kuona ni nani, ni meli gani au ni vyombo gani vinavyoingia hata meli za uvuvi tu. Kuna meli chungu nzima zinavua. Ukiangalia tunachopata ni kidogo na wale wanaweza kuvua kwa sababu hawachunguzwi. Sasa ni vizuri kwa hili basi wakaangalia kwa sababu hiyo kuvua ni sawa wanapata fedha wao na sisi tunakosa samaki, lakini wakitumwagia sumu tunakosa na roho pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu mimi nimeona kitu Pemba wanaita *a flot* hizi ni boti eti ni hoteli. Wazungu wajanja sana eti ni hoteli ziko baharini zinaelea. Watu wanakwenda wanalipa wanakaa humo wanafanya *diving* hizo meli zipo karibu mwaka wa kumi pale kwetu lakini huoni Maafisa kwenda kuchunguza wala hujui kuwa zinakuwa meli wakati wa mchana tu usiku pengine zinageuka vitu vingine, watu wanafanya vitu vya ajabu ajabu. Sasa mimi ningeomba katika suala hili Serikali ijaribu kuangalia kwa

kina kikubwa ili tusije tukapata matatizo ambayo yanaweza yakatufikisha nchi yetu katika mahali ambapo watu wetu wataumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzoni, mimi sina tatizo na hotuba hii. Ninawapongeza sana kaka zangu wawili hawa kwa kazi wanayoifanya na wajitahidi kwa sababu malalamiko mengine mimi nina hakika yako nje ya mikono yao lakini na wao wanapozungumza na walio na mamlaka wawaambie kuwa watu wanalalamikia haya, hebu kaeni myamalize ili hizi tofauti ndogo ndogo tusiziachie kumeya katika nchi ambayo tunaamini juu ya umoja tunaamini juu ya udugu na tunaamini juu ya ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ZAHORO JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri kwa hotuba aliyoiwasilisha Bungeni asubuhi hii ambayo ina mwelekeo wa kusaidia kuimarisha umoja wa Taifa na maendeleo ya Taifa. Pia, niipongeze Kamati ambayo imechambua hotuba hii iliyowasilishwa mbele yetu asubuhi hii na pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitangulie kusema kwamba naunga mkono hotuba hii. Pamoja na hayo, kuna maeneo ambayo nakusudia kuyazungumzia pengine labda kusaidia kuweka sawa baadhi ya maeneo ambayo nahisi yana mapungufu madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 5 – 12, ambapo anazungumzia masuala ya Muungano, ametaja mambo mengi tu na niseme nampongeza pamoja na kwamba mambo haya vile vile yamejumuisha mambo mengi, ni mtiririko wa muda mrefu ambao umekuwa ukiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku ya tarehe 25 Aprili, 1977, Baba wa Taifa alitoa hotuba na katika hotuba hiyo natumaini alikuwa analihutubia Bunge na sehemu ya hotuba yake alisema hivi, naomba kunukuu: "Kwa wote hao napenda kusema hivi, nchi kama yetu ni sawa na kijana mwenye afya na ambaye bado anakua. Katiba ya nchi ni sawa na vazi lake, vazi tulilomshonea mtoto Tanzania miaka 13 iliyopita, sasa linabana. Tunaamini kwamba vazi hili tunalolileta litamtosha kijana Tanzania endapo baada ya miaka mingine mingi au michache vazi hili nalo litabana. Sina shaka kwamba wenzetu watakaofuata au sisi hawa hawa tutampima tena na kumshonea vazi lingine." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tunalolizungumzia hapa au ufafanuzi wa hotuba hii. Leo hii ndiyo zile tunazoziita kero za Muungano. Sasa maelekezo ya wakati huo ni kwamba kila vazi hilo litakapombana maana yake juhudi za kufanyika ni kumshonea vazi lingine. Sasa tatizo tulilonalo hii leo, tumekuwa tuko taratibu sana katika kubadilisha hilo vazi ambalo lina mstahiki kijana wa Tanzania kwa wakati huu wa leo. Mfano wa hayo, kulikuwa na *white paper*, nadhani miaka mitano zaidi ya nyuma, sikumbuki ilikuwa ni

mwaka gani. Katiba ilirekebishwa mara ya kwanza na mara ya pili imerekebishwa hivi karibuni.

Lakini Serikali imetamka italeta hatua kwa hatua mabadiliko hayo. Sasa suala lililopo, hivi wananchi tuliwauliza kwamba ridhaa yao mabadiliko yale kwenda hatua kwa hatua au ni uamuzi wa Serikali? Wananchi walieleza matatizo ya wakati ule si ajabu ukiipitia tena *white paper* ile ile kwa sasa hivi, kuna maeneo ambayo yamepitwa na wakati. Kwa hiyo, ni vyema kila jambo lije kwa wakati wake.

Wazungu wana utaratibu katika chakula, wanapoita *lunch* inakwenda na wakati, wakisema *breakfast* maana yake inakwenda na wakati, huwezi ukajikusanyia vyakula vya asubuhi jioni ukasema ile ni *breakfast*. Sasa wananchi walieleza tatizo la wakati huo, kwa hiyo, ni vyema nayo tukaona kwamba kila kitu tunakileta kulingana na wakati unaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo, nadhani ndiyo tulikwenda mpaka tukafikia hatua ya ile 4.5 ikiwa kama ni ufumbuzi wa muda.  Tumeunda Tume ya Shellukindo, hivi karibuni kuna *report* nyingine. Mimi sitaki kwenda kuleta mjadala kwenye 4.5, kwa sababu kwanza ninachoamini ule ulikuwa ni ushauri, kwa hiyo, sio kitu ambacho kilikuwa kiko kisayansi. Kwa hiyo, mimi nikisema vinginevyo pia itakuwa hoja siyo ya kisayansi.

Lakini ninachoamini ni kwamba lazima tufike pahali tuzungumze kitu ambacho kiko kisayansi. Iwe na sababu kwanini. Mimi sitashangaa hata kama tutafika mahali tutazungumza 2.1, lakini iwe na hoja ya msingi ambayo Watanzania wataielewa. Leo hii ukiulizia hii unaambiwa tulizungumza tulikubaliana, lakini kwa misingi ipi huwezi ukapata jawabu la uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeunda Tume nyingi hivi karibuni, tumeambiwa kuna *report* ambayo Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini sasa hizi Kamati, *report* zimeshakuwa nyingi, lazima tufike mahali sasa tuone matokeo ya hayo. Kwa hiyo, ningeliomba Mheshimiwa Waziri Wizara yako inahusika na kutoa msukumo kwenye hilo, kwa hiyo, tunategemea msukumo huo uonekane kwa maslahi ya Taifa hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Kamati inayohusika na Wizara hii naamini ina mchango muhimu sana wa kulisaidia Taifa hili la Tanzania kuliunganisha kwa karibu zaidi. Kamati hiyo iliyoundwa na Kanuni hii ya Bunge Toleo la 2004 na imetajwa katika Ibara 101, naomba kunukuu sehemu ndogo ya Ibara hiyo, inasema hivi:

“Kamati ya Maliasili na Mazingira itakuwa na Wajumbe watakaoteuliwa na Spika na itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:- Ofisi ya Makamu wa Rais ikawekwa kwenye mabano (Mazingira na Kuondoa Umaskini), mbili ni Wizara ya  Mali asili na Utalii.”

Sasa hiyo Kamati inaitwa Maliasili na Mazingira na kosa moja ambalo limefanywa na hii Kanuni, Ofisi ya Makamu wa Rais ikawekwa kwenye mabano Mazingira na kuondoa umaskini. Mimi ninavyoamini hilo ni kosa na ninasema ni kosa kwa sababu maelekezo yangu najielekeza katika Ibara ya 47, ibara ndogo ya (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo nayo nitaomba kuinukuu inasema hivi:

"Kutakuwa na Makamu wa Rais ambaye atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano kwa jumla.

(a) Atamsaidia Rais katika kufuatilia utekelezaji wa siku hata siku za mambo ya Muungano;

(b) Atafanya kazi zote atakazoagizwa na Rais;

(c) Atafanya kazi za Rais kama Rais hayupo." Mwisho wa kunukuu.

Katiba haikutaja mazingira, haikutaja umaskini. Kamati imetaja mazingira umaskini, ile sababu ya msingi ya kuwepo Ofisi hiyo imewekwa kando. Sasa hilo ni tatizo na nadhani hata pengine ndiyo inashindwa labda kukusaidia kikamilifu Mheshimiwa Waziri kwa sababu ukiangalia hasa kama kwa maana ya hii Kanuni Kamati hii jukumu la Muungano si lake, halikutajwa humu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani Bunge lingejitazama, likajipanga vizuri. Kwa sababu Bunge tunaita Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wapi ile nafasi ya Muungano ilipopachikwa? Maana yake inaelea. Sasa si vizuri Bunge tukalifikisha mahali pabaya kama hapa tulipolifikisha. Nadhani hapa kidogo tumeteleza, nadhani ni vizuri tukafanya masahihisho kwenye Kanuni zetu ili twende sambamba na huu mwelekeo wa kudumisha Taifa linaloitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi hii ya Makamu wa Rais kwa bahati mbaya sana tokea imeanzishwa mpaka hii leo kule Zanzibar haina Ofisi, iko nyumba tu ya Makamu wa Rais, lakini yeye Makamu wa Rais sina hakika shughuli zake huwa anafanyia wapi? Ndiyo pale pale nyumbani kwake au vipi. Lakini nina hakika Mheshimiwa Waziri akienda kama hakujiegemeza kwenye nyumba ya Makamu wa Rais, basi itabidi shughuli zake afanyie hotelini, hana Ofisi.

Wale Watendaji wake wamejibanisha mlemle ndani ya Ofisi na si Watendaji wake. Niweke sawa hapo kidogo. Ni wale wahudumu wa Makamu wa Rais wamejibanza mlemle ndani ya Ikulu ya Rais wa Zanzibar. Kwa maana hiyo, Ofisi hawana. Sasa na wale siiti Idara, *in fact*, kwa sababu ukiita Idara mimi nadhani utakuwa umeikuza tofauti na ilivyo, wale ni huduma za Makamu wa Rais, wajue Makamu wa Rais anakuja, atalala wapi? Atakula nini? Hizo ndiyo shughuli zao.

Sasa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja, Kikatiba imetajwa inashughulikiwa masuala ya Muungano, lakini Zanzibar haipo. Humu yamekutwa tu maandishi, itajengwa, itajengwa, nadhani karibu kuna kama milioni 800 zimeshatumika kuujenga ule ukuta, napo panaambiwa pame-*fail*. Mpaka sasa haina Ofisi.

Pia, ukiangalia katika makisio haya ya mwaka huu, hiyo Sekretarieti inayoitwa ya Muungano katika kitabu hiki, ukurasa wa 48, kiasi cha fedha kinachotengwa naona bado ile *seriousness* haijitokezi. Ukiondoa lile fungu lililotengwa kwa ajili ya Zanzibar, ukiondoa kifungu cha mishahara na zile posho, fedha zinazobakia, naanza mwaka juzi 2003/2004 kulikuwa kunabaki ya Sh.42,000,0155/= mwaka 2004/2005, Sh.18,000,599/= mwaka 2005/2006 zinabakia Sh.30,000, 499/=. Yaani ukishaondoa milioni 24 zile ukiondoa mshahara na posho za wafanyakazi, maana yake hizo ndizo zinazobakia kwa maana hiyo ya kufanya kazi. Kuelewa kujua mazingira mazima ya Tanzania na taratibu zake nyingine zinazohusika, fedha wanazotengewa ni fedha hizo. Hata ukiangalia hii Idara yenyewe nacho ni hivyo hivyo kiko dhaifu sana. Sasa hii ni Idara muhimu ya kusimamia uhai wa Taifa la Tanzania. Lakini iko dhaifu sana.

Sasa kwa hali hii nadhani kuna haja ya makusudi kabisa kuona ulazima wa kuipa uhai, kuipa wataalam na hii ni Idara ya Utafiti. Wafanye utafiti waelewe Mzingira mazima ya uhai wa Taifa la Tanzania. Waelewe tuna matatizo yapi, kipi cha kufanyika, kipi wakifuatalie, mtiririko mzima wa uhai wa Taifa hili. Hawa ni Ofisi ya kiungo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo lingefanyiwa kazi na ni vyema hata Mheshimiwa Waziri anayehusika na Ofisi hii awe na taratibu za kufanya ziara, pengine kuzitembelea hata zile Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar. Hivyo, hajafanya akaelewa miongoni mwa matatizo waliyonayo kwa sababu wanafika mahali ni sawa na kusema wanahudumia tuseme labda mabwana wawili kwa wakati mmoja. Wapo ndani ya Zanzibar, pana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini wao pia wakati huo huo ni watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, wanapata matatizo ambapo wanafika mahali penye kulemewa. Kwa hiyo, wanahitaji msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui hata hiyo *organization chart* ya Ofisi hii ya Makamu wa Rais ikoje kwa sababu kama Zanzibar hawana Ofisi, sijui kuna sehemu ambayo inajitokeza hiyo Ofisi ya Zanzibar wakati Ofisi hawana! Hilo nalo pia ningeomba lifanyieni kazi *at least* tuonekane kwamba tunakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo niombe kuishia hapo. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini naomba kwa heshima na taadhima niwapongeze sana hawa Mawaziri wawili wanaofanya kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na maneno ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliyechangia mada hii kama Msemaji wa kwanza kwamba kwa kweli wanaweza kuwa ni Askiri wa Miavuli lakini vile vile wanaweza kufananishwa na Askari wa Miguu kwa sababu wamesimamia Mifuko ambayo inaonekana imeleta matunda makubwa sana katika kuendeleza jamii ya Watanzania.

Kwa hiyo, nami naungana nao na kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa kweli tunaomba kuwapongeza sana. Lakini hasa tunampongeza Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwenye kushikilia Mfuko wa *TASAF* na tunaona kabisa Watanzania hawakufanya makosa kulipia ngoma na ngoma hiyo wao wenyewe wakachagua wimbo na wimbo ukawa ni wa maendeleo kwa maana ya kwamba kila anayelipia ngoma ndiye atakayechagua wimbo.

Kwa hiyo, kuchagua Chama cha Mapinduzi kumesaidia sana kuleta maendeleo ya nchi hii na hasa kwa usimamizi makini wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Mifuko hiyo iliyofanya kazi chini ya Ofisi ya Rais na Ofisi ya Makamu wa Rais kama tulivyoona imefanya kazi kubwa sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba kazi kubwa ya Mawaziri hawa kwa kipindi kilichopita na kipindi kijacho wameweza kushirikiana sana na Watendaji wao, Katibu Mkuu na timu ya Wataalam katika Mifuko mbalimbali. Naomba pia nao niwapongeze, lakini lengo kubwa lilikuwa ni kupambana na kupunguza umaskini, ajenda ya kupunguza umaskini ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza kupunguza umaskini sasa hivi mpango mzima wa MKUKUTA unajilenga katika kukuza kipato cha mwananchi lakini vile vile kuimarisha ama kuleta hali ya maendeleo ya maisha ya jamii na kuboresha zaidi suala zima la utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, upunguzaji wa umaskini unahitaji ukuaji endelevu wa pato la Taifa. Kama pato la Taifa litakuwa na ukuaji wake utakuwa endelevu, basi mimi naamini kabisa hali ya kipato kwa wananchi itaongezeka na hali ya uduni wa maisha ya jamii itapungua na hivyo basi tutakuwa tumeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupambana na umaskini ambao tunao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nasema kwamba suala hili la umaskini ni mduara uliojifunga na nilikuwa nazungumza hapa na wenzangu Mheshimiwa Mbunge, Mzee wetu John Malecela amenichekesha sana hapa anasema unapozungumzia mduara huo ni kama vile paka anakimbiza mkia wake, unamfanya paka ashike mkia wake ama panya akamate mkia wake. Sasa hapo ndiyo unapata picha jinsi gani kazi ya ziada inatakiwa ifanyike ili paka huyo aweze kukamata mkia wake yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezekano upo. Hapo inatakiwa lazima kuwe na mbinu mbadala za kumfanya paka huyo akamate huo mkia na mimi nafananisha huyo paka anayetaka kukamata mkia ni huyo mwananchi ambaye hana kipato ama maisha

yake ni duni na sasa unataka kumwondoa katika uduni huo ili aweze kuwa na nafasi nzuri ya maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba Wizara zote za kisekta zinatakiwa zifungamane kwa kiasi kikubwa kuhakikisha suala zima la ukuaji wa uchumi endelevu linafanikiwa na suala zima la kuondoa umaskini wa kipato na kuboresha hali ya maisha ya jamii linafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapo sasa ni suala la msingi la Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa kama ni *coordinator* wa mipango hiyo yote na kusimamia itakiwavyo na kuhakikisha kwamba paka huyo anakamata mkia wake kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa tuangalie kwamba tunahakikisha hao wananchi ambao wana maisha duni na wengi wao ni wale wanaoishi katika maeneo ya Vijijini wanafanya ama wanaboresha uzalishaji wao kutoka katika uduni na kuwa na uzalishaji wenye tija. Lakini watawezaje kufanya hayo? Ni lazima kuboresha mashamba yao madogo madogo, ni lazima kukuza biashara zao ndogondogo, ni lazima kuwapelekea zana bora za kilimo na zana bora za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni lazima kuendelea na mikakati iliyowekwa ya kuwafanya wananchi na wazalishaji hao wadogo wadogo waweze kupata pembejeo kwa ajili ya uzalishaji wao na ili iweze kuwa uzalishaji wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu ya masoko ni muhimu. Mikopo nafuu na yenye kufikika kwa urahisi kwa hao Wananchi wanaotaka kuboresha ama kupambana na umaskini wa kipato hilo ni suala la kuzingatia. Vinahitajika viwanda vidogo vidogo vya kuweza kuanza kubadili mazao yao na kuyafanya yawe ni mazao yenye tija ya kuweza kununulika na kuwa na mkakati ambao unatakiwa usimamiwe ili kuweza kusaidia. Lakini vile vile usafirishaji rahisi, hata kama barabara zile zinaweza tu kusafirisha mazao kwa kutumia mikokoteni, inaweza kusaidia Wananchi hao na kubadilishia maisha yao ya kila siku. Kuna umuhimu wa kuhifadhi mazingira na uboreshaji wa tekinolojia kutoka tekinolojia zinazoharibu mazingira kwenda tekinolojia zitakazorahisisha shughuli mbali mbali ambazo pia zitaboresha mazingira yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia mambo haya yote, yanaweza kuwa ni wajibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa sababu ndiye aliyevaa koti la kupambana na umaskini, lakini utakuta kwamba, kuna wajibu mwingine wa Wizara Kisekta ili kuhakikisha masuala haya yanaweza kufanikiwa. Kwa hiyo, tunaamini kabisa, Bajeti hii tunapoipitisha, wenzetu Askari hawa wawili, wana kazi kubwa ya kuona wanatengeneza sasa mipango gani ya kumsaidia huyo Paka kukamata mkia, kwa maana ya kuwasaidia maskini kupata kipato na kuondokana na hali duni ya maisha yao kwa kufuata haya ambayo nimeyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini matokeo ya mambo haya kama yatafanyika, ina maana basi, umaskini huo wa mahitaji ya jamii utakuwa umeondoka. Wananchi watapata mahitaji yao kwa kadri wanavyohitaji, lakini chakula bora kitaboreka, Wananchi watapata chakula cha kutosha na hivyo utaoana kwamba, hata ajira zinaweza kujitengeneza kwa kiasi kikubwa na hivyo tukawa na jamii endelevu katika maendeleo. Lakini pia tukaendelea kuwa na ukuaji endelevu wa uchumi na Pato la Taifa la Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapozungumza hayo, ninaipongeza sana Ofisi ya Makamu wa Rais. Ninafikiri Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kugundua kuwa mpango mzima wa kupambana na umaskini, ndiyo maana kwa makusudi, ilianzisha Mifuko hiyo ya *SELF, TASAF* na *NIGP,* kwa ajili ya malengo hayo ambayo nimeyataja awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana *TASAF,* kule kwetu wamefika na wamefanya kazi kubwa. Ninawapongeza *SELF*, kwa kweli sisi Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, wamekuwa ni wa kwanza kupata matunda ya *SELF.* Lakini sasa tunawaomba waungane na Vijana pia, waungane na *SACCOS* nyingine ambazo ziko katika maeneo hayo ili kuweza kusaidia kupeleka hayo matunda moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninasema kwamba, tuone sasa Mifuko hii ina majukumu mazito na ina kazi kubwa sana ya kuweza kuboresha hali ya kipato ya Wananchi na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia ripoti ya Mheshimiwa Waziri, nimeangalia Mfuko wa *TASAF.* Katika miradi yote ambayo imefanyika katika mwaka huu unaoishia 2005, miradi inayohusu miundombinu ya kiuchumi ni 12 tu. Miradi inayohusu miundombinu ya umwagiliaji ni saba tu kati ya miradi karibu 1,389 iliyofanyiwa kazi. Kwa hiyo, miundombinu ya kiuchumi na miundombinu ya umwagiliaji, imekuwa ni miradi michache sana kwenye Mfuko huo wa *TASAF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunakubaliana kwamba, ili umaskini uweze kuondoka, tunahitaji kuwa na ukuaji endelevu wa Pato la Taifa na tunaamini kabisa kwamba, kilimo ndicho kinachochangia kiasi kikubwa sana cha Pato la Taifa, nadhani pamoja na mipango mizuri iliyokwisha kufanywa na inayoendelea kufanywa, lakini Mfuko huu wa *TASAF* sasa uangalie namna gani utaweza kuboresha miundombinu hiyo midogo ya kiuchumi, lakini pia Mfuko huu uchangie sasa hasa katika miundombinu ya umwagiliaji katika yale mashamba madogo madogo kule Vijijini na hivyo basi yataweza kuchangia kiasi kikubwa sana ongezeko la Pato la Taifa, yataweza kuchangia sana kupunguza umaskini wa kipato, yataboresha hali ya jamii na yataboresha lishe na chakula katika jamii yetu na hivyo wale watu maskini na hasa wanaokaa vijijini wasioweza kufikika, wataweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona Mfuko wa *NIGP* umetengewa fedha za ndani kama shilingi milioni mia mbili na kitu, lakini nilikuwa nafikiri kwamba, kwa kuwa ukiwa nacho wewe mwenyewe unaweza kupanga na kufanya mambo mengi sana,

ninaomba Serikali iongeze fedha katika Mfuko huu na Mfuko huu pia ushirikiane na Mifuko mingine, kuboresha yale mambo 10 ambayo nimeyataja hapo awali. Kama tumeweza kutumia Mifuko hii, tukaona kwamba inaweza kuanzisha hivyo viwanda vidogo vidogo kwa kushirikiana na *SIDO*, labda kwa kushirikiana na Mfuko wa viwanda vidogo vidogo tunaweza tukajikuta kwamba, tumewasaidia Wananchi wengi sana maskini katika harakati zao na mipango yao wanayoifanya ili kuweza kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunao Mfuko wa *SELF,* kama nilivyosema hapo awali kwamba, bado tunahitaji mitaji ambayo inaweza kuwafikia Wananchi katika maeneo ambayo Mabenki hayafiki, ama masharti mengine ya mikopo ni magumu na hayawezekaniki. Tunawapongeza *SELF* wameanza vizuri, lakini tunaendelea kuwaomba waongeze bidii. Kwa kweli wazisaidie sana *SACCOS* za Wananchi zinazoanzishwa ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *SACCOS* nyingi zinaanzishwa hazina mitaji, hazina wataalam wa kuziendesha na kama tulivyoelezwa katika Bajeti, Mfuko wa *SELF* una lengo la kusaidia kutoa mafunzo, kutoa mitaji midogo midogo na una lengo la kusaidia kusimamia shughuli hizo za Benki ndogo ndogo za Wananchi. Kwa hiyo, naupongeza lakini ninaomba uende kwa *speed* hasa uangalie mazingira ya Wananchi kule vijijini na usibakie tu katika maeneo ya mijini, ambako *SACCOS* nyingi sana zimejiweka katika maeneo hayo ya vijijini na nafikiri iangalie zaidi maeneo ambayo makundi makubwa ya watu yapo na yanahitaji kufikiwa na kupewa misaada hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko Sera inayosimamia Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Fedha nyingi zimekuwa zikiingia nchini kupitia Mashirika hayo yasiyo ya Kiserikali na nadhani sasa hivi uko utaratibu wa kujua fedha hizo zinafanya nini katika kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kuunda Sera hiyo mpya, ambayo inasimamia Mashirika hayo yasiyo ya Kiserikali. Lakini nadhani Serikali bado ina jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba, kazi zinazofanywa na Mashirika hayo yasiyo ya Kiserikali, ya Kimataifa lakini na yale yaliyoko ndani, yanakuwa na mgawanyo sawa wa kiutendaji, yasibakie katika eneo moja tu na kuacha maeneo mengine bila kufikika na kupatiwa huduma hiyo. Kwa hiyo, ninaomba ili kupambana na umaskini, suala la Mashirika yasiyo ya Kiserikali ni muhimu na wao ni wadau wakubwa sana wa kuchangia maendeleo ya Taifa letu. Lakini naomba sana Serikali isimamie vizuri kuhakikisha kuwepo kwa mgawanyo sawa wa kiutendaji wa kutoa huduma katika maeneo mbali mbali kwenye nchi yetu na siyo kuyaacha Mashirika haya yakifanya kazi katika eneo moja tu na kuacha maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, ninaomba tena nichukue nafasi hii, niwapongeze sana Mawaziri hawa wawili. Lakini nirudie tena kusema, kwa kweli nawapongeza sana ndugu zetu wa Mfuko wa *TASAF* na Mfuko wa *SELF*. Naomba nichukue nafasi nyingine kuwashukuru sana ndugu zangu wa *SELF,* kwa msaada waliowapa wanawake wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niongee katika hoja hii ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu kuwapongeza Mawaziri hawa wawili, ni makini sana, kazi zao tunaziona zinafanyika na kwa kweli ni Mawaziri ambao wanakuwa mfano kwa wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea katika suala zima la kupunguza umaskini au kuondoa umaskini. Naongelea suala hili kwa sababu katika Jimbo langu, Wananchi walionituma kuja katika jumba hili ni maskini na wanasikia tu kuwa, kuna mipango mingi ya kupunguza umaskini ambayo inaendelezwa na Serikali lakini hawajaiona. Kwa kweli umaskini lazima tuanze kuutazama kutoka kwenye mizizi yake siyo kwenye matawi. Kama asilimia 80 ya Wananchi wanakaa vijijini na wakulima wadogo wadogo, huko ndiko umaskini kama tunataka kuupunguza, tujaribu kuboresha kilimo. Kilimo kikiboreshwa tutakuwa tumeanza kuondoa umaskini.

Ofisi ya Makamu wa Rais ni Ofisi Kuu Kikatiba, nayo inaweza kuchangia sana katika kupunguza umaskini kwa kuanza kuondoa mizizi ya umaskini. Mimi naweza kusema kuwa, umaskini utaanza kupungua tu pale ambapo tutaboresha kilimo. Pasipo kufanya hivyo tutakuwa tunaimba nyimbo tu, hata tukileta wimbo wa MKUKUTA tutaimba utapita, lakini Wananchi wataendelea kuwa maskini. Tutajipongeza kwa misamiati mingi, ambayo tunaitunga kuhusu umaskini, lakini kwa vitendo bado. Nasema kuwa suala hili tuwe makini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndicho ambacho kingekuwa ni kitu kimojawapo ambacho kingechangia sana, Ofisi ya Makamu wa Rais, ina uwezo Kikatiba kabisa kuingilia na kuhakikisha kuwa kilimo kinaboreshwa. Kilimo kuboreshwa kwake ni kuleta Mapinduzi na Mapinduzi hayo ni kutafuta misaada ambayo itawezesha Vijana wetu walioko vijijini, wazamie kwenye kilimo badala ya sasa ambapo wanamiminika kwenda Mijini. Kwa sababu Mashirika mbalimbali ambayo yanaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, misaada mingi inapelekwa kwenye miji mikubwa na kwenye mikoa fulani fulani tu, lakini sehemu nyingi zimeachwa hivi hivi. Sasa ningeomba Ofisi hii, itumie uwezo wake Kikatiba kuzielekeza pia Wizara za Sekta nyingine, kwenye mikoa na wilaya ambazo hazipati misaada yoyote ya kupunguza umaskini.

Katika hali halisi kilimo kitaboreshwa tu kama tutazamia katika kuchimba mabwawa madogo madogo. Naweza kutoa mfano mmoja, katika nchi ya Zimbabwe misaada ya *NGOs* au Mashirika yasiyo ya Kiserikali, yanawasaidia vijana kuchimba mabwawa madogo madogo kusudi waendelee katika kilimo. Hili suala la mabwawa madogo madogo ambayo yangechimbwa ili vijana hawa waendelee katika kilimo badala ya kwenda mijini, sisi tunalidharau. Kilichofanyika, tunazungumzia tu kuwa kilimo cha kumwagilia kinakua, lakini ukweli uko pale pale kuwa hakijakua na kinaendelea kudidimia. Kama hakijapungua itakuwa maajabu sana.

Tuliambiwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kuwa, sasa hivi kuna hekta 200,000, ambazo zinaendelezwa katika kilimo cha kumwagilia, lakini uwezekano wa hekta milioni 29 zinaweza zikawekwa sawa katika kilimo cha kumwagilia, ni idadi ndogo sana ya hekta hizi ambayo sasa hivi zinaendelezwa katika kilimo cha kumwagilia. Naiomba Wizara hii, ione umuhimu wa kutafuta misaada kutoka Mashirika mbalimbali ya Kimataifa na yale ya nchi ambazo tunashirikiana katika misaada ya maendeleo, kwa mfano, Benki ya Maendeleo ya Afrika, ingependelea sana kusaidia katika miradi ya mabwawa madogo madogo. Misaada kama mikopo ya masharti nafuu sana, kuna Benki ya Dunia pia inatoa misaada kama ile. Kuna nchi kama Marekani, *USAID, SIDA* na *CIDA*, zinaweza kusaidia lakini hazijaelekezwa, hazijaombwa na pia ningeomba Ofisi hii ya Makamu wa Rais, ione umuhimu wa kufidia ile Mikoa na Wilaya ambayo misaada haijafika kuwasaidia vijana wetu. *(Makofi)*

Mwaka 2001 wakati wa Bajeti katika Bunge lako Tukufu, niliongelea suala la kuwa kuna Mikoa mingi na Wilaya nyingi kama Wilaya ya Iramba, zimeachwa hivi zinapiga miayo tu na zinatazama Mikoa mingine au miji mikubwa inasaidiwa na ndiyo maana vijana sasa wanamiminika kwenye maeneo yale. Mfano mzuri ni Dar es salaam, Mwanza na Arusha, unakuta Mashirika mengi sana yameelekeza nguvu zao huko. Sasa kwa kuwa Mashirika yale yana haki ya kuchagua kwenda mahali yanapotaka, lakini Serikali ifidie kule ambako hayajafika. Ningeomba sasa Bajeti hii na Wizara hii, ione umuhimu wa kufidia maeneo yale ambayo kwa kweli yana upungufu wa misaada au Mashirika yanayosaidia.

Katika Wilaya yangu hasa Jimbo langu la Iramba Magharibi, vijana wengi wanalalamika na wengi sasa wanahama wanakwenda Dar es Salaam, Arusha au Mwanza, kwa sababu hakuna misaada inayokwenda. Sasa ningeomba Wizara hii, hasa Mawaziri hawa wawili, waone umuhimu wa kufanya *intensive and detailed study,* mahali ambapo misaada haijafika kuwasaidia vijana, ipelekwe kule. Hatuwezi kuwa mahali pengine wanaendelea, mahali pengine wanarudi nyuma. Kwa hiyo, ningeomba hilo suala lishughulikiwe kikamilifu. *(Makofi)*

Katika Wilaya yangu ya Iramba Magharibi, ningeomba misaada hasa *TASAF* na *SELF,* ifike na iwasaidie vijana ambao Vijiji vyao viko katika Barabara Kuu hii ya kutoka Dodoma, Singida, Shelui, Nzega, Shinyanga, Mwanza. Vijana hawa wanaweza wakapewa misaada ya kusaidia huduma za usafiri na usafirishaji. Sasa wanakaa na kungojea pale wakati mwingine wanageuka vibaka au kungonjea ajali ikitokea ndiyo wanajaribu kuvuna kutokana na maafa yanayotokea. Sasa mahali kama pale, ningeomba Wizara hii ione kuwa iwe maeneo ya kuelekeza, ya kuwasaidia vijana hawa wakae katika ajira halali. Pia ningeomba katika Maziwa madogo kama Ziwa la Kitangire - Wilaya ya Iramba, Wananchi pale miaka yote wamejihusisha na uvuvi lakini wana uduni wa zana za uvuvi.

Katika Kijiji cha Doromoni walikuwa na kiwanda chao cha kutengeneza mitumbwi lakini miaka ya nyuma kikaharibika, kiwanda kile sasa hakifanyi kazi. Ningeomba sasa kiwanda hiki kifufuliwe kwa kupatiwa misaada, ambayo inaweza

kupatikana kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais. Kijiji cha Doromoni, wavuvi wanaomba wasaidiwe wafufue kiwanda chao cha kutengeneza mitumbwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza haya, pia nataka kuongelea kuhusu mazingira. Mazingira yanakuwa duni katika maeneo mengi kwa sababu ya umaskini. Kama tutakuja kuboresha kilimo ambacho ndicho kitaongoza katika kuondoa umaskini na mazingira yataboreshwa. Katika Wilaya yangu ya Iramba Magharibi, kuna suala zima la wafugaji, wana ng'ombe wengi sana lakini wanapokuwa na maziwa yanayotokana na ng'ombe au nyama, inakuwa hakuna soko. Sasa suala la kupata masoko na kuweza kuhifadhi maziwa na kupeleka kwenye masoko ni muhimu. Hawa ni vyema wakapatiwa misaada kusudi waweze kuhifadhi maziwa wanayokamua kutoka kwenye ng'ombe wao kabla ya kupeleka kwenye masoko kwa mauzo. Nilipita kwenye kijiji kimoja cha Ntwike, nikawakuta mvuvi wengi ambao wanavua samaki lakini inabidi samaki wale wakaushwe kwa kuni. Kwa kufanya hivyo, maeneo yote milimani yamekuwa ni vipara. Mwaka 2004 tuliomba kama ikiwezekana umeme upelekwe vijijini katika maeneo ambayo wanaweza wakatumia kuhifadhi samaki.

*Biogas* ni nishati muhimu sana kwa sababu kama wafugaji wana mbolea nyingi, wanaweza kuitumia katika kupata nishati ya kupikia. Mimi binafsi nina mtambo wa *biogas,* mwaka 2004, Maofisa kutoka Wizara ya Nishati, walikuja wakatembelea na wakaandika ripoti, wakasema watanipa nakala ya ripoti na nikawaomba misaada kwa wafugaji wenzangu kujengewa mitambo ya *biogas,* lakini mpaka leo sijapata jibu.

Sasa ningeomba kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, wawaulize Wizara ya Nishati kuwa, kama ikiwezekana watutafutie misaada ya kuwasaidia wale wafugaji wetu wapate kuwa na viwanda vya *biogas* kusudi waokoe mazingira pia.

Mwisho kabisa, ningeomba suala la *Solar Power* litazamwe kwa umuhimu zaidi vijijini, kwa sababu umeme kama ulivyo sasa ni gharama sana, hata ukipelekwa Wananchi hawatautumia sana. Lakini *Solar Power* na *Biogas,* ndiyo inaweza kuwa nishati mbadala kwa matumizi ya Wananchi wetu vijijini.

Kwa hiyo, ningemalizia tu kwa kusema kuwa, kweli suala la umaskini litazamwe kwenye mizizi yake na siyo suala la kupeleka misaada midogo midogo mahali popote, lakini kama tutazamia zaidi katika kuboresha kilimo, basi na umaskini utakuwa ndiyo uwezekano wa kupungua au kutokomezwa kabisa, utakuwa dhahiri.

Kwa haya, ningeomba kusema tena pia kuwa nawashukuru na kuwatakia kila la heri Mawaziri wetu, waliotuletea hotuba hii nzuri na pia nakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniruhusu na nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa kunipa ridhaa ya kurudi hapa, kwa sababu wameniambia nitarudi tu, kwa sababu ajenda yangu haijakamilika na ajenda hii siyo tu ya Jimbo langu, ni ya Kitaifa ya kuhakikisha kuwa kilimo kinahitaji Mapinduzi siyo kuendeleza, hakuna la kuendeleza katika kilimo cha sasa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu, ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwanza, kabla ya yote, napenda kuwashukuru Mawaziri wawili wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri wanayoifanya, pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ujumla, Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu Mwandamizi, Bwana Raphael Mollel, pamoja na Mama Mary Mushi na Wakurugenzi wote ambao wanafanya vizuri katika ofisi hiyo. Nawapongeza kwa kazi zao za kila siku wanazozifanya. *(Makofi)*

Pili, nataka kuchangia sehemu ndogo tu katika ukurasa wa 35 ibara ya 30 na ukurasa wa 40 ibara ya 33. Hayo ndiyo maeneo yangu mawili ambayo nataka kuchangia. Kwanza, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*, halafu pili ni Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo Midogo *(SELF).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika maeneo haya mawili, yote yanalenga kuinua maisha katika vijiji, kuwashughulikia watu wanaoishi vijijini ili hali zao za maisha zipande, pengine ziwe zaidi ya miji au zilingane na maisha ya mijini. Sasa, masuala haya katika nchi yetu ni lazima yapewe kipaumbele sana kwa sababu kwa muda mrefu katika nchi yetu maeneo mbalimbali yalikuwa nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia lengo la Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* pamoja na kazi nzuri ambayo imefanywa na *TASAF* katika maeneo ambayo Mfuko huu umeanza, basi utaona lengo hili linataka lipate nguvu mpya au kasi mpya. Pale katika ukurasa wa 35 ibara ile ya 30 anasema: "Lengo lake kuu ilikuwa ni kushughulikia mahitaji ya Wananchi waishio vijijini na pembezoni mwa miji ili kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii". Lengo la Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo Midogo *(SELF)* pale katika ukurasa wa 40 ibara ya 33 linaelezwa vizuri sana. Kwa kutambua tatizo la ajira nchini, basi Serikali ya Awamu ya Tatu ilianzisha Mradi wa *SELF* ili kuongeza ajira na kipato kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, falsafa ya *TASAF* na *SELF,* naita kidogo ina kasoro, kwa sababu na mimi naelewa falsafa kidogo, kwamba ni kama vile msaada unaotolewa kwa Wananchi, ni wa siku moja. Mwanafalsafa mmoja wa Kichina alisema, ukitaka kumpa mtu kitoweo, basi mpe mshipi pamoja na zana za kuvulia, huyu atapata kitoweo kila siku, lakini ukimpa samaki wenyewe atakula siku moja au siku mbili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, falsafa ya *TASAF* na *SELF,* imeangalia suala la kumpa Mwananchi chakula cha siku moja au kitoweo cha siku moja. Kujenga shule au kisima au zahanati maana yake ni kumfanya huyu Mwananchi, aweze kupata manufaa mafupi ya kile kitu kilichokuwa kimetengenezwa au kimejengwa pale kijijini kwa siku ile, lakini jinsi ya kuendeleza kile kitu kazi hiyo kwake itakuwa ngumu kwa sababu kipato chake kiko chini na uwezo wake ni mdogo. Kwa maana hiyo basi, pakiwa na shule au pakiwa na zahanati au pakiwa na barabara, yeye kila siku atategemea asaidiwe ili mradi ule au jambo lile liweze kuendelea. Nadhani hapa kuna kasoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeanza kumpa nguvu huyu Mwanakijiji *(to empower this villager),* kumpa nguvu ya kiuchumi atakayomiliki mwenyewe mkononi ambayo itamwezesha yeye kuchangia kila siku maendeleo yake mwenyewe badala ya kumpelekea pale msaada. Kwa hiyo, nadhani msaada wa *TASAF,* falsafa ingegeuka sasa, badala ya kupeleka pale Mwananchi achangie na huku Serikali inamletea kukamilisha nguvu zake kumwezesha, basi imwezeshe yeye kiuchumi, amiliki nguvu ya kujisaidia yeye mwenyewe pale. Kwa hiyo, tusingeanza kumpelekea pale msaada wa kujenga zahanati au shule au barabara au kingine chochote kile au kuchimba kisima, bali tumpe msaada wa yeye mwenyewe kuweza kujiendesha, ambao yeye atakuwa na uwezo nao, mfuko wake utamwezesha kuweza kuendesha maendeleo hayo kijijini pake. Hili nadhani lingekuwa la maana zaidi katika kumwona huyu mkulima au huyu mtu wa kijijini, tunataka maisha yake yaboreke.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo ninaunga mkono kabisa wazo lile la kupeleka nyenzo muhimu katika upande wa kilimo. Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukilizungumza hili suala kwa muda mrefu sana. Kilimo cha umwagiliaji kimekuwa ni nyimbo za *Alfulela-Ulela* au habari za *Alfulela-Ulela.* Ninachoiomba Serikali ni kwamba, kama kweli inakusudia kuwaendeleza Wananchi wake vijijini, basi iangalie jinsi gani ya kupindua na kugeuza hali ya kilimo na kwamba kilimo kile cha kujikimu sasa kiondoke, kiwe cha biashara, ambacho kitamwezesha huyu mwanakijiji kumiliki uwezo wa kuendesha mambo yake ya kimaendeleo pale kijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, si tu kupindua kilimo, hapana. Hapa kutakuwa na vitu vingi vya mtambuko vinavyohusiana, kwa mfano, viwanda vidogo vidogo. Baada ya kulima mazao haya, huwa mara nyingi sehemu kubwa inapotea karibu asilimia 50 au 65, kwa sababu mkulima vitu vingine hawezi kuvitunza, haviwezi kukaa kwa muda mrefu vinapotea huko shambani, kama matunda yanapotea sehemu kubwa sana. Tusindike matunda haya ili kuyapa thamani zaidi, yaweze kukaa kwa muda mrefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kupeleka viwanda vidogo vidogo vijijini *(small industries, cottage industries)* kama walivyofanya wenzetu kule India, China na Japan, walianza huko. Hakuna budi ndugu zangu tunapozungumza masuala ya kupeleka hali nafuu na kupunguza umaskini vijijini ni lazima huyu mkulima tumwezeshe, siyo tumpelekee msaada wa kujenga zahanati na shule au barabara, hapana. Yeye mwenyewe tumwezeshe kutokana na nafsi yake, awe na uwezo wa kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri *SELF* kama jina lenyewe lilivyo katika Kiingereza, *SELF* maana yake ni nafsi, mtu binafsi, basi tumwezeshe huyu mtu binafsi. Huu msaada mdogo mdogo umwezeshe huyu mtu binafsi ili aweze kuondoa umaskini wake yeye mwenyewe na familia yake na kaya yake.

Natoa wito kwa *SELF* na *TASAF,* falsafa igeuke, badala ya kupeleka fedha asilimia 80 imsaidie mwanakijiji na yeye mwenyewe atoe asilimia 20, bali asilimia 80 hii iwe ya kumwezesha yeye asaidiwe katika kilimo chake kubadilisha kama ni mvuvi apate zana nzuri zaidi za uvuvi, ikiwa ni mkwezi wa minazi apate zana nzuri za kukwelea

minazi, ikiwa ni mkulima wa korosho au mazao yoyote apate zana nzuri za kufanyia kazi hiyo na kugeuza maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF* na *SELF* sasa igeuke kabisa badala ya kupeleka fedha za kusaidia tu kujenga zahanati, shule, visima na barabara, sasa ni kwamba, imsaidie huyu mkulima kugeuza maisha yake yeye mwenyewe katika kazi yake ili kazi iwe bora zaidi, itoe tija kubwa zaidi, aweze kuchangia maendeleo yake kila siku, siyo mara moja tu au mara mbili tu katika mwaka, hapana, kila siku katika maisha yake, awe na uwezo wa kuchangia maendeleo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi hili nalielekeza katika Ofisi ya Makamu wa Rais, wenye dhamana ya kuondoa umaskini, hasa hasa Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, ni mtani wangu, ndugu yangu, ninamjua kwa muda mrefu sana amekuwa pale, kwa muda wa miaka 30 amekuwa Mbunge wa Nachingwea kule. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kabla hajaacha ofisi, ingawa yeye anasema mwaka huu ndiyo anamalizia kipindi hiki cha Ubunge kama mimi, ninamwomba jambo hili aweze kulishughulikia ku...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, umekubali itoke taarifa?

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Yeye ni rafiki yangu hawezi kunikatalia. Subiri bwana usiniharibie mambo yangu, sijakutangazia rasmi, subiri. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeikubali taarifa hiyo na ninafuta usemi wangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najua Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo katika Ofisi ya Makamu wa Rais, atafanya kazi nzuri kama alivyofanya *TASAF* ya kuweka asilimia 80 iende katika miradi hiyo ya kusaidia Wananchi, basi sasa iende katika kuwapa nguvu wakulima kule vijijini ili waweze kuendelea katika kazi zao za kuwapatia maisha yao yawe bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, langu lilikuwa ni hilo tu nimechangia katika ukurasa ule wa 35 na 40, ibara za 30 na 33 na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, imetolewa taarifa hapa, ni kweli kila mtu ana utaratibu wake na mbwembwe zake za kujiwekea mikakati ya mbele na kuaga au kuendelea. Sasa si vizuri kusemeana, kila mtu ana utaratibu wake.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, nami niwe mmojawapo katika wanaochangia hoja ya Ofisi ya Makamu wa

Rais. Hoja iliyoko mbele yetu inasema kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya mwaka 2005/2006. Nimekubali kwa kuwa hata Mpinzani ameunga mkono. Kwa hiyo, tumeona kwamba, kumbe mbele ya Watanzania wanaojua maslahi ya nchi hii, wameamua kuunga mkono hoja za Serikali ya Chama cha Mapinduzi (Chama Tawala), ili kuona kwamba, tunaiendeleza nchi yetu. Huo ni ustaarabu siyo wa Venice, ni ustaarabu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi ni kwamba, nilitoa shukrani, niliishawaandikia tayari watendaji kule kwa kufika hapa salama na hili ndiyo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huyo ndiyo Naibu Spika na mimi ndiyo Semindu Kisange Pawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ni mmoja katika Viongozi ambao wanajituma, huwa wanafanya kazi leo, hawangoji kesho, wanajua kabisa kesho ni ndoto, jana historia, leo vitendo na anatenda kweli. Ni mwanasayansi, lakini amejikita katika siasa kwa sababu anamuweka Mungu mbele, umma kati na kubaki nyuma yeye ili kuongoza umma wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mawaziri wake wawili hawa, nimewaita Wabunge njiti, kwa sababu imeonekana kama wamekuja kabla ya wakati wao, walitakiwa waje Bungeni mwaka 2005. Naomba mgombee, msije mkajitangaza vingine. Ninyi ni Wabunge njiti, mlikuja kabla ya wakati wenu, ni wale *premature,* mnabaki kuwa ni Wabunge wa aina hiyo. Waendelee kutumikia watu wao katika maeneo yale ili tumsaidie kijana wetu ambaye atashika madaraka ya Kitaifa. Huwezi ukaacha shamba likawa halina hata kisiki, wazee mnahitajika sana. Ukilima shamba bila ya kisiki, maana yake ni kiwanja cha mpira, sasa huwezi kupanda. Naomba tafadhali sana wazee wenye busara mbaki tumuongoze kijana wetu Awamu ya Nne ili tumuendeleze vizuri. Huo wito utolewe kwa Wananchi wa Majimbo yote kuanzia Lindi huko mpaka Mikoa yote ya Tanzania, tunataka muongoze kutokana na uzoefu ambao mmeupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *NEMC,* Bwana Reginald Mengi na kuna mtu anaitwa Yonas, huyu alitusaidia kurekebisha ile Katiba ya Muungano Mazingira *Organization* mpaka tukaiandikisha. Mama Mushi, ninamtaja ili itoke kwenye *Hansard,* kwa sababu yeye ndiyo alituelekeza vizuri kuandikisha *NGOs* tatu katika Jimbo hili ili kusimamia mazingira. Kwa hiyo, kuna *NGOs* tatu, ipo *Magera Women Organization,* ambayo inapanda miti, ipo *NGO* nyingine inaitwa *Mtukinge Women Organization* ya Ngerengere na ipo *Muungano Mazingira Organization,* ambayo inashughulikia milima ya Uluguru yote kuanzia kule Logo, Uponda, Mifulu, Hewe, Bagilo, Nyamigadu, Mkololo, Kumba, Amini, Ludewa, Burugi, Lung'ala mpaka maeneo ya kule Tandai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuja nao juzi, lakini bahati mbaya kumbe ilikuwa siyo siku ya Wizara hii, nimeamua waondoke kwenda kushughulikia kupanda miti, ila Kamati yao ya watu wawili bado ipo hapa inasikiliza jinsi mlivyosaidia. Wale wa *Muungano Mazingira Organization,* wapo kushoto kwangu, mtawaona baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza utangulizi, naingia upande wa Muungano. Muungano siyo nchi, ni nchi na watu. Hivyo, ukipeperusha na kupekua na kukokotoa dosari za Muungano utasema kwamba ni mimi na wenzangu. Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Abeid Amani Karume, ambao wanapongezwa kwa kitendo chao, baada ya uhuru walisema, kwanza sisi wengine baadaye. Tukaungana nchi za Tanganyika na Zanzibar kufanya Tanzania na kuwa na Serikali ya Zanzibar. Hatukugombana kuhusu majina, majina ni uelekeo ule ule kama chai. Sukari, maji na maziwa walipokutana katika birika walisema, jamani samahani, wote tuitwe chai, ili wote tupoteze majina yetu. Wakakubaliana ikaitwa chai. Hata ukila na kuku wanasema vinaitwa vitafunwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitokea vurugu za kutokukubaliana kati ya mchanganyiko ufuatao; kitunguu, nyanya, pilipili na chumvi kidogo, wakasema kila mtu anataka aitwe yeye, matokeo yake binadamu aliyetengeneza mchanganyiko huo akawaambia, hakuna kutaja kitu chochote tutaona ubishi wenu, mtaitwa kachumbali. Hakuna kutaja mtu pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Muungano wetu ni wa makubaliano ya watu ambao tumekaa na siyo lazima kila mtu awe anaulizwa, ni lazima kuna *founder* kama akina *Avolgado's Principles,* asingoje kuuliza dunia nzima. Watu kama *Pythagoras Theory* au *Archimedes Principles*, wangesema tuulize mmoja mmoja kuanzia Marekani mpaka wapi kwamba, kitu kikielea maana yake nini, ingechukua miaka laki moja kupata *formula. Archimedes* aliamua mwenyewe kwamba, *floating body presents its own weight.* Watanzania duniani kote, nchi zote Afghanistan mpaka wapi, dunia nzima wanafuata *principles,* kilichobakia wanatumia *formula* ile sasa ku-*modify* meli ambayo haizami kutokana na *principles.* Wazee walifanya *principles,* sisi tunakwenda kufuatilia masuala ya utekelezaji. Kwa hiyo, Muungano udumu daima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazingira nimesema kwamba, kusimamia mazingira kule kwenye *sub-vote* ile kwa kiasi kile ni sawa sawa na kuomba jamvi kwenye msiba. Kiasi kilichotolewa ni kidogo mno katika mazingira, kwa sababu mazingira ni suala la Kitaifa na Kimataifa. Dunia sasa hivi inakemea mpaka tumeweza kuweka sheria hapa. Tembeeni mwone. Wakati mmoja tulikwenda Namibia, tuliiona Afrika, tulianza kubadilika. Kutoka Msumbiji kwenda Kusini, yaani miti imekwisha kabisa!

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana chura alipata mlio wa ajabu kwa kutokutembea. Alizaliwa kule kisimani akiwa kiluilui, akakua akawa chura, bila kutoka nje kuangalia mazingira yake. Matokeo yake alipoulizwa swali kwamba, mbingu ikoje, akasema ni kubwa kweli inaziba mdomo wa kisima changu. Hiyo yote ni kwa sababu hakutembea kuona mazingira ya nchi. Lakini baada ya maji kukauka kutoka nje, akaona mbingu haina mwisho ndiyo akaanza kushangaa hee, hee, hee. Mlio ule anashangaa ikawa milele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutembee tuone mazingira ya wenzetu yalivyoharibika. Tumejifunza kule kwamba, ukichezea mazingira unachezea hali ya maisha ya nchi yako.

Kwa hiyo, tuyalinde mazingira yetu kwa utaratibu huu. Napenda nimpongeze Mwenyekiti wa *NEMC* na Wasimamizi Wakuu wa Idara *NEMC,* ambayo nilikuwa Mkurugenzi pale. Kwa muda wa miaka mitatu, pamoja na Baraza lile, tuliweza kufanya mambo mengi, lakini wenzetu wamekwenda mbele zaidi. Kutembelea maeneo ambayo yanahusika na uharibifu wa aina hiyo, hii ni kazi nzuri. Nachukua nafasi hii, kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kufanya mambo haya mpaka Kamati yake imetembelea maeneo mbalimbali, maeneo ya wakimbizi yanaharibiwa kule, maeneo ya Kibondo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nilisema juhudi za watu za kujiletea maendeleo zinaharibu mazingira, kama suala la kuchimba shimo kufukia kichuguu kazi ya ambayo haiishi. Kama unaona kichuguu kinakuudhi kisambaze, usichimbe shimo kwenda kufukia kichuguu kile, utapata mchanga ambao utatokea kama kichuguu cha kwanza, itabidi uchimbe shimo lingine kufukia mchanga uliotoka shimo la kwanza. Kwa hiyo, itakuwa *continuous processes based upon the sure foundation of previous successful and effectiveness.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira nayo tuyasimamie wote kwa pamoja kama ni vita. Tumetangaza vita ya mazingira kutokuharibiwa. Kwa upande wa viwanda, tumeshapitisha Mikataba mingi hapa tu ya Kimataifa, kwa mfano, ile ya kuondoa taka ngumu, usafirishaji wa kemikali, *organic persistent,* vipo vingi tu. Sijui kama ipo *taken care* katika ile Sheria ya Mazingira au ilikuwa inatengenezwa kama ile *Kyoto Convention* au *Bael Conventions.*

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa mito inayotoka milima kama ya Uluguru kule na mito mingine inayotoka milima mingine yanakuja maji *fresh* na kupita kuingia baharini, lakini mito inayoanzia na kupitia kwenye miji inachafuliwa kweli. Nilikuwa naangalia tovuti kule kuangalia *part per million on chemical composition* katika mito kama Mississippi ambayo ina kilomita karibuni 6,019 ama Amazon ambao urefu wake ni kilomita 6,515 au *Danube Delta* kule Ulaya au Panama na mito kama Volga, tulinganishe na mito yetu ya hapa Afrika kama Mto Zaire na mito kama ya Ruvuma, Ngerengere na Ruvu, tuone nani watundu wanaharibu mito yao zaidi. Lakini taarifa hiyo nitaipata sasa hivi, nimemtuma kijana akailete, najua mtakuwa mmeipata, lakini nitaleta kama kusisitiza mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo, tumeunda kikundi ambacho kinaitwa *Muungano Mazingira Organization*. Kulikuwa na vikundi vinatoka Dar es Salaam, wakidanganya eti wanapanda miti milima ya Uluguru, jambo ambalo si kweli. Tumeamua kwamba, wanaokaa katika milima ile wapande miti. Kwa hiyo, vijiji nilivyovitaja ndiyo wanasimamia wenyewe na mimi ndiyo mlezi wa kikundi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuja hapa Bungeni, tumemwona Mheshimiwa Zakia Meghji na leo watamwona Mheshimiwa Waziri, kama atapata muda au kesho, pamoja na Katibu Mkuu wake ili tuongelee masuala ya mazingira. Tulishaandika *write-up* yetu kwa ajili ya kupanda miti katika milima ile ya Uluguru na yupo Chifu kule Kingalu Mwanabanzi. Miaka ile walitumia mwiko, siku hizi vijana hawajui mambo ya

mwiko, ni lazima kuwe na utaratibu wa kuwaeleza kisayansi kwamba, mnapoteza hali ya hewa, hewa ni safi. Nimeshamweleza Waziri kikundi hicho kimeshaandika *write-up* na kuomba msaada fulani. Ni vikundi vya akina mama, vijana na kadhalika. Kwa hiyo, mazingira nimemaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaingia upande wa umaskini. Maskini niliwaambia ni mtu asiyekuwa na kipato. Hakuna *definition* maalum inayoeleza maana ya maendeleo. Wataalam walisema, *no single definition of economic development, is entire satisfactory.* Kuna *tendency* ya kutumia ya maneno yafuatayo: *Economic growth, per capita increment, interchangeably* na *secular change. But what extent can you ask such a term?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Tanzania imechukua hatua nzuri sana katika kupambana na umaskini. Wamechukua hatua kwanza ya kuwaambia Watanzania waunde vikundi mbalimbali. Pato la Taifa lilipokua tukasema ule uchumi jumla utamsaidiaje Mtanzania wa kawaida katika kuhakikisha kwamba, anaepukana na matatizo yake binafsi? Kabla hatujawagawia Watanzania, Serikali ya Tanzania, imeamua angalau kumpunguzia mzigo kutokana na pato hili, kufuta kodi sitini ambazo zilikuwa ndani ya Halmashauri, ile ilitokea ili kumpa afueni Mtanzania huyu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili, tukafuta kodi za maendeleo. Hiyo ni moja, nyingine ni kuanzisha vikundi vya akina mama, vijana, makundi maalum na watu wengine na tunavyo vikundi hivi na hapa ninawapongeza vijana. Zamani kulikuwa na utaratibu wa vijana, wakifika tu miaka 18 anahamia mjini, lakini vijana sasa hivi kwa kweli mkienda vijijini mnawakuta wengi, wameamua kubaki pale pale na wanahitajika kuhudumiwa huko huko. Tusitumie mfumo tochi, kuwamulika kwetu likabaki giza. Tuwapelekee maendeleo vijana pale walipo, mfano maeneo ya kule Lung'ala, Kandai, Bagilo, Mgozo, Amini, Kiloka na maeneo ya Kiziwa kule Mikese na sehemu za mchangayiko. Maeneo ya Fulu na Ngerengere, wamejitengenezea vikundi vyao na vimeshazinduliwa tayari. Wao wenyewe walitengeneza baiskeli na vitu vingine na akina mama wanajitokeza kufanya biashara mbalimbali. Nimemaliza upande wa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naingia *TASAF. TASAF* wamefanya kazi nzuri. Kwa upande wa elimu, Kitaifa mmefanya miradi 782. Kwa Wilaya yangu elimu ni miradi 11, maji mlikuwa na miradi 216 Kitaifa, lakini kwa Wilaya ni miradi minne, yote imekamilika. Tunasikitika kwamba, mradi mmoja wa Kidugallo, kuna mtu analeta mchezo pale. Tumeshaleta nguzo tayari, *wiring* imefanyika, lakini bado toka mwaka 2004 mradi haujakamilika. Wananchi wamepata matatizo kwani wamechimba mtaro ukafukiwa, wakachimba mwingine ukafukiwa. Kwa hiyo, sasa hivi tunawashauri wachimbe tena ili nguzo za umeme zipate umeme uende pale kutoa umeme, maji yapo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la afya, tuna miradi 834 Kitaifa, Wilayani tuna miradi kama 13. Kule nashukuru ipo miradi 18, lakini bado mingine haijakamilika. Ni lazima muangalie miradi ambayo haijakamilika katika jedwali mliyoitoa hapa, pengine fedha imeliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili twende pamoja ni lazima tujitume, tujiamini na tuamini wenzetu, tuwe waangalifu, kutohoji mambo ambayo yamekamilika, lakini ambayo wewe hukushiriki. Kwa hiyo, watu wanaopuuza kwamba, Tanzania haina maendeleo au Jimbo halina maendeleo, nimesema aidha ni mgeni na kama ni mgeni aelimishwe. Lakini kama ni mwenyeji, kwa sababu mfumo wa uendelezaji wa nchi hii ulikuwa shirikishi, huyo apuuzwe. Tuwe na ushindani, kuacha mizaha, kujali wanavijiji, kujipa moyo, kujipanga vizuri na kwenda mbele ya Taifa, siyo kwenda mbele yako binafsi. Vile vile, kuna kuelewana na kukubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wawili walikubaliana bila kuelewana. Mmakonde mmoja alikuwa anauza muwa, Mmasai akauliza, muwa shilingi ngapi? Mmakonde akajibu, muwa Sh. 200/=. Mmasai akasema, punguza. Mmakonde akajibu, nikipunguza itakuwa Sh.100/=. Mmasai aliposikia kwamba, itakuwa Sh.100/=, akamwambia Mmakonde, Yero, mimi nataka bei ya mwisho. Mmakonde akamwambia, bei ya mwisho Sh.20/=. Mmasai alipotoa Sh.20/= kumpa Mmakonde, Mmakonde akakata mwisho wa muwa kule ambako siyo kutamu. Mmakonde aliposikia bei ya mwisho, yeye alidhani kwamba, alitaka mwisho wa muwa, kumbe alitaka bei ya mwisho kwa muwa mzima. Kwa hiyo, wale hawakuelewana, zilitaka kupigwa pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, twende mbele tusisisitize mambo, kwa sababu kuna mambo mengine ukisisitiza yanakuwa hayana msingi. Kwa mfano, inaundwa timu, ni timu ya mpira, lakini timu timu ukisema mara mbili ni kutibua. Ukisema kutibu ni kutibia, lakini ukisema tibu tibu umeharibu. Mtu akiumia ukimwambia pole maana yake umemfariji, lakini akiumia mara mbili ukimwambia pole pole ni taratibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii, asubuhi hii, nikushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia katika hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais. Pamoja na kunipa nafasi hii, nianze kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri anayesimamia Mazingira, pamoja na Muungano. Vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kipindi chote ambacho wamekuwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi ya pekee, nimshukuru Mheshimiwa Ntagazwa, kwa jinsi ambavyo alitukubalia mwaliko wetu kule katika Wilaya ya Same, kuhudhuria kongamano la kuweza kupambana na uharibifu wa mazingira kwa Wilaya mbili za Mwanga na Same, kongamano ambalo liliendeshwa na kugharamiwa na Mhashamu Baba Askofu, Jacob Venance Koda wa Jimbo Katoliki la Same. Aliweza kuwa pamoja na sisi kwa muda wa siku nne za kongamano, kushiriki pamoja na Wajumbe wa Wilaya zote mbili na kuona athari za uharibifu wa mazingira na alionesha uvumilivu mkubwa na mchango mkubwa katika kongamano lile.

Ninakushukuru sana na ninakupongeza kwa jinsi ambavyo umeweza kushirikiana nasi. *(Makofi)*

Lakini pamoja na kukushukuru, nikuombe kwamba, yale Maazimio yaliyopitishwa na lile kongamano, ukiwa Waziri ambaye umeshika dhamana ya mazingira katika nchi yetu, uweze kuyawekea kumbukumbu na mpango wa kufanyiwa kazi ili kuweza kuzinusuru Wilaya za Same na Mwanga katika uharibifu wa mazingira ambao hivi sasa umekuwa ni tishio la Wananchi wetu kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nichukue nafasi nyingine kuwapongeza Viongozi ambao walipata nafasi za uteuzi za Kitaifa kwa tiketi ya CCM. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze, pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuteuliwa kwa nafasi ya kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uteuzi wake, kule kwetu Same wameanza kuwa na salamu mpya. Jina Jakaya kwetu maana yake ni habari za nyumbani. Sasa siku hizi watu wakiamkiana Jakaya wanasema Kikwete. Yaani habari za nyumbani, wanasema Kikwete. Kwa hiyo, wanaanza kumpigia kampeni ya nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi nyingine kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuweza kupata nafasi ya kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kwa nafasi ya Mgombea Mwenza kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, ninampongeza sana. Nimpongeze pia Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuweza kuteuliwa kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nichangie katika hotuba ya Waziri wa Nchi. Nianze kwanza na Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo Midogo, huu wa *SELF*. Katika ukurasa wa 41 fungu la 33, iko sehemu ambayo Mheshimiwa Waziri, amesema *84 percent* ya mikopo inatolewa kwa Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS),* ikiwa na maana asilimia nyingine 16 inatolewa kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs).*

Sina mgogoro na utaratibu wa Waziri, lakini nafikiri hizi *SACCOS* watu wanaweka ili wakope na pale katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali nafikiri Wananchi wetu, ambao wengi wamezidiwa na umaskini, hawaweki pale, wala hawakopi pale. Kwa hiyo, wale wanachukua fedha zile kwa ajili ya kuwakopesha tu Wananchi lakini Wananchi hawakuwekeza pale. Wanasema mwananchi anajikuna pale mkono wake unapofikia na nafikiri kwa Wananchi wetu wengi walio masikini, mkono wao unajikuna pale unapofikia kwenye *SACCOS* ambayo ameweka na hivyo anaweza kukopa. Kwa hiyo, ningeomba kwa wakati ujao, Mheshimiwa Waziri sasa atoe asilimia 100 kwa hizi *SACCOS. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuweza kuipatia mkopo *SACCOS* yetu moja kule Same *(Same Chamber SACCOS)* wa shilingi milioni 75. Lakini nimtahadharishe Mheshimiwa Waziri kwamba, baada ya ule mkopo kutolewa kwa ile *SACCOS* moja, ziko *SACCOS* nyingine nane ambazo wamekuwa wakilalama sana, kwa sababu wao hawakuweza kupata mkopo hata shilingi moja. *SACCOS* hizi ni ile ya Mwangaza, *SACCOS* ya Mji wa Hedaru, *Kwanduju SACCOS* ya Mji wa Makanya, *Shengena SACCOS* ya Kata ya Suji, *Mkombozi SACCOS* ya Kata ya Mwembe, *Kisiwani SACCOS* ya Kata ya Kisiwani, *Kumekucha SACCOS* ya Kata ya Njoro, *Ushamiru SACCOS* ya Kata ya Ruvu na *Same Kaya SACCOS,* ambayo ni *SACCOS* ya karibu Wilaya nzima. Hizi zote Wananchi wameweza kuchangia mno kuwekeza, lakini hawakuweza kupata hata mchango wa shilingi moja kutoka *SELF.* Ningekuomba Mheshimiwa Waziri, katika Bajeti yako ya sasa, uweze kufikiria *SACCOS* hizi nazo ziweze kupata mgao wa mkopo ili ziweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, aangalie *SACCOS* zilizoko Vijijini hasa ambazo ni *typically rural* na zilizoko Mijini *(urban),* zina tofauti. Maskini wa kijijini na maskini wa mjini hawafanani. Ujanja wa maskini wa kijijini na ujanja wa maskini wa mjini haufanani. Mimi ningefikiri maskini wetu wengi walioko vijijini wamezidiwa mno, wanahitaji kupewa msaada zaidi ya wale walioko Mjini. Kwa sababu kwanza, kule vijijini mzunguko wa fedha ni mdogo sana, hawa walioko mjini mzunguko wa fedha ni mkubwa. Kwa hiyo, kama tunataka usawa, Mheshimiwa Waziri, nguvu zako nyingi zielekeze kwenye *SACCOS* zilizoko vijijini na huko ndiko Watanzania wengi walipo na ndipo ambapo Mheshimiwa Waziri, pamoja na sifa hizi ambazo tumekupamba nazo na ambazo unastahili pamoja na Mheshimiwa Waziri mwenzako, tunasema ukizipeleka kule, basi wewe utakuwa unawaka kama nyota ya angani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili niongelee kidogo kuhusu *TASAF.* Naipongeza Serikali na Waheshimiwa Mawaziri wawili hao, kwa kuweza kusimamia *TASAF* vizuri na imefanya mabadiliko makubwa sana katika nchi yetu, sehemu ambapo miradi yake imeelekezwa. Kwa bahati mbaya kule kwetu Same na sehemu nyingine za nchi yetu, *TASAF* haijafika. Lakini kwa sasa hivi, naambiwa na tumeelezwa hapa Bungeni kwamba, itasambazwa nchi nzima.

Sasa ningekuomba Mheshimiwa Waziri, wakati inapopelekwa nchi nzima, ikiwa ni pamoja na kule Same, ukatusaidie kuiangalia ile Wilaya kwa jicho la huruma, ndiyo Wilaya ambayo ni maskini sana katika Mkoa wa Kilimanjaro, ndiyo Wilaya ambayo imezidiwa. Uchumi wake bado ni ule wa kutembea kwa miguu. Asilimia 80 ya wakazi wa Same wanaishi milimani, ambapo barabara ni mbovu. Wale ambao wameweza kufahamu ile Wilaya, watakubaliana na mimi kwamba, uchumi wetu bado ni wa mguu wa kushoto kulia, kushoto kulia kama ambavyo Mheshimiwa Profesa Sarungi, ananiangalia, anafahamu alikuwa Mkuu wa Mkoa kule. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri, wakati *TASAF* inakwenda kule, zile barabara zikaboreshwe, tuondolewe ule uchumi wa kutembea kwa miguu, tuwe na uchumi wa kutembea kwa magari na kusafirisha mazao yetu kwa magari, badala ya kusafirisha kwa kichwa au kwa punda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningemwomba Mheshimiwa Waziri, wakati *TASAF* inafika kule, waweke miradi ya kuboresha huduma za maji safi na salama, afya na elimu. Ni kweli MMEM imefanya kazi nzuri na sasa MMES inaingia, lakini bado kuna haja ya kuboresha Elimu yetu ili iweze kuwa ya juu mno na ndiyo nguzo pekee ya kuweza kumwondolea mwananchi umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeomba *TASAF* iangalie ni kwamba, kule Same tuna rasilimali za mito mitano ambayo ina maji majira yote ya mwaka, tuna Mto wa Pangani, Hingilili, Yongoma, Sasemi na Nakombo, yote hii ina maji lakini kilimo cha watu wetu hakijaweza kuendelezwa na siyo cha kisasa. Ningeomba *TASAF* ikiingia kule Same, ikaangalie hilo. Tuna rasilimali ya milima pale, ningeomba ile milima tuvune maji ya mvua sehemu ambazo kuna ukame ili Wananchi waweze kuhifadhi mazingira, pamoja na kukuza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia eneo la Same pale kuna upepo sana, tutumie ule upepo kama rasilimali tuweze kutumia kwa *pump* za kutumia upepo kupandisha maji, pia kuweza ku-*generate* umeme, ambao utawasaidia watu wetu kuachana na adha hii ya kuharibu mazingira kwa kuni na mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee la tatu kuhusu mazingira. Kule Same mazingira yameharibika sana kwa sababu ya kuchoma mkaa, kuni, pamoja na ufugaji. Sasa ningeiomba Ofisi ya Makamu wa Rais, inayohusika na mazingira, itusaidie wale watu hawachomi mkaa kwa sababu wanapenda, hakuna mtu aliyepata wimbo mzuri akashindwa kuimba, hawajaupata. Watu wanaoharibu mazingira wanaharibu kwa sababu uchumi wetu ni wa kupata chakula cha siku ile ile na siyo cha kesho. Wazungu wanaita *hand to mouth life.* Sasa haya maisha ya *hand to mouth,* siyo mazuri. Serikali iingilie kati, watu hawa wanaoharibu mazingira mpaka sasa wanauza mkaa nje ya nchi, nimelisema hapa, sijui Serikali imechukua hatua gani. Mkaa unafanywa sasa umekuwa ni bidhaa ya kuuzwa nchi za nje, mazingira yanazidi kuharibika ni moja ya kuongeza umaskini, nchi inakuwa jangwa. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, aweke mikakati, pale ambapo Wananchi wanachoma mkaa wawekewe miundombinu ya kilimo, wafanye kazi ya uzalishaji katika kilimo badala ya kuchoma mkaa. *(Makofi)*

Hawachomi mkaa kwa sababu wanapenda, sisi viongozi tunapita barabarani tunakuta magunia mengi ya mkaa na wengi tunatamani kutumia mkaa huo kupikia nyumbani kwetu, lakini huo mkaa utatuingiza katika janga kubwa la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuielimisha jamii kuhusu athari za kuharibu mazingira. Naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa vipindi wanavyoweka, lakini bado vipindi hivi na elimu hii haiwafikii Wananchi kule Vijijini. Misitu yetu inaharibiwa mno, mazingira yetu yanaharibika mno, hii elimu ikifikishwa Wananchi wataweza kujua thamani na dhamana ambayo mazingira yao yamewawekea katika uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kukushukuru wewe kwa kazi yako nzuri na makini, ambayo umekuwa ukiifanya ya kumsaidia Spika wa Bunge letu, kuliongoza vizuri katika kipindi cha miaka mitano. Nakupongeza sana kwa busara zako nzuri na sisi tunakuombea, kwa imani yako kwetu na sisi imani yetu kwako, Wananchi wa Jimbo lako la Tunduru, wawe na imani hiyo hiyo, wakurudishe hapa Bungeni. Wanasema imani huzaa imani na mimi naamini kabisa, Wananchi wale watazaa imani ambayo na sisi tumekuwa nayo na wewe. *(Makofi)*

Mwisho, naunga mkono hoja na kumwomba Mheshimiwa Waziri, akumbuke zile *SACCOS* zangu ambazo hazikupata fedha na jinsi mazingira kule Same yanavyoharibika sana, aweze kuangalia ni vipi ataweza kuweka mkakati wa kusaidiana na sisi ili kuweza kunusuru yale mazingira yasiwe jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki, hautoshi kwa Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, kuchangia, sasa atapata nafasi mchana kabla ya Waziri kuanza kujibu. Kwa hiyo, tukirudi ataanza Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, kwa muda wa dakika 15 halafu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Kuondoa Umaskini, ataanza katika ule utaratibu wa kujibu hoja.

Baada ya kufika hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Wizara hii muhimu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kutaka kuwaunga mkono Mawaziri wetu wawili hawa kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa Taifa letu hili na kudumisha Muungano wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uadilifu wake mkubwa na kuweza kuisimamia Ofisi hii kwa mafanikio makubwa ambayo yamethibitisha Muungano wetu wa Tanzania.

Lakini vile vile mafanikio ya Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, hayakuja tu, lakini pia ni uaminifu mkubwa, upendo mkubwa aliyoupata kwa Mawaziri hawa wawili. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri hawa pamoja na Watendaji wao kwa ushirikiano mkubwa yaliyomwezesha Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuanza kutekeleza majukumu yake ya Taifa kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi mkubwa Mheshimiwa Mwenyekiti, unaonyesha hata Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa haikufanya kipingamizi kuweza kumteua kwa kushirikiana na mgombea wetu wa Urais kwa kupitia CCM kumteua awe mgombea mwenza katika uchaguzi mkuu unaofuatia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mafanikio haya hayakuja tu. Laiti kama hakupata msaada mkubwa wa watendaji wa Mawaziri hawa kwa kweli asingelifikia hatua aliyofikia na kwa hapo nataka nitamke kwa wazi kwamba ninaunga mkono hotuba hii asilimia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nashukuru kwamba katika ukurasa wa tano ameelezea kuhusu Muungano na akasema Muungano wetu umetimiza miaka 41 tangu kuundwa. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri kwamba ni kweli mafanikio makubwa yamepatikana na tuombe wale Watanzania wenzetu ambao wanatumia sababu zao za ubinafsi zaidi, kusema labda Muungano wetu hauna faida yoyote. Kwa kweli wakae wafikiri na kwa kweli wawe wa kweli kwa umma wa Tanzania wathibitishe kwamba Muungano wetu una faida katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 41 si kidogo sana na tunafanya makosa tunapolinganisha Muungano wetu wa miaka 41 tukalinganisha na Muungano wa Amerika *(United States of America).* Wenzetu wapo tangu mwaka 1976, Tuangailie ni miaka mingapi wako katika dunia hii ndani ya Serikali zao hizi.

Kwa hiyo, ni vizuri Watanzania tukawa wa kweli, tusifanye haraka ya kukimbilia mbele wakati bado tunaanza kuondoka, sasa cha msingi tuimarishe umoja wetu, tuimarishe uadilifu wetu, tuimarishe mshikamano wetu, ili kujenga umoja wetu wa Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 8, ameeleza kwamba tatizo la wafadhili kusitisha misaada kwa Zanzibar limepata ufumbuzi na misaada hiyo kwa sasa inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nithibitishe ni sahihi kabisa hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kwa kweli tunashukuru sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ninaamini wafadhili hawakurudi tu, inawezekana ni juhudi kubwa ambayo Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeifanya. Kwa kweli Zanzibar tulipozuiwa misaada tulipata matatizo makubwa sana na hakuna nchi yoyote ambayo inaweza kuendelea bila kupata misaada ya wafadhili na nchi zile wahisani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada ndiyo inayosaidia, kuisaidia nchi kufikia malengo yake iliyokusudia. Hakuna hata nchi moja iliyokuwa bila kupata misaada ya Mataifa makubwa kama inaweza kuendelea. Kwa hiyo, nataka nikiri kwamba Mheshimiwa Waziri hotuba yako ni sahihi. Kwa kweli kwenye miaka ya 1980, 1985, 1990 na 1995 tulipata matatizo sana Zanzibar, hasa kwa sekta ya afya. Watoto wengi walifariki, wazazi walisumbuka sana. Mashule yetu yalikuwa katika kiwango cha chini sana kwa kuzuiwa misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwatake wenzetu viongozi wa vyama vya siasa, kwa sababu la Zanzibar kuzuiliwa misaada lilichangiwa zaidi na viongozi wa vyama vya siasa kwa ubinafsi wao zaidi. Tunapomaliza uchaguzi twendeni katika kupanga Serikali, kama hivi alivyosema kwamba tunazungumzia mustakabali wa Taifa letu. Kama ingekuwa mwaka 1995 walifikiria hivyo, sisi tusingepata tatizo lile. Kwa hivyo, nataka nithibitishe kwamba ni kweli Mheshimiwa Waziri hotuba yako ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai, hivi karibuni kupitia televisheni nimeona, *EU* wametoa bilioni 43 kusaidia ujenzi wa gati pale Zanzibar. Kwa hivyo, ni sahihi na vile vile barabara yetu kutoka Mkoani mpaka Chake Chake imejengwa kwa msaada wa Benki ya Dunia, shilingi bilioni 6.4 ambazo ni ahadi ambayo aliiweka Rais Benjamin Mkapa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2002 kwamba barabara ile kama itachaguliwa CCM wataijenga.

Kwa hiyo, inaonyesha hapa mafanikio makubwa. Kwa hiyo, ni vizuri wenzetu viongozi wa vyama vya siasa, kama tunakwenda kwenye uchaguzi, turudi katika kulipanga Taifa letu, si vizuri kulisaliti. Zanzibar ilisalitiwa na Wazanzibar wenyewe, wala asikudanganye mtu. Walitoka baadhi ya viongozi ndani ya Zanzibar kwenda kusaliti kuzuia misaada nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilithibitishe hili kwa wazi kabisa. Lingine ambalo nataka nilisemee ni kwamba ni kupambana na umaskini. Nataka nikuunge mkono Mheshimiwa Waziri. Lakini tusiseme tu, tufanye kazi katika kupambana na umaskini. Hakuna kitu kibaya katika maisha ya mwanadamu kama umaskini. Kwa hiyo, hapa tuelekeze nguvu zote za Serikali, wataalam wa sekta zote waende vijijini wakawasaidie wananchi kukwamua maisha yao ambayo kwa kweli yako duni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusizungumzie umaskini mjini, mjini hakuna maskini. Kila mmoja atakuwa na ujanja wa kuweza kufanya. Lakini kwa kweli vijijini kuna matatizo makubwa sana. Wataalam wetu wa kilimo, biashara na wataalam wetu wa kila aina, waende vijijini wakawasaidie wananchi kuondokana na matatizo haya ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuunga mkono, lakini kazi moja kubwa ya Serikali isiwe ya kusema. Ifanye kazi na tuone mabadiliko makubwa kwa faida ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Nasema Serikali ya Tanzania ilianzisha Mfuko

wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* kama moja ya mikakati yake ya kuondoa umaskini na kuchangia kufikiwa kwa malengo ya kuondoa umaskini uliobuniwa mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa dhati kabisa nataka nimpongeze aliyebuni Mfuko huu wa *TASAF.* Mwenyezi Mungu alimpa hekima kubwa sana na mfuko huu umeleta maendeleo makubwa katika Taifa letu la Tanzania na bahati nzuri katika sekta ambayo mfuko huu umefanya kazi ni sekta zote muhimu ambazo hata Mwenyezi Mungu yuko radhi nazo. Imesambaza maji maeneo makubwa. Binadamu bila maji hawezi kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yanatumika katika maeneo mbali mbali, hata katika masuala ya ibada, katika maisha ya watu yaani maji huwezi kusema kwamba labda siyo kitu muhimu katika maisha ya mwanadamu. Kwa hiyo, ni jambo la msingi. Lakini lingine katika shule bila ya elimu hakuna maendeleo. Mmejenga shule nyingi sana, lakini vile vile katika huduma za afya bila ya maisha ya watu, hatuwezi kufika tunakokwenda. Kwa hiyo, mimi nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, na nimtakie mafanikio makubwa kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa kweli aliyebuni mfuko huu wa *TASAF* akaweza kuu-*draft* mpaka ukafikia ulipofikia, kwa kweli Mwenyezi Mungu ambariki na atayakuta mengine mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie liko ukurasa wa 49 linaelezea kuhusu Sheria za Mazingira. Mheshimiwa Waziri nataka nikupongeze sana. Nataka niulize Sheria hizi za mazingira ziko vipi, je, zinakwenda nchi nzima na maeneo yote? Na kama zinaenda katika maeneo yote tunaambiwa kwamba watu wanaoshughulika na migodi ni sehemu kubwa kwamba migodi inasababisha uchafuzi wa mazingira katika nchi yetu. Je, hili Serikali inaliona vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizoko kwenye migodi ni hizi zilizoko kwenye hotuba yako au wale wa migodi wana sheria zao kuhusu suala la mazingira? Kwa hiyo, vile vile hili ningemtaka Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa mapana na marefu kabisa ili kuleta mafanikio makubwa katika kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huu wa 91 nataka nirudie alilolizungumzia kuhusu masuala ya Muungano. Anasema Serikali itaendelea kushughulikia masuala ya Muungano kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kero mbalimbali zilizoainishwa katika Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niulize kwanza, hebu hii Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo kuna nini na kama yako haya mambo ambayo yameorodheshwa, hivi kuna kasoro gani kwamba Serikali inashindwa kuweka wazi ili wananchi wakayajua, wakaweza kusaidia mawazo kwa Serikali. Kwa sababu mpaka leo wameshindwa wao kuyamaliza, ni vizuri kabisa tukaweka wazi, umma wa Tanzania wakajua, ili tuamue kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna budi, lazima tuulinde Muungano wetu kwa nguvu zetu zote. Tusiende kwa jazba tu na niwatake wale viongozi wa vyama vya siasa wasifanye jazba kutaka kuvunja Muungano kwa kuweka historia zao. Muungano wetu huu ni sahihi. Tuangalie wenzetu Wajerumani wamerudi katika kuungana. Lakini vile vile tuangalie mfano, sisi *East Africa* tunarudi katika kuanzisha Shirikisho la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri wasomi wa nchi hii wasione watu kama ni wajinga, kitu ambacho kimewekwa na waasisi wetu lazima tukienzi. Nikinukuu hotuba ya Rais Benjamin Mkapa, aliyoitoa Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2004 kuadhimisha miaka 40 ya Muungano wetu wa Tanzania alisema: "Muungano wetu umefikisha miaka 40 na upo imara. Nguvu yake ni Watanzania wenyewe, wengi wao asilimia 84.8 wakiwa hawajui uraia mwingine isipokuwa Utanzania. Watanzania hawa waliozaliwa mwaka 1964 na kuendelea, hawana uzoefu kuwa kitu kingine isipokuwa Watanzania, hawajui mfumo mwingine wa Muungano isipokuwa wa Serikali mbili."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jamani hakuna viongozi wengine wenye maneno ya hekima kama aliyo nayo Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa? *(Makofi)*

Kuna kasoro gani kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais? Kama mwaka 1964 tuliweka Muungano wetu ni wa Serikali mbili, wewe unataka kuweka Serikali tatu, wataka kuitoa wapi? Na tukiangalia vijana asilimia 84.8 wanajifahamu wao ni Watanzania tu. Tunataka kuwapeleka wapi? Ni vizuri kama Taifa, tukakaa, tukaondoa ubinafsi, tukaimarisha nchi yetu, tukaheshimu Katiba ya nchi na Sheria za nchi. *(Makofi)*

Nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais katika kipindi chake amesimamia Katiba yetu kwa uwazi kabisa bila kuogopa na nashukuru jana vijana wamemwita pale kwenda kuwafungulia mkutano na viongozi wa vyama vya siasa wapo. Huwezi ukawaambia wananchi kwamba nikishindwa uchaguzi watu walale barabarani, unawapeleka wapi wewe Profesa wa watu. *(Makofi)*

Lazima Katiba ya nchi na sheria zifuatwe. Tume ya uchaguzi imepewa uwezo kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, nina imani kwamba Serikali hii italiangalia. Lingine ambalo mimi nataka nilizungumze, kwa kweli mimi nataka nimpongeze Mheshimiwa KhalifaSuleiman Khalifa, leo asubuhi alipochangia hapa na amethubutu kusema kwamba hakuna anayeweza kuuvunja Muungano, nataka nimpongeze sana kwa sababu Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa muda mrefu ndio tuna wasi wasi nao, wanaleta mambo ya ajabu ajabu tu. Namshukuru sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifarijika sana kumsikia anatoa yeye kauli na kuna watu wanasema kwamba labda sehemu moja ya Muungano inaonewa Zanzibar, si kweli. Lakini vile vile kuna watu wanaichukulia nafasi hii kwamba Wapemba tunaonewa si kweli. Nafasi aliyo nayo Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ni mtu wa pili katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mpemba na amepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Mawaziri wake. *(Makofi)*

Sijui Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo anatokea wapi? Lakini kwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa tulipita tulipokwenda ziara Kigoma, Jimboni kwake, napajua na wanaishi kama Tanzania. Si vizuri kuwagawa tu kwa ubinafsi. Waasisi wetu wameondoka, wametuachia Taifa zuri kabisa. Mzee Abeid Karume na Mwalimu Julius Nyerere. Sasa leo wewe kwenye mwaka 2004 karne ya 21, 2005, karne ya 21 unataka kuleta historia gani.

Nikimkuu Mwalimu, anasema: "Wakubwa wanaungana, itakuwa sisi maskini. Tuondoe ubinafsi, tujenge umoja, tulete maendeleo kwa Taifa letu la Tanzania." Asilimia 84.8 sisi ni vijana hatujijui tunajua ni Watanzania na nataka nimpongeze Mheshimiwa Kepteni John Chiligati. Juzi alipokuwa akijibu swali la vitambulisho hawa wenzetu walishazungumza kwenye vitambulisho, labda litafikia kwenye mambo mengine. Lakini Mheshimiwa Chiligati akawaambia vile vitambulisho ni kwa ajili ya ukaazi, sio uraia. Uraia ni Utanzania hakuna raia wa Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hiyo, masuala kama haya ni vizuri tukayaweka wazi kwa faida ya Taifa hili na wenzetu warudi tuwe kitu kimoja kwa kuliendesha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache nawatakia mafanikio Waheshimiwa Mawaziri hawa, Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunakushukuruni sana. Mmemsaidia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Mimi ni Mpemba ninayezungumza, natokea Pemba, wala atakayesema kama Wapemba wanadharauliwa si kweli, ielezeni dunia ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika suala la kupambana na umaskini. Mchango wangu unalenga zaidi kwa wakulima wa zao la Korosho ambalo ni maarufu sana katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Dar es Salaam, na Tanga. Wakulima wa zao la korosho kama wangewezeshwa kimtaji wangeweza kuondokana na umaskini kutokana na hali nzuri ya bei ya zao hilo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bei ya sasa ya shilingi 700/= na kuendelea kwa kilo moja ya korosho ghafi ingewasaidia wakulima wengi kuondokana na umaskini kama kilimo chao cha korosho kingeboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa korosho wanachokihitaji ni mashamba yao kuweza kupaliliwa kwa wakati, hivyo kuhitajika matrekta yawe ya kumiliki wao wenyewe kwa wale wenye mashamba makubwa na ya kukodi kwa wale wenye mashamba madogo. Ni kawaida kwa wakulima wa korosho kuwa na mashamba yenye ukubwa wa ekari kumi na kuendelea hivyo kufikiria kuwa mashamba hayo yanaweza

yakapaliliwa kikamilifu kwa jembe la mkono haiwezekani. Ndiyo maana mashamba mengi hupaliliwa kwa moto hivyo kuathiri mikorosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa korosho vile vile wanahitaji mashine za kupulizia dawa ziwe za kumiliki wenyewe au za kukodi. Hali kadhalika wakulima wanahitaji madawa ya mikorosho ambayo bei zake sasa ni juu sana kwa wananchi wa kawaida kuzimudu.

Kwa hiyo, masuala kama haya ni vizuri tukayaweka wazi kwa faida ya Taifa hili na wenzetu warudi tuwe kitu kimoja kwa kuliendesha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache nawatakia mafanikio Waheshimiwa Mawaziri hawa, Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunakushukuruni sana. Mmemsaidia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Mimi ni Mpemba ninayezungumza, natokea Pemba, wala atakayesema kama Wapemba wanadharauliwa si kweli, ielezeni dunia ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika suala la kupambana na umaskini. Mchango wangu unalenga zaidi kwa wakulima wa zao la Korosho ambalo ni maarufu sana katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Dar es Salaam, na Tanga. Wakulima wa zao la korosho kama wangewezeshwa kimtaji wangeweza kuondokana na umaskini kutokana na hali nzuri ya bei ya zao hilo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bei ya sasa ya shilingi 700/= na kuendelea kwa kilo moja ya korosho ghafi ingewasaidia wakulima wengi kuondokana na umaskini kama kilimo chao cha korosho kingeboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa korosho wanachokihitaji ni mashamba yao kuweza kupaliliwa kwa wakati, hivyo kuhitajika matrekta yawe ya kumiliki wao wenyewe kwa wale wenye mashamba makubwa na ya kukodi kwa wale wenye mashamba madogo. Ni kawaida kwa wakulima wa korosho kuwa na mashamba yenye ukubwa wa ekari kumi na kuendelea hivyo kufikiria kuwa mashamba hayo yanaweza yakapaliliwa kikamilifu kwa jembe la mkono haiwezekani. Ndiyo maana mashamba mengi hupaliliwa kwa moto hivyo kuathiri mikorosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa korosho vile vile wanahitaji mashine za kupulizia dawa ziwe za kumiliki wenyewe au za kukodi. Hali kadhalika wakulima wanahitaji madawa ya mikorosho ambayo bei zake sasa ni juu sana kwa wananchi wa kawaida kuzimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji yote hayo yanahitaji mtaji wa kutosha na wananchi hawana kwa sasa. Hivyo naomba Serikali, kuwasaidia wakulima wa korosho kwa kuwapatia mitaji au mikopo kulingana na ukubwa wa mashamba waliyonayo. Mikopo hiyo inaweza ikawa ya zana, madawa, na fedha ili kulimo cha korosho kiweze kuboreshwa. Nina hakika kilimo cha korosho kikiboreka wakulima wake wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili waliopo katika Ofisi hii ya Makamu wa Rais wa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katibu Mkuu, Maafisa na Watendaji wote wa Ofisi hii kwa hotuba yao hii nzuri yenye kuimarisha Muungano wetu pamoja na Maendeleo ya Nchi yetu hii ya Tanzania. Ninaunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi hii kwa kweli ndiyo msingi na roho ya Muungano wetu wa Tanzania. Ofisi hii imefanya kazi kubwa, iliyo nzuri na sahihi katika kujenga na kuimarisha umoja wa wananchi wote wa nchi hii ya Tanzania. Muungano wetu wa mwaka 1964 umejenga heshima kubwa kwa nchi yetu na wananchi wa nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, inaelezea masuala ya Muungano wetu wa Tanzania. Tumeelezwa kuwa Muungano wetu umetimiza miaka 41 tangu kuundwa kwake. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutoka moyoni mwangu ninakiria ni kweli katika kipindi hiki cha miaka 41 kuna mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika nchi yetu. Tujitahidi kuondoa kasoro ndogo ndogo ambazo hujitokeza ili kunusuru kuyaharibu mafanikio haya yaliyopatikan na kutokana na Muungano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwa viongozi wote hapa nchini pamoja na wananchi wote tuondoe ubinafsi miongoni mwetu, tuzidishe kujenga na kuimarisha umoja wetu wa kitaifa. Tusiwaruhusu wale wote ambao hawapendi kuona kuwa Muungano wetu unaendelea kuwepo na unadumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaipongeza sana hotuba hii kwa kuelezea kumalizika kwa tatizo la Wafadhili kusitisha misaada kwa Zanzibar. Kwa kweli tatizo hili lilikuwa ni kubwa sana na kwa kweli liliathiri sana maendeleo yetu sis watu wa Zanzibar na Zanzibar kwa ujumla.

Pamoja na kwamba tatizo hili halikuanzishwa na wafadhili hao, liliandaliwa na ndugu zetu wanasiasa ambao pia walikuwa wenye asilia ya Zanzibar kwa hatua zao za kuwashawishi wafadhili hao kuzuia misaada kwa Zanzibar kitu ambacho kiliathiri, maisha ya watu na uchumi wa Zanzibar kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tatizo hili liliathiri sana katika Sekta za elimu, afya utumishi na uchumi wote wa Zanzibar. Mahospitali yetu mengi yalikosa huduma na madawa kitu ambacho kiliathiri sana maisha ya Mama Wajawazito na watoto kwa kweli tunawashukuru sana wafadhili wetu hawa pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondoka kwa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi yoyote ile hapa duniani ambayo inaweza kupata maendeleo ya kiuchumi na kisiasa bila ya kupata misaada na mashirikiano kutoka kwa nchi wafadhili na mashirika mengine mbalimbali ya Kimataifa .

Ninaitumia fursa hii kuwapongeza sana wafadhili hawa kwa kumaliza matatizo haya yaliyokuwepo Zanzibar, na pia ninawaomba wafadhili hawa wasichukue mamuzi makubwa kama haya ambayo waliwahi kuyachukua kwa Zanzibar kwa sababu na maslahi ya wanasiasa wachache. Uamuzi mkubwa kama huu unaathiri sana nchi na wananchi wa nchi hiyo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa ishirini na saba 27 inaelezea juu ya kupambana na na umaskini. Kwa kweli ninaipongeza sana Serikali yetu ya Muungano kwa kuweka mpango huu wa kupambana na umaskini katika nchi yetu na wananchi kwa ujumla. Ninaomba mipango yote iliyopangwa kuhusiana na mpango huu kuusimamia vizuri na kwa mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaipongeza sana Serikal yetu ya Muungano wa Tanzania kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu umefanya kazi nzuri katika maendeleo ya nchi yetu. Kwa kweli hatuna budi kumpongeza sana mbunifu na mwanzilishi wa Mfuko huu na ninamtakia kila la kheri, mafanikio mema, yenye upendo, maisha mazuri na salama hapa duniani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtakia kila la kheri mbunifu na mwanzilishi wa Mfuko huu kwa sababu amefanya kazi ambazo hata Mwenyezi Mungu Mwenyewe amezifurahia kama zitafanywa na kiumbe wake mwanadamu (binadamu). Kazi hizo kuweza kuwasaidia watu kupata maji ya kunywa na ya shughuli nyingine kama za ibada na matumizi ya kawaida majumbani na sehemu nyingine mbalimbali ambazo haziwezi kufanywa bila ya kupatikana au kuwepo maji.

Lingine ni suala zima la elimu. Elimu ni kitu cha msingi sana kwa mwanadamu yeyote yule. Mfuko huu umefanya mambo mbalimbali yanayohusiana na elimu. Pia huduma za afya na kadhalika. Naomba Serikali yetu awamu ya inayofuata ya *TASAF* inafanya kazi zake vizuri na kwa mafanikio makubwa kama yalivyo kusudiwa na kuangalia zile kasoro zilizotokea *TASAF* ya kwanza.

Mwisho ninaomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mfuko wake huu wa *TASAF*, awamu inayofuata na sisi vitongoji tupate fedha za *TASAF*.

Tuna tatizo kubwa la maji Gombani na Kibokoni. Pia vitongozi kujenga shule ya Sekondari .

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii, nitoe shukrani kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri ambayo imekuwa inatekeleza kwa nyanja zote zilizo chini ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimelazimika kutoa mchango wangu huu wa maandishi kuhusu suala la Muungano, ambalo kwa mawazo yangu naona halikupewa uzito unaostahili katika hotuba ya Waziri mhusika. Katika kitabu cha hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, suala la Muungano limetajwa katika ukurasa wa 91 (Ibara ya 99) kwa maelezo mafupi ambayo kwa kweli hayakidhi hoja kwa suala zito kama Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wepesi wa maelezo yaliyomo katika hotuba hii ni udhibitisho mwingine wa jinsi masuala haya ya Muungano yanavyochukuliwa *for granted* bila ya kuzama kwa kina yale masuala/kero zinazozungumzwa mara kwa mara na wadau wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi tu kutaja kuwa masuala ya kukuza uchumi na upunguzaji wa umaskini yatashughulikiwa. Baada ya zaidi ya miaka 40 ya Muungano wananchi wametaka kuona hatua thabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lako Tukufu kwa mfano zimetolewa rai ya masuala ya Muungano kuyaundia Wizara yake. Hapa suala siyo ukubwa wa Wizara kama Ofisi ya Makamu wa Rais. Hapa suala ni kuwa na Wizara ambayo itaratibu masuala yote ya Muungano kwa kina zaidi. Kero kama kuwepo sheria zinazogongana, mfumo wa kodi unaozikaba roho sehemu moja ya Muungano, mgao wa fedha za misaada hayana budi kupatiwa majibu ya uhakika yanayoridhisha pande zote mbili za Muungano badala ya masuala kama hayo kuyatolea maelezo mepesi mepesi ya kuondoa ugomvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshashuhudia mifano ya hatari kuyachukulia mambo *for granted* mfano mzuri ni ule uliotokea katika Umoja wa Nchi za Ulaya pale baadhi ya raia wa baadhi ya nchi walipokataa Katiba ya Umoja huo. Muungano wetu umeshapita huko. Lakini bado hatua za uhakika kuondoa kero za Muungano zisipuuzwe wakati upande mmoja wa Muungano unaonekana unapiga hatua kimaendeleo na mwingine unashindwa hata kulipa mishahara ya wafanyakazi wake wa Serikali kwa wakati kila mwezi, hali hiyo haiwezi kuitwa nzuri kwa Muungano wetu. Nimatumaini yangu kuwa katika awamu ijayo ya Serikali ya Muungano masuala yanayoleta kero yatashughulikiwa kwa udhati na uwazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nachukua fursa hii kukushukuru wewe na kwa kupitia kwako kumshukuru Spika kwa uongozi wenu mzuri katika kipindi hiki cha Bunge. Pia nawashukuru Wenyeviti waliowasaidia katika kazi zenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia natoa rambirambi zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao waliitwa na Mwenyezi Mungu wakati wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili pamoja na Maafisa wao kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Ofisi hii pamoja na hayo napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa *SELF* ujitangaze zaidi Unguja na Pemba ili wadau waujue na kuweza kunufaika nao.

(ii) Mradi wa *TASAF* awamu ya pili ujitahidi kumaliza viporo vilivyobakishwa katika awamu ya kwanza. Mfano katika Jimbo la Dimani kumalizia soko la dimani na barabara ya kuendea bandarini pamoja na kuvuta umeme.

Pili, katika hospitali ya Shakani – kujenga nyumba za madaktari na wauguzi pamoja na kuvuta umeme wa uhakika.

(iii) Mradi mpya wa MKURABITA ufike Zanzibar ili wananchi wa upande huu nao wafaidike na raslimali zao ambazo nyingi ni mfu sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo, napenda kusema naunga mkono huja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Waziri Arcado Ntagazwa Mbunge Waziri, Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo Mbunge, Katibu Mkuu ndugu Mollel na Mama Mushi, Wakuu wa Idara, Wakurugenzi *DAP*, Watendaji wote. Hongera kwa kazi nzuri Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano uliopo uimarike. Viongozi tulioko madarakani isiwe chanzo cha migogoro tuwe ndiyo wafumbuzi na hamasa kwa wananchi, Kuelewa Muungano Makamu wa Rais awe na Ofisi Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF*. Miradi ambayo haijakamilika ifuatiliwe pengine fedha zimeliwa na wajanja hasa mradi wa maji Kidugalo unasua sua naomba maelezo. *TASAF* Wilaya hawako makini naomba wapigiwe simu 023- 3183 *DED* Morogoro upate maelezo.

Idara hii inayoshughulikia mazingira kuleta sheria za mazingira, kuweka vyombo vya uthibiti, kuratibu shughuli za *NGO* za mazingira, kuweka utaratibu wa kutembelea maeneo yenye matatizo na kuwa pamoja kama timu kuhudumia umma wa Tanzania.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuza swali je, Watanzania tuko tayari kuendeleza mazingira yetu?

(b) Je, Muungano wetu hivi sasa unaridhisha?

(c) Je, baada ya sheria hii mpya *NEMC* imepewa meno kiasi gani ili isimamie vizuri?

(d) Je, *NEMC* imepewa fedha ya kutosha kukamilisha malengo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara ya mazingira iimarishwe kuwapa nyenzo, fedha na magari kutembelea nchi ili kutoa Elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Tanzania ina Serikali 2 tu mchango na matumizi ya fedha yao. Muungano Tanzania na Zanzibar ipo ila Zanzibar ipo kama Serikali ya Zanzibar. Ugomvi uko wapi tume iliyoundwa. Ofisi ya Makamu wa Rais wote kupitia kwa Katibu Mkuu karibuni Dodoma kuungana nasi hapa Bungeni. Nawatakia kila la kheri kukubaliwa Bajeti yenu mkafanye kazi ya taifa, pongezi nyingi sana kwa kusimamia sekta zinazowahusu. Baada ya pongezi hizi Dodoma muondoke na kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya kuendeleza nchi yetu.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na manung'uniko kutoka pande zote mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba kuna kasoro kadhaa ambazo hadi leo hazijapatiwa ufumbuzi. Miongoni mwa kasoro hizo ni pamoja na kutokuwa na uwiano mzuri wa watendaji katika maofisi ya Wizara na Taasisi za Muungano. Ni wazi kuwa kuna idadi ndogo sana ya watendaji katika Ofisi hizo kutoka upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa kuelezwa ni kwa nini hadi leo kasoro hii haijashughulikiwa na hasa ukizingatia kuwa haina gharama yoyote na ni lini Serikali itakuwa tayari kuweka urari ulio mzuri wa kuajiri watendaji katika Ofisi na Taasisi za Muungano ili kuondoa manung'uniko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa Ofisi ya Makamu ya Rais kule Zanzibar haijajengwa pamoja na kwamba kiwanja kimeshapatikana na fedha zimeshatengwa. Je, Mheshimiwa Waziri anatueleza nini kuhusu ucheleweshaji huu na ni lini ujenzi huu utaanza na unatarajiwa kumalizika lini?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Ingawa Ofisi yako inajihusisha na mambo ya Muungano. Mbona Wizara

yako inaachia kutolizungumzia wala kufuatilia matatizo ya kero za Muungano yatageuka kuwa maudhi ya Muungano baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara yako isiogope kuyazungumza mambo ya Muungano kwa uwazi. Niwapongezi Mawaziri wote kwa kazi zenu. Naomba miradi ya *TASAF*/MKUKUTA/MKURABITA ihimizwe ifikie Wilayani mapema sana. Kila la kheri na baraka.

**MHE. YUSSUF KOMBO JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pole kwa misiba yote iliyotokea hapa Bungeni. Naomba kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Sehemu ya *TASAF*, naipongeza Ofisi hii kwa kuweza kuutekeleza mradi huu kwa vizuri nchi nzima. Kwani hata jimbo langu la Kwamtipura nalo limefaidika. Kwa ujenzi wa kituo cha afya na kuifanya Kwamtipura kwani miongoni mwa Majimbo yaliofanya vizuri kwenye miradi ya *TASAF*.

Sasa kwa heshima kubwa nimetumwa na wanajimbo niombe tena *TASAF*, awamu ya pili (II) ije tena ili tuweze kujenga mtaro wa kupitisha maji ya mvua, kwani Jimbo la Kwamtipura linazungukwa na vijito vidogo vidogo hivyo husababisha uharibifu ukubwa wakati wa mvua kubwa au ndogo zinapokuja.

Naomba sana *TASAF II* ikianza ije tena Kwamtipura ili iweze kunusuru watu wa Jimbo hilo. Pili naipongeza Serikali kwa kujitahidi kuandaa kero za Muungano kwa kushughulikia mambo mengi kidogo. Je, vipi kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na nyumba ya Makamu huyo? Naomba suala hilo nalo lipewe umuhimu wa kutosha.

Mwisho naipongeza hotuba hii na naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri na yenye kutegemewa sana kwa uhai wa maendeleo ya wananchi.

Kwanza, ili tufanikiwe kupata maendeleo ya kweli na haraka ni lazima Ofisi ifanye ufuatiliaji kwa karibu katika Vijiji ili matumizi ya fedha za *TASAF* zitumike kwa lengo la kufanikisha kazi, hasa matumizi yote ya *TASAF* na *SELF* yaambatanishwe na muhtasari ya maamuzi ya vikao vya wanavijiji wote. Aidha ihakikishe kuwa hoja zote zinazotolewa na wananchi kuhusu matumizi zichambuliwe na kuzingatiwa bila kujali itikadi.

Pili, kwa kuwa makaa ya mawe ya Kiwira yapo Wizara na Ofisi hii ifanye maandalizi ya kuwaelimisha wananchi na watendaji wa majiko yake ili makaa hayo yatumike badala ya mkaa wa miti ambao unasababisha mazingira kuharibika kwa ukataji miti ovyo.

Pia, kuwepo na ulazima wa kila ajengaye nyumba mahali alazimike kupanda miti kadhaa kuzunguka jengo lake na iwe hivyo kwa kila mtu Vijijini kila mmoja apande miti

ya kuni katika eneo lake. Hili litapunguza akina mama kusafiri mwendo mrefu kufuata kuni porini na kuweza kufanya kazi zenye tija kwa maendeleo ya familia.

Tatu, ili kufanikisha MKUKUTA inabidi itungwe sheria ya kila kijana na mwanakijiji awe na hati miliki ya kimila ili aweze kulitumia eneo hilo kwa uzalishaji. Ipo hatari baadaye ardhi itakapopata wamiliki na kwisha wale watakaokosa bado watakuwa ni tatizo kitaifa. Kwa msingi huu hatutaweza kudhibiti vijana kukimbilia Mijini na kuzidisha uzururaji. Aidha tunahitaji kufikiria tena kuirudisha sheria ya nguvu kazi ili kila mwananchi ahusike kuzalisha mali na kupambana na umaskini.

Nne, kila *NGO*, iwe na utaratibu wa kutoa taarifa katika vikao vya Halmashauri na kamati za *RCC*. Vile vile kazi zao zikaguliwe na kamati ya mipango ya Wilaya ili kuwa na usimamizi wa kudumu pamoja na tathimini zenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba maelekezo ya Mawaziri wahusika.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa shukrani kwa kupata nafasi hii ya kutoa angalau mchango wangu mdogo katika Wizara hii. Lakini awali ya yote natoa pongezi zangu za dhati kwa kuteuliwa kuwa mgombea urais kwa tiketi ya CCM Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa mgombea Mwenza. Aidha nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa Mgombea Urais wa Zanzibar. Nawatakia kila la kheri na ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pole zangu za dhati kwa kuondokewa na Waheshimiwa Wabunge, wenzetu Mheshimiwa Ahmed Diria, Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Margareth Bwana. Mungu azilaze mahali pema peponi roho zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, iliyogusa mahali pote katika Muungano wetu. Aidha ni hotuba nzuri iliyoonesha mafanikio makubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye sekta ya mazingira. Pamoja na juhudi kubwa inayochukuliwa katika suala zima la kuhifadhi mazingira lakini bado kunatakiwa jitihada zaidi kuchuliwa. Suala la miti bado bado inakatwa ovyo na ili juhudi ya kata mti panda mti imeachwa na sasa hali inakuwa mbaya na kukabiliwa na jangwa katika baadhi ya Mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchimbaji wa michanga kwa matumizi ya ujenzi, uchimbaji, umekuwa ovyo mno na kusababisha kuacha maandaki makubwa na kuharibu mandhari ya ardhi yetu, nadhani lazima kuwepo mpango mzuri wa kupandwa miti maendeleo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala umwagaji mafuta machafu na mataka baharini (*pollution*) bado meli kubwa za Kimataifa bado zinaendelea kuchafua mwambao wa

bahari yetu ya Hindi, yaani *Indian Ocean*. Kuna haja kubwa ya kuwa na vyombo vya ulinzi vya kisasa ili kuweza kudhibiti hali hiyo aidha kuzipata fidia za Kimataifa ambazo tuliridhia hapa Bungeni. Suala la *TASAF*.

Nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha hizo za msaada wa Tanzania kwa kutupatia fedha hizo ya msaada wa kupunguza umaskini.

Juhudi kubwa ya mafanikio imepatikana lakini naomba zaidi isogezwe kule Zanzibar hasa katika jimbo langu la Bumbwini kwani bado *TASAF* haijaimarishwa ipasavyo na ni sehemu ambayo bado ina umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zetu viongozi wetu na msaada wa Serikali Kuu lakini tunakiri sehemu kubwa ya kuondoa umaskini ni kuboresha viwanda vyetu, kilimo bora cha kisasa, uvuvi wa kisasa wenye vyombo vya kisasa na utaalam bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea tena kukupongeza wewe Waziri na watendaji wako wote kwa kazi nzuri. Aidha kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini tunaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ninaomba wakubaliwe Bajeti hii. Ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza sana kwa hotuba nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako, pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa kuna uchafuzi mkubwa sana wa mazingira katika miji yetu hasa utupaji takataka na umwagaji maji machafu ovyo na kwa kuwa chanzo kikubwa cha magonjwa ya kuambukiza ni uchafu. Je, Serikali imeweka mikakati gani kudhibiti hali hiyo na je, sheria zilizopo kwa nini zisitekelezwe au kusimamiwa ili kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo na Arcado D. Ntagazwa kwa hotuba yao nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imewasilishwa hapa Bungeni asubuhi ya leo. Tumeona waziwazi namna Ofisi ya Makamu wa Rais ilivyojitahidi kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, hongereni sana.

Kipekee naomba nichukue fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kuhusu andiko ambalo nilimkabidhi ili aone namna ya kulisaidia jimbo langu katika mradi wa kupanda miti katika *catchment areas* za maji na kuhifadhi mazingira kwa ujumla. Bado tuna matumaini kuwa ombi hilo litatekelezwa kama Mheshimiwa Ntagazwa alivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitowe shukrani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kuwepo kwenye Bunge hili Tukufu mpaka leo hii tukiwa wazima na afya nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nipongeze Wizara hii kwa hotuba yake nzuri na imechambuliwa kwa urefu na fasaha kubwa sana na imegusa nyanja zote au pembe zote za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa jinsi wanavyoendesha Wizara hii kwa mpangilio mzuri sana. Nawaombea dua Mungu awape maisha marefu na waendelee na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naupongeza mradi huu wa *TASAF* umetusaidia sana kuondoa kero nyingi majimboni mwetu tunashukuru sana. Lakini mimi ningeshauri Serikali au mradi huu wa *TASAF* ili utakapoanza mara nyingi basi waangalie sana vile vijiji ambavyo bado havijafaidika na mradi huu, basi vipewe kipaumbele zaidi ili na wao wafaidike na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili na Ofisi ya Makamo wa Rais Zanzibar hili limekuwa ni kero ya muda mrefu sana kila mwaka mazungumzo ni haya haya kwa kweli hiki kilio kikubwa ningeshauri Serikali ilitupie macho jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naipongeza Serikali kwa kuunda hicho chombo cha usalama wa Taifa ambacho kinasimama pande zote za Muungano hili napongeza sana Serikali kwa sababu naamini kitatuwezesha kufanya kazi zetu vizuri za kimuungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwanzo kwamba bajeti hii ni nzuri na imegusa maeneo yote mimi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii ya kuwashukuru Mawaziri wote wanaoshughulikia Ofisi hii kwa kazi nzuri wanazofanya. Pia ninampongeza Katibu Mkuu, maafisa mbalimbali wa ofisi hii kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pamoja na kazi nyingi zinazofanyika ninaomba yafuatiliwe mambo yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa wananchi wameamua kujenga banda la shule huko Kijiji cha Chokocho katika Jimbo la Mkanyageni na banda jingine katika Shule ya Mkanyageni, Michenzani na kwa vile tumejitahidi kuchangia nguvu na fedha taslimu, nguvu na fedha hizo inazidi asilimia 20% kwa juhudi hizo ambazo tumezichukua ninaomba Ofisi ya Makamu wa Rais itusaidie.

(b) Kuondoa umaskini, ili umaskini uondoke ninashauri Serikali ipunguze bei ya mbolea kwa sababu maskini wengi wanategemea kilimo, wakulima wengi wanalima bila kutumia mbolea. Hivyo Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Kilimo na Chakula, ili bei ya

mbolea ipungue ili wananchi walime maeneo machache lakini wavune mazao mengi hapo ndipo umaskini unaweza ukapungua.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wahamasishwe wajiunge na vikundi vya ushirika ili mfuko wa *TASAF* uelekeze nguvu zake katika vikundi vya ushirika.

(d) Mfuko wa *TASAF* uliopeleka maji Kijiji cha Makoongwe Wilaya ya Mkoani. Umesababisha kukosa maji kwa maeneo yaliyopangiwa kupata maji hapo zamani katika Vijiji vya Chokocho, Mkanyageni, Michenzani na Kisiwa Panza. Mfuko wa *TASAF* ungejenga kisima huko Makoongwe baada ya kuvuta maji kutoka Jimbo la Mkanyageni, ninakumbusha tu kuwa Makoongwe si jimbo la Mkanyageni. Hivyo naomba *TASAF* waangalie tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia (100%)

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitaungana na wenzangu kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais ikiongozwa na Waziri Arcado Ntagazwa anayeshughulikia mambo ya mazingira na mambo ya Muungano na Mheshimiwa Edger Maokola-Majogo, anayehusika na mambo ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawapongeza Mawaziri hao kwa kazi nzuri wanyoifanya katika kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu umeimarika vizuri sana na uko imara sana. Baadhi ya kero za Muungano pia zimepungua na baadhi ya mambo yaliyokuwa sugu ni ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Bunge, iliyojengwa sehemu ya Tunguu nje kiasi cha maili 11 kutoka mjini Unguja. Hivi sasa kwa upande wa Ofisi ya Bunge Zanzibar linatumika jengo la kurithi ambalo lipo Mwanakwerekwere mjini Zanzibar. Lakini baada si muda mrefu jengo jipya litatumika. Vile vile Jengo la Tawi la *BOT* Zanzibar ni jengo la kukodiwa, lakini hivi sasa Tawi la *BOT* linajengwa na jengo hilo liko mbioni kumalizika, pia kuwa suala la mgawanyo wa fedha au Tume ya Pamoja na Fedha pia inatekeleza mgawanyo wa fedha 4.5 kama ilivyokubaliwa. Kwa hayo, machache lakini yako mengi tu yanaoneshwa wazi kuwa Muungano wetu unaimarika. Tunaomba na mengine yaliyobaki vilevile yatatuliwe kwa faida ya Jamhuri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuoondoa umaskini. *TASAF* kazi iliyofanya hatuna budi kuishukuru. Lakini tukitaja *TASAF* kwanza tumkumbuke Rais Benjamini William Mkapa kwani ndiye aliyoileta Tanzania na imeenea Tanzania nzima. *TASAF* imeleta maendeleo makubwa na umaskini umeondoka kwa asilimia kubwa. Sasa *TASAF* inaondoka na kuja MKUKUTA. Tunaomba MKUKUTA nayo ifanye kazi kubwa zaidi ya *TASAF* kwa kipindi kifupi tu, ili umaskini uondoke.

Vile vile hivi sasa pia umeanzishwa mradi wa *SELF* nao umeanza kupata mafanikio ya kupunguza umaskini kutokana na mikopo inayotolewa kwa wananchi. Wananchi wengi waliopata mikopo wamedhihirika kuwa kipato chao imeongezeka

kutokana na biashara mbalimbali wanazofanya kutokana na mikopo hiyo. Pia tatizo la ajira linapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza na mimi naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri Mheshimiwa Dr. Edgar D. Maokola-Mjogo, Mbunge na Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa, Mbunge Waziri wa Nchi Mazingira na Muungano, kwa hotuba nzuri iliyochambua kwa kina sana utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2004/2005 na mipango ya uhakika ya 2005/2006 na njia mbalimbali za utekelezaji wake. Kutokana na hali hii mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe naunga mkono hotuba asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini ili uweze kufanikiwa ipasavyo Serikali inatakiwa ifanye yafuatayo:-

(a) Umaskini uliokidhiri uko vijijini, kutokana na hali hii ngumu vijana wengi wanahamia mijini kukimbia ugumu wa maisha. Hivyo Serikali inatakiwa kuboresha maisha ya vijijini ili vijana waweze kukbaki huko. Hatua mbalimbali zichukuliwe za kuboresha miundombinu ikiwemo, barabara, umeme, maji na huduma za afya ziwe za uhakika.

(b) Serikali iwekeze zaidi kwa wakulima ili kumwezesha mkulima kuzalisha kwa wingi kwa kutumia nguvu kidogo. Hali hii itawavutia vijana kubaki vijijini na kujiajiri katika kilimo na biashara ndogo ndogo.

(c) Sehemu kubwa ya mikopo ielekezwe vijijini kwa wakulima, wafanyabiashara na wavuvi wadogo wadogo ili wapate uwezo wa kuzalisha na hatua hii itasaidia kuinua mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama maisha ya wananchi vijijini yakiboreka muda wao mwingi watatumia kwa kuzalisha mali badala ya kutumia muda mwingi kufuata huduma mbalimbali kama maji, elimu au huduma ya afya. Haya yakifanyika uchumi wa nchi hii unaweza kukuwa kwa kiwango kikubwa pengine kufikia zaidi ya asilimia 10 badala ya kukua kwa pato letu la Taifa kwa asilimia 6 ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu tukufu mara zote inaelekeza mipango yote ya maendeleo katika Maziwa mawili tu badala ya maziwa matatu, Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kwa mfano mpango wa kuwakopesha wavuvi wadogo wadogo, mpango wa kuhifadhi mazingira ya maziwa yote hayo yanaelekezwa Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika na si Ziwa Nyasa. Wananchi wa Tanzania wanaoishi kuzunguka Ziwa Nyasa waelewe nini juu ya hali hiyo?

Mwisho wa tatizo hili litadumu mpaka lini na mwisho wake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono tena hoja asilimia mia kwa mia.

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Wizara hii muhimu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kutaka kuwaunga mkono Mawaziri wetu wawili hawa kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa Taifa letu hili na kudumisha Muungano wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uadilifu wake mkubwa na kuweza kuisimamia Ofisi hii kwa mafanikio makubwa ambayo yamethibitisha Muungano wetu wa Tanzania.

Lakini vile vile mafanikio ya Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, hayakuja tu, lakini pia ni uaminifu mkubwa, upendo mkubwa aliyoupata kwa Mawaziri hawa wawili. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri hawa pamoja na Watendaji wao kwa ushirikiano mkubwa yaliyomwezesha Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuanza kutekeleza majukumu yake ya Taifa kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi mkubwa Mheshimiwa Mwenyekiti, unaonyesha hata Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa haikufanya kipingamizi kuweza kumteua kwa kushirikiana na mgombea wetu wa Urais kwa kupitia CCM kumteua awe mgombea mwenza katika uchaguzi mkuu unaofuatia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mafanikio haya hayakuja tu. Laiti kama hakupata msaada mkubwa wa watendaji wa Mawaziri hawa kwa kweli asingelifikia hatua aliyofikia na kwa hapo nataka nitamke kwa wazi kwamba ninaunga mkono hotuba hii asilimia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nashukuru kwamba katika ukurasa wa tano ameelezea kuhusu Muungano na akasema Muungano wetu umetimiza miaka 41 tangu kuundwa. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri kwamba ni kweli mafanikio makubwa yamepatikana na tuombe wale Watanzania wenzetu ambao wanatumia sababu zao za ubinafsi zaidi, kusema labda Muungano wetu hauna faida yoyote. Kwa kweli wakae wafikiri na kwa kweli wawe wa kweli kwa umma wa Tanzania wathibitishe kwamba Muungano wetu una faida katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 41 si kidogo sana na tunafanya makosa tunapolinganisha Muungano wetu wa miaka 41 tukalinganisha na Muungano wa Amerika *(United States of America).* Wenzetu wapo tangu mwaka 1976, Tuangailie ni miaka mingapi wako katika dunia hii ndani ya Serikali zao hizi.

Kwa hiyo, ni vizuri Watanzania tukawa wa kweli, tusifanye haraka ya kukimbilia mbele wakati bado tunaanza kuondoka, sasa cha msingi tuimarishe umoja wetu, tuimarishe uadilifu wetu, tuimarishe mshikamano wetu, ili kujenga umoja wetu wa Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 8, ameeleza kwamba tatizo la wafadhili kusitisha misaada kwa Zanzibar limepata ufumbuzi na misaada hiyo kwa sasa inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nithibitishe ni sahihi kabisa hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kwa kweli tunashukuru sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ninaamini wafadhili hawakurudi tu, inawezekana ni juhudi kubwa ambayo Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeifanya. Kwa kweli Zanzibar tulipozuiwa misaada tulipata matatizo makubwa sana na hakuna nchi yoyote ambayo inaweza kuendelea bila kupata misaada ya wafadhili na nchi zile wahisani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada ndiyo inayosaidia, kuisaidia nchi kufikia malengo yake iliyokusudia. Hakuna hata nchi moja iliyokuwa bila kupata misaada ya Mataifa makubwa kama inaweza kuendelea. Kwa hiyo, nataka nikiri kwamba Mheshimiwa Waziri hotuba yako ni sahihi. Kwa kweli kwenye miaka ya 1980, 1985, 1990 na 1995 tulipata matatizo sana Zanzibar, hasa kwa sekta ya afya. Watoto wengi walifariki, wazazi walisumbuka sana. Mashule yetu yalikuwa katika kiwango cha chini sana kwa kuzuiwa misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwatake wenzetu viongozi wa vyama vya siasa, kwa sababu la Zanzibar kuzuiliwa misaada lilichangiwa zaidi na viongozi wa vyama vya siasa kwa ubinafsi wao zaidi. Tunapomaliza uchaguzi twendeni katika kupanga Serikali, kama hivi alivyosema kwamba tunazungumzia mustakabali wa Taifa letu. Kama ingekuwa mwaka 1995 walifikiria hivyo, sisi tusingepata tatizo lile. Kwa hivyo, nataka nithibitishe kwamba ni kweli Mheshimiwa Waziri hotuba yako ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai, hivi karibuni kupitia televisheni nimeona, *EU* wametoa bilioni 43 kusaidia ujenzi wa gati pale Zanzibar. Kwa hivyo, ni sahihi na vile vile barabara yetu kutoka Mkoani mpaka Chake Chake imejengwa kwa msaada wa Benki ya Dunia, shilingi bilioni 6.4 ambazo ni ahadi ambayo aliiweka Rais Benjamin Mkapa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2002 kwamba barabara ile kama itachaguliwa CCM wataijenga.

Kwa hiyo, inaonyesha hapa mafanikio makubwa. Kwa hiyo, ni vizuri wenzetu viongozi wa vyama vya siasa, kama tunakwenda kwenye uchaguzi, turudi katika kulipanga Taifa letu, si vizuri kulisaliti. Zanzibar ilisalitiwa na Wazanzibar wenyewe,

wala asikudanganye mtu. Walitoka baadhi ya viongozi ndani ya Zanzibar kwenda kusaliti kuzuia misaada nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilithibitishe hili kwa wazi kabisa. Lingine ambalo nataka nilisemee ni kwamba ni kupambana na umaskini. Nataka nikuunge mkono Mheshimiwa Waziri. Lakini tusiseme tu, tufanye kazi katika kupambana na umaskini. Hakuna kitu kibaya katika maisha ya mwanadamu kama umaskini. Kwa hiyo, hapa tuelekeze nguvu zote za Serikali, wataalam wa sekta zote waende vijijini wakawasaidie wananchi kukwamua maisha yao ambayo kwa kweli yako duni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusizungumzie umaskini mjini, mjini hakuna maskini. Kila mmoja atakuwa na ujanja wa kuweza kufanya. Lakini kwa kweli vijijini kuna matatizo makubwa sana. Wataalam wetu wa kilimo, biashara na wataalam wetu wa kila aina, waende vijijini wakawasaidie wananchi kuondokana na matatizo haya ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuunga mkono, lakini kazi moja kubwa ya Serikali isiwe ya kusema. Ifanye kazi na tuone mabadiliko makubwa kwa faida ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF).* Nasema Serikali ya Tanzania ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF),* kama moja ya mikakati yake ya kuondoa umaskini na kuchangia kufikiwa kwa malengo ya kuondoa umaskini uliobuniwa mwaka 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa dhati kabisa nataka nimpongeze aliyebuni Mfuko huu wa *TASAF.* Mwenyezi Mungu alimpa hekima kubwa sana na mfuko huu umeleta maendeleo makubwa katika Taifa letu la Tanzania na bahati nzuri katika sekta ambayo mfuko huu umefanya kazi ni sekta zote muhimu ambazo hata Mwenyezi Mungu yuko radhi nazo. Imesambaza maji maeneo makubwa. Binadamu bila maji hawezi kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yanatumika katika maeneo mbali mbali, hata katika masuala ya ibada, katika maisha ya watu yaani maji huwezi kusema kwamba labda siyo kitu muhimu katika maisha ya mwanadamu. Kwa hiyo, ni jambo la msingi. Lakini lingine katika shule bila ya elimu hakuna maendeleo. Mmejenga shule nyingi sana, lakini vile vile katika huduma za afya bila ya maisha ya watu, hatuwezi kufika tunakokwenda. Kwa hiyo, mimi nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, na nimtakie mafanikio makubwa kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa kweli aliyebuni mfuko huu wa *TASAF* akaweza kuu-*draft* mpaka ukafikia ulipofikia, kwa kweli Mwenyezi Mungu ambariki na atayakuta mengine mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie liko ukurasa wa 49 linaelezea kuhusu Sheria za Mazingira. Mheshimiwa Waziri nataka nikupongeze sana. Nataka niulize Sheria hizi za mazingira ziko vipi, je, zinakwenda nchi nzima na maeneo yote? Na kama zinaenda katika maeneo yote tunaambiwa kwamba watu

wanaoshughulika na migodi ni sehemu kubwa kwamba migodi inasababisha uchafuzi wa mazingira katika nchi yetu. Je, hili Serikali inaliona vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizoko kwenye migodi ni hizi zilizoko kwenye hotuba yako au wale wa migodi wana sheria zao kuhusu suala la mazingira? Kwa hiyo, vile vile hili ningemtaka Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa mapana na marefu kabisa ili kuleta mafanikio makubwa katika kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huu wa 91 nataka nirudie alilolizungumzia kuhusu masuala ya Muungano. Anasema Serikali itaendelea kushughulikia masuala ya Muungano kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kero mbalimbali zilizoainishwa katika Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niulize kwanza, hebu hii Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo kuna nini na kama yako haya mambo ambayo yameorodheshwa, hivi kuna kasoro gani kwamba Serikali inashindwa kuweka wazi ili wananchi wakayajua, wakaweza kusaidia mawazo kwa Serikali. Kwa sababu mpaka leo wameshindwa wao kuyamaliza, ni vizuri kabisa tukaweka wazi, umma wa Tanzania wakajua, ili tuamue kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna budi, lazima tuulinde Muungano wetu kwa nguvu zetu zote. Tusiende kwa jazba tu na niwatake wale viongozi wa vyama vya siasa wasifanye jazba kutaka kuvunja Muungano kwa kuweka historia zao. Muungano wetu huu ni sahihi. Tuangalie wenzetu Wajerumani wamerudi katika kuungana. Lakini vile vile tuangalie mfano, sisi *East Africa* tunarudi katika kuanzisha Shirikisho la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri wasomi wa nchi hii wasione watu kama ni wajinga, kitu ambacho kimewekwa na waasisi wetu lazima tukienzi. Nikinukuu hotuba ya Rais Benjamin Mkapa, aliyoitoa Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2004 kuadhimisha miaka 40 ya Muungano wetu wa Tanzania alisema: "Muungano wetu umefikisha miaka 40 na upo imara. Nguvu yake ni Watanzania wenyewe, wengi wao asilimia 84.8 wakiwa hawajui uraia mwingine isipokuwa Utanzania. Watanzania hawa waliozaliwa mwaka 1964 na kuendelea, hawana uzoefu kuwa kitu kingine isipokuwa Watanzania, hawajui mfumo mwingine wa Muungano isipokuwa wa Serikali mbili."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jamani hakuna viongozi wengine wenye maneno ya hekima kama aliyo nayo Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa? *(Makofi)*

Kuna kasoro gani kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais? Kama mwaka 1964 tuliweka Muungano wetu ni wa Serikali mbili, wewe unataka kuweka Serikali tatu, wataka kuitoa wapi? Na tukiangalia vijana asilimia 84.8 wanajifahamu wao ni Watanzania tu. Tunataka kuwapeleka wapi? Ni vizuri kama Taifa, tukakaa, tukaondoa ubinafsi, tukaimarisha nchi yetu, tukaheshimu Katiba ya nchi na Sheria za nchi. *(Makofi)*

Nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais katika kipindi chake amesimamia Katiba yetu kwa uwazi kabisa bila kuogopa na nashukuru jana vijana wamemwita pale

kwenda kuwafungulia mkutano na viongozi wa vyama vya siasa wapo. Huwezi ukawaambia wananchi kwamba nikishindwa uchaguzi watu walale barabarani, unawapeleka wapi wewe Profesa wa watu. *(Makofi)*

Lazima Katiba ya nchi na sheria zifuatwe. Tume ya uchaguzi imepewa uwezo kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, nina imani kwamba Serikali hii italiangalia. Lingine ambalo mimi nataka nilizungumze, kwa kweli mimi nataka nimpongeze Mheshimiwa KhalifaSuleiman Khalifa, leo asubuhi alipochangia hapa na amethubutu kusema kwamba hakuna anayeweza kuuvunja Muungano, nataka nimpongeze sana kwa sababu Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa muda mrefu ndio tuna wasi wasi nao, wanaleta mambo ya ajabu ajabu tu. Namshukuru sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifarijika sana kumsikia anatoa yeye kauli na kuna watu wanasema kwamba labda sehemu moja ya Muungano inaonewa Zanzibar, si kweli. Lakini vile vile kuna watu wanaichukulia nafasi hii kwamba Wapemba tunaonewa si kweli. Nafasi aliyo nayo Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ni mtu wa pili katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mpemba na amepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Mawaziri wake. *(Makofi)*

Sijui Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo anatokea wapi? Lakini kwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa tulipita tulipokwenda ziara Kigoma, Jimboni kwake, napajua na wanaishi kama Tanzania. Si vizuri kuwagawa tu kwa ubinafsi. Waasisi wetu wameondoka, wametuachia Taifa zuri kabisa. Mzee Abeid Karume na Mwalimu Julius Nyerere. Sasa leo wewe kwenye mwaka 2004 karne ya 21, 2005, karne ya 21 unataka kuleta historia gani.

Nikimkuu Mwalimu, anasema: “Wakubwa wanaungana, itakuwa sisi maskini. Tuondoe ubinafsi, tujenge umoja, tulete maendeleo kwa Taifa letu la Tanzania.” Asilimia 84.8 sisi ni vijana hatujijui tunajua ni Watanzania na nataka nimpongeze Mheshimiwa Kepteni John Chiligati. Juzi alipokuwa akijibu swali la vitambulisho hawa wenzetu walishazungumza kwenye vitambulisho, labda litafikia kwenye mambo mengine. Lakini Mheshimiwa Chiligati akawaambia vile vitambulisho ni kwa ajili ya ukaazi, sio uraia. Uraia ni Utanzania hakuna raia wa Zanzibar. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ambayo ni ya ubia na mtoa hoja. Nawapongeza wote ambao wamezungumza katika kikao hiki ambacho ni cha mwisho na pia Mawaziri wote ambao wamenitangulia kutoa hoja mbele yetu. Naungana na kama alivyosema Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, asubuhi kuhusu kutoa rambirambi kwa wale Wabunge wenzetu ambao wamepoteza maisha katika kipindi hiki. Mungu azilaze pema roho za marehemu, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitatenda haki sitarudia hapa kusema ili iingie kwenye *Hansard* kwamba ndugu yangu, Waziri mwenzangu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa tarehe 5 Desemba, 2004 alifiwa na mke wake, Mama July Thomas Halie Ntagazwa. Tunawashukuru wote ambao walimpa pole wakati ule na tunaendelea kuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake marehemu mahala pema Peponi. *Amin.*

Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuteuliwa kugombea nafasi ya Urais kupitia CCM. Pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais kwa kuwa mgombea mwenza na nampongeza Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuteuliwa kugombea Urais Zanzibar. Wote

nawatakia mafanikio na mimi kama mwana CCM lazima niseme wazi kwamba ninaotaka washinde ni hawa.

Katika wosia wangu nitakaoutoa mwishoni leo kwa wapiga kura wangu, wosia wangu mmoja ni kwamba mchagueni Jakaya Kikwete kwa kumpa kura zote, mchagueni Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kumchagua Jakaya Kikwete kwa sababu tiketi yao ni moja na wale wa Zanzibar wamchague Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watatuvusha, watatupeleka mbele zaidi na mimi nina imani kwa sababu wote nawafahamu, watatuvusha. Mheshimiwa Jakaya Kikwete nimefanya naye kazi muda mrefu na aliwahi kuwa Katibu wangu wa Wilaya. Ni mtu makini sana na ni mcheshi. Ila ucheshi wake wakati mwingine unaweza kukupumbaza wewe. Kwa sababu ni mcheshi. Mtu mcheshi huwezi ukaelewa amekasirika saa ngapi, na kwa nini. Na yeye huwezi kumkuta hata siku moja amekasirika. Kwa vyovyote nataka kuwahakikishieni ni mfanyakazi makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio ya kufikiria kwamba atafanya mambo namna gani, maana yake unajua, hasa watu wengine, si yeye mwenyewe, magazeti yanaandika sana. Watu wanasema mtu fulani fulani wamesema, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, akiingia Ikulu mimi nitapata cheo hiki. Kila mtu ana cheo. Loo! Tufanye kazi ya kuhakikisha anapata Urais kwanza, siyo kutafuta vyeo saa hizi. *(Makofi)*

Mpaka mtu ujichagulie cheo leo, hakuna mtu wa kuwachuja hao watakaopewa vyeo. Tumsaidie ashinde urais kwanza na mengine atayafanya kama Katiba inavyomruhusu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, hotuba yangu Mwenyekiti, itakuwa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza nitajibu hoja. Sehemu ya pili, nitaliaga Bunge. Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mbunge wa Vitongoji, Pemba kuwa mimi naitwa Maokola-Majogo, Mbunge wa miaka 30 Bungeni. Natoka Jimbo la Nachingwea, Mkoa wa Lindi na ndiyo niliyemrithi Ubunge Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Mbunge wa Nachingwea tangu Uhuru. *(Makofi)*

Tuko wawili tu tangu Uhuru. Sasa wewe rafiki yangu Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, siku zote tunasalimiana, kumbe hujui ninakotoka. Loo! Kwa hiyo, nafikiri taarifa hiyo itakusaidia na mimi nakutakia kama ninavyotakia Wabunge wengine, ushindi katika uchaguzi ujao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la jumla, *TASAF* imebuniwa na Rais Benjamin Mkapa na ndiyo msimamizi mkuu wa mradi huu na kwa hiyo, sifa zote kwanza ziende kwa Mheshimiwa Benjamin Mkapa, maana ulikuwa unasema huyo aliyebuni apewe sifa zote. Mimi nataka iwekwe kwenye *Hansard* kuwa aliyebuni *TASAF* ni Rais Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya ujumla kwenye hotuba yake ambayo aliitoa wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya mfuko wa *TASAF* Rais alisema hivi na

nanukuu na vitabu hivi vimegaiwa kwa Wabunge wote: *"TASAF* haina miradi. Miradi ni ya wananchi. *TASAF* haileti maendeleo. Inawezesha tu wananchi kutekeleza vipaumbele vyao vya maendeleo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mradi huu ni sehemu ya mikakati ya kuondoa umaskini, ningependa pia nimnukuu Rais katika ukurasa wa 22 kuhusu umaskini. Nanukuu: "Baada ya miaka 43 ya Uhuru sasa nadhani tumeelewa, kunahitajika nini ili maendeleo yaje kwa kasi ya kutosha kupunguza na hatimaye kuondoa umaskini. Hatua ya kwanza ya maendeleo ni mtu kutoridhika na hali duni ya maisha yake. Ni kujenga tamaa ya maendeleo na wivu wa maendeleo na kuchukia hali ya umaskini."

Pili, hatua ya pili ni mtu kuamua kwa dhati kutafuta maendeleo kwa jasho lake na inapobidi kwa kushirikiana na wenzake wanaochukia umaskini kama yeye. Kwa hiyo, nilitaka kusema misingi ni kufanya kazi ndiyo utaondokana na umaskini. Utatekeleza MKUKUTA kwa kupeleka mbele ufanyaji kazi kwa bidii."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nakushukuru sana ukiwa Mwenyekiti wetu wa Sekta yetu ulipokuwa unachangia wakati wa Semina ya MKURABITA uliposisitiza kwamba Watanzania wasipoamua kufanya kazi kwa bidii basi sera zetu zote hazitakuwa na faida yoyote.

Sasa baada ya kusema hayo, pia ningependa nijibu hoja mbalimbali kwa kifupi, wakati wa majadiliano ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib na Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, wote walizungumzia juu ya umuhimu wa MKUKUTA kutengewa fedha za kutosha. Aidha, walizungumzia pia kwamba urasimu uliopo katika kuidhinisha miradi ya *TASAF* upunguzwe. *(Makofi)*

Pia Serikali itafute fedha ili miradi ya *TASAF* iliyokwama iweze kukamilishwa. Sasa hili la urasimu, kwa kawaida fedha zinatolewa kama hatua ya mwanzo imekwishatekelezwa. Kwa hiyo, ni muhimu kutoa taarifa na kama nitakavyojibu zaidi huko mbele kuhusiana na *TASAF II,* ile miradi ya nyuma ambayo haijakamilika inatakiwa Kamati zinazohusika zitoe tena maombi ambayo kwa sababu miradi ilikwishakubaliwa, itafikiriwa kwa ajili ya kuimaliza na sasa kwenye *TASAF II* tunaenda nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ali Said Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, anasema Tanzania haina mkakati wa kuondoa umaskini ila mkakati tunaoambiwa tumeletewa na washauri toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemkumbusha kwamba ameshiriki uandaaji wa MKUKUTA na wadau wengi wamehusishwa safari hii kuliko mkakati wa kwanza. Hii inaonyesha wazi kabisa kwamba Tanzania tumeanzisha mkakati wetu sisi wenyewe na ndiyo maana mataifa mbalimbali yanatusifu kwamba mikakati tunayotekeleza siyo ya kuletewa na watu wengine na ushahidi upo na kesho kutwa tunazindua MKUKUTA na

tumewagawia kitabu ambacho kinaelezea jambo hili. Tujivune kwa kuwa tumebuni MKUKUTA sisi wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa wafuatao pia walichangia kwa mfano, Mheshimiwa Ali Said Juma, nimekwishaeleza na Mheshimiwa Juma Mikidadi kuhusu *TASAF* na *SELF* katika kuleta maendeleo iwe makini. Kama nilivyosema hii ni miradi ambayo imebuniwa na wananchi wenyewe na ni washiriki wa *TASAF* katika kuleta miradi ya maendeleo. Yeye anasema kwa nini tunakwenda kwenye afya, elimu na kadhalika na tusiende kwenye kuwezesha wananchi wenyewe. Lakini usipokuwa na barabara huwezi kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa na shule huwezi kuelewa namna ya kufanya biashara. Kwa hiyo, haya mambo yanategemeana na pia *SELF* inalenga kutoa huduma ya mikopo midogo midogo kupitia asasi ambazo zina uwezo wa kutoa huduma hizo katika maeneo husika, ili kuzitambua asasi hizo vigezo vifuatavyo zinazingatiwa:-

Kwanza, uwezo wa *management* ya asasi husika, pili, namna asasi inavyotoa mikopo kwa kuzingatia kanuni bora za mikopo kama riba, tatu, upanuzi wa eneo na asasi inayotoa huduma, nne, uwezo wa kitaalam wa asasi katika fani ya utoaji mikopo pale penye mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SELF* pia inatoa mafunzo kwa asasi ili kuboresha utoaji wa huduma. Aidha, kuna ufuatiliaji wa karibu, kuangalia kama *SELF* inatoa huduma zinazotakiwa ili kurekebisha kasoro zilizopo. asasi zenyewe zinafanya tathmini ili kuona kuwa kama utendaji wao unaleta faida kwa asasi yenyewe na walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo yametolewa kwa walengwa ili watambue aina ya miradi inayoweza kuwaletea faida na uendeshaji na usimamizi wa miradi yao. Hatua hizi zote kwa miradi ya *TASAF* na *SELF* zinalenga kuhakikisha kuwa kuna maendeleo endelevu na kuwapa nguvu walengwa.

Aidha, Waheshimiwa wafuatao aidha kwa kuchangia kwa mdomo au kwa maandishi, kwa mfano Mheshimiwa Yusuf Kombo Juma, Mheshimiwa remidius Kissassi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Mheshimiwa John Singo, hao wote wametoa mapendekezo ya miradi kwa ajili ya kupata fedha kutoka *TASAF* katika awamu ya pili ya *TASAF* Vijiji vyote vitapata fursa sawa ya kupata msaada kutoka *TASAF* kwa kuzingatia maombi toka jamii husika.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge mnashauriwa kuhamasisha jamii husika kutoa mapendekezo ya miradi kwa kuzingatia mahitaji yao ya kipaumbele. Fedha zilizoombwa kwa ajili ya Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa Semindu Pawa, wote walisema utaratibu wa kukamilisha viporo vya awamu ya kwanza ya *TASAF* ufanye. Kama nilivyoeleza kwenye maelezo hayo kwamba walete tu, maelezo ya sehemu gani imebaki kupitia Kamati zao ambazo tulizieleza hapa kwenye Semina. Halafu fedha zitatengwa kwa ajili ya kumalizia miradi hiyo.

Mheshimiwa John Singo, anasema pamoja na jitihada za *SELF* kutoa mkopo wa shilingi milioni 75 kwa *Same Chamber of Commerce SACCOS. SACCOS* zingine bado hayajashughulikiwa. Maelezo yetu ni kwamba ni kweli *SELF* imetoa mkopo wa shilingi 75 milioni kwa chama cha akiba na mikopo cha *Same Chamber of Commerce* ambao hivi sasa wamebadilisha jina na kuitwa *Kaya SACCOS.* Mradi wa *SELF* unashirikiana na mradi wa *SFSP* ulioko chini ya Waziri Mkuu kuzipa uwezo na hatimaye mikopo. *SACCOS* ndogo ndogo zilizoko kwenye baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro ikiwemo Wilaya ya Same zimepata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kupitia mradi wa *SFSP* maombi yalipokelewa kutoka asasi 7, yaani *Same Teachers SACCOS, Mkombozi SACCOS, Kumekucha SACCOS, Kinduju SACCOS, Sengena SACCOS, Kisiwani SACCOS* na *Mwangaza SACCOS.* Mradi wa *SELF* umefanya tathmini ya maombi haya na kukuta mapungufu mbalimbali. Aidha, mapungufu yafuatayo yamebainika:-

(i) Vyama kutosajiliwa;
(ii) Kutowasilisha hesabu zilizokaguliwa;
(iii) Kutowasilisha wasifu wa viongozi; na
(iv) Kutowasilisha Katiba na taarifa nyingine kama riba inayotozwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *SELF* umewasiliana na *SACCOS* hizi ili ziwasilishe nyaraka na taarifa na hatimaye kukamilisha tathmini ya maombi na kutoa mikopo au kukataa maombi na kuwashauri kurekebisha mapungufu yaliyoonekana na kuleta maombi tena. Mpaka tarehe 20 Julai ni *Same Teachers SACCOS* pekee ilikuwa imewasilisha. Mradi bado unaendelea kuwasiliana na *SACCOS* zilizobaki ili ziwasilishe taarifa na nyaraka zinazotakiwa. Kwa hivyo, Mheshimiwa Mbunge maadam bado tuko hapa tutaendelea kuwasiliana na naweza nikakupa maelezo zaidi ili kusudi ukawashauri wahusika waweze kufaidika na mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama atakavyowataja waliochangia Waziri mwenzangu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwenye majumuisho haya ningependa na mimi niseme hapa kwamba hoja zilizo nyingi itabidi zifanyiwe kazi ili zituwezeshe kutekeleza miradi hii kwa ufanisi zaidi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu karibu wote wametupa pongezi kwa kazi nzuri tunazofanya pamoja na wataalamu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na mimi nazipokea pongezi hizo na kwa kweli kama mtu unagombea Ubunge katika hali ya namna hii tumekwishafagiliwa vya kutosha, tunawashukuruni sana. Mimi nasema haya yote tumepata nguvu ya kuyafanya kutokana na usimamizi mzuri wa Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiingereza wanasema ukishakabidhi kazi, usifanye wewe mwenyewe bali fuatilia *(don't delegate and do it yourself).* Makamu wa Rais sisi ametuachia kabisa kwa sababu ametuamini, kitendo cha kutuamini ninamshukuru mimi hapa Makamu wa Rais. Mara moja moja anatuita tunamweleza mambo yanayotokea lakini kwa ujumla tumeaminiwa tufanye kazi hiyo kwa niaba yake. Mimi pia namshukuru

yeye kwa uongozi mzuri na bila shaka kama walivyosema Wabunge wenzangu ndio iliyowezesha CCM kumfikiria kwamba aendelee na nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefaidika sana wakati wa ziara yake aliyoifanya Dubai, Singapore, Indonesia, *South Korea* pamoja na Japan mwezi Mei kwa sababu nilikuwa mjumbe katika msafara huo. Kila tulipokwenda ameielezea Tanzania vizuri Bara na Visiwani na amekutana na makampuni yote makubwa katika nchi hizo na kuwafanyia semina kuhusu umuhimu wa kuja Tanzania kuja kuwekeza. Kwa kweli tunaye kiongozi mwenye hazina kubwa na ushahidi ni safari kama hiyo ambayo watendaji mbalimbali katika Wizara mbalimbali wanafanyia kazi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo sasa naingia kwenye sehemu yangu ya tatu sababu dakika zilizobaki siyo nyingi ili niseme yafuatayo:-

Kwanza kabisa mimi kama Mbunge wa miaka 30 mfululizo Bungeni, nimejifunza mambo mengi sana hapa Bungeni. Wabunge lazima kuwatembelea wananchi, Wabunge lazima kuwasiliza wananchi na kuchukua shida zao, Wabunge lazima kuwaambia ukweli wananchi katika lile linalowezekana na lisilowezekana. Siyo kuwakwepa kwepa unasema ninajitahidi kumbe *solution* (ufumbuzi), ukifanya hivyo wananchi watakuthamini na watakuheshimu. Hayo ni baadhi ya mambo ambayo yamenisaidia mimi kukaa miaka 30 Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kunipa imani *(trust)* wakati aliponiteua kuwa Waziri wa Ulinzi na JKT mwaka 1995. Hicho ni kitendo cha kuaminiwa, Rais mpya anamteuwa Waziri wa Ulinzi mpya na hapo nyuma nilikuwa Naibu Waziri 1995 - 2000 nikawa Waziri wa Ulinzi. Mwenzangu Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi ameendelea miaka mitano. Hii ni *trust* (imani) aliyonipa mimi napenda niingie kwenye *Hansard* kwamba namshukuru sana kwa imani hiyo aliyonipa na nawashukuru Makamanda wote kwa kazi ambazo tulifanya nao vizuri mpaka nikatambua zaidi umuhimu wa Jeshi letu hapa Nchini. *(Makofi)*

Pia nataka niingie kwenye *Hansard* kumshukuru Rais wa kwanza Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, yeye ndiye aliyeniamini mara ya kwanza kwa kunifanya Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi mwaka 1978. Hakuwa ananijua nilitoka vijijini na vumbi tupu la uchaguzi akaniamini na ndipo hata Rais Ali Hassan Mwinyi akaniamini na Rais Benjamin William Mkapa akaniamini, hao pia nataka niende kwenye *Hansard* kwamba nimewashukuru. Hakuna nilichowafanyia sana sana tu nilishiriki kumaliza nyumba ya Mwalimu nikiwaongoza wanajeshi. Nilishiriki kumzika Baba wa Taifa, nikiwa kama mwanakamati ya mazishi na wanajeshi ambao niliwasimamia kufanya kazi ile. Hilo ni jambo ambalo nitajivunia na kulikumbuka katika historia yangu. *(Makofi)*

Aidha, pia namshukuru Mzee Rashid Kawawa ambaye nilimrithi Ubunge wa Nachingwea mwaka 1975, alinipa mwongozo na niliufuata na mpaka leo huwa tunashauriana. Katika kipindi hiki cha mwaka 1975 mpaka leo nimekuwa Naibu Waziri

wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri wa Maji na Nishati, *Regional Commissioner* Lindi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, pia nimekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais hadi leo.

Kwa hiyo, nawashukuru wote walioniamini, nawashukuru Wabunge wote ambao tumeshirikiana katika hoja mbalimbali, namshukuru Spika na Wenyeviti, nilianza Ubunge na Mzee Adam Sapi akaja Mzee Mang'enya, akaja Mheshimiwa Pius Msekwa ambaye yuko mpaka leo. Kwa hiyo, hawa wote nimejifunza mambo mengi kutoka kwao, ninapenda vilevile waingie kwenye shukrani zangu. Sasa nasema pia kwamba bila wazazi wangu nisingefika hapa, bila uvumilivu wa mke wangu Elizabeth pamoja na watoto wangu watano nisingiweza kufika hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wosia alionipa mtoto wangu anasoma udaktari sehemu fulani, mtoto wa mwisho ndio ameninunulia juzi suti hii akasema ukavae siku ya hotuba yako ya mwisho Bungeni, kwa hela zake mwenyewe za kufanya kibarua. Namshukuru sana kwa sababu leo nafikiri nimeonekana onekana hivi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri niliofanya nao kazi kwanza nilianza na Marehemu Armir Jamal, Al-Noor Kassum, Mama Anna Abdallah, Mheshimiwa Nalaila Kiula na baadaye nikawa mwenyewe Waziri hao wote nataka waingie kwenye *Hansard* kwamba nimewashukuru. *(Makofi)*

Sasa baada ya kukaa miaka 30 nimejifunza pia kwamba awamu zote hizi zimefanya kazi nzuri. Awamu ya tatu ambayo tumeifanyia kazi sisi Wabunge miaka 10 iliyopita ndio iliyofanya kazi kubwa hii ambayo Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, anasifiwa. *(Makofi)*

Mimi nasema hivi, lakini hakuna aliyenituma Rais Benjamin Mkapa, juzi alikuwa kwenye mdahalo na wale wakubwa wa dunia. Ameitwa kwenye Mkutano wa *G8* huko Scotland, mbona kuna Marais wenye mapembe mapembe hawakuitwa? Kwa hilo ni lazima CCM tujivunie kwamba tumekuwa na kiongozi shupavu. Hata hawa wageni waonakuja mara mke wa Bush, leo ameingia Clinton wanamfuata nchi mwetu na yeye binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, anajua kwamba kama viongozi hawa wanakwenda nchi fulani miezi miwili mizima, maofisa wao wanatembelea nchi hizo na kukaa huko miezi miwili kuchunguza watu hawa ni sawa sawa hakuna vichwa maji hapa, hakuna anayeweza kumtupia mawe kiongozi wetu ndiyo baadaye wanakuja. Sasa yule mkubwa mwingine mke wa Bush amekuja, halafu Rais aliyemtangulia Bush, Clinton anakuja leo maana yake tunaaminika sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wewe unaweza kuwa unafanya vizuri usijielewe kwamba unafanya vizuri na mimi nasema hivi kama Mheshimiwa Rais Benjamini William Mkapa anapata sifa zote hizi na anastahili kweli kupitia CCM, basi

Baraza lake la Mawaziri limefanya kazi nzuri na Waziri Mkuu wake na Wabunge wake wamefanya kazi vizuri, wote hata wa Upinzani. *(Makofi)*

Maana yake wasingefanya vizuri hawa wapinzani, tungepigana nao hawa ngumi humu Bungeni, mbona hatujapigana nao? Kwa sababu kuna watu ambao mimi nazungumzia juu ya nchi nzima siyo Wilayani kwangu tu ambao kwa kutaka kugombea Ubunge wanawabeza Wabunge waliopo. Wewe kama unataka kugombea Ubunge ni haki yako ya Kikatiba kugombea, nenda kagombee Ubunge popote pale. Lakini usigombee Ubunge kwa kuwaponda Wabunge waliokutangulia. Kwa sababu Rais Benjamin Mkapa, amefanya kazi na ninyi Wabunge sifa za Rais Benjamin Mkapa ni za kwenu pia, mtu anasema Mbunge huyu hajafanya lolote hapa huku akiwa anapita kwenye barabara tulizotengeneza sisi. Unajua bwana huku hakuna maendeleo yoyote, huku anazungumza na simu tulizopeleka sisi, hakuna maendeleo mimi ndio nitakaye kuwa Mbunge hapa maendeleo huku kumeoza kabisa. Kumeoza ungezungumza na simu hiyo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe kama unataka Ubunge nenda kagombee Ubunge, tena kama mtu wa CCM unampondaje Mbunge aliyekutangulia? Si useme tu mimi nitagombea nitaleta maendeleo kwa kasi zaidi kama alivyosema Mheshimiwa Jakaya Kikwete, ari mpya na kadhalika. Wakijibiwa mbona barabara ile imejengwa? Anasema ile ni *TASAF* bwana. Je, *TASAF* imekuja bila Mbunge? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kusema Waheshimiwa Wabunge mnapoondoka hapa Bungeni msiwe wanyonge maana wengine naona juzi nimetoka kule nje rafiki yangu mmoja Mbunge mmoja sitaki kumtaja jina. Nimeona pale anatembea kama mnyonge mnyonge, kumbe kuna mtu anamwambia hajafanya maendeleo. Umefanya maendeleo nenda kawaambie. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya kusema hayo nataka kutamka kuwa nimeshauriana na wananchi wangu, marafiki zangu, familia yangu na nataka maneno haya wasikie wananchi wa Nachingwea kuwa kwa hiari yangu mimi mwenyewe baada ya miaka 30 na ni Mbunge mkongwe humu ndani, nimeamua kwamba sigombei Ubunge mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haina maana kwamba natoka kwenye siasa hapa nchini, bado ninazo nguvu na sitoki kwa sababu ya uzee wala nini, nimeamua tu baada ya mashauriano niwaachie wananchi wangu watafute sura mpya tu. Maana kuna watu wengine wanasema Mbunge huyu anafaa sana lakini safari hii tunataka sura mpya tu na mimi ningegombea ningeshinda tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaonisema vibaya waelewe hivyo ningeshinda na sina mtu ambaye nampeleka, lakini watajitokeza watu watawapimwa na mimi nitawafuata wananchi wanavyosema. Sina mtu wasije wakasema anamleta huyu, anamleta yule, lakini nitakuwepo kwenye vikao katika michujo na kuona kwamba nani atawafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, ukinitukana mimi kwamba sijaleta maendeleo Nachingwea wakati maendeleo ya Nachingwea yapo, unawatukana wananchi walionichagua miaka 30 mfulululizo, unaibeza pia CCM iliyokuwa inatekeleza ilani ya uchaguzi, siyo mimi. Kwa hiyo, nawapa usia wananchi wangu chagueni Mbunge ajaye kwa utulivu siyo kwa shari, siyo kwa kuhangaika, wala siyo kwa kutishwa tishwa na mtu na mimi sitoki kana kwamba ninamkimbia mtu, hakuna ninayemkimbia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwaka 2000 nilitishwa hivyo hivyo nikashinda na mwaka huu ningegombea ningeshinda, hayupo ninayemchukia, wote watakaogombea nawapenda. Lakini tutatafuta mtu ambaye anaelekea ana uzoefu na anafanana na kazi ya Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo ajira kwamba na mimi nikaonje, hakuna kuonja hapa ndio maana nilikaa miaka 30 ndani ya Bunge kupitia wananchi wangu. Nawashukuru sana wananchi wote kwa heshima waliyonipa, kwa imani waliyonipa na mimi nawathibitishia nitakuwa mzee mstaafu ambaye sitaingilia na mambo yoyote atakayokuwa anafanya Mbunge ajaye kama atakuja kuniuliza mambo nitamwambia. Mambo yafuatayo kwa mfano anatakiwa ayafuatilie ni Mradi wa Maji wa Bwinji una shilingi bilioni saba na nusu ili kuyatoa maji milimani kuyaleta Nachingwea Mjini na Masasi tunajenga barabara ya Kilimarondo kwa *OPEC Fund* kwa bilioni 1.62, tunapanua Hospitali kubwa ya Kilimarondo kwa ajili ya wananchi ambao wako mbali na Mji wa Nachingwea na tunatekeleza miradi mbalimbali ya maji vijijini na ujenzi wa sekondari katika kila Kata. Nitakaa chini kumwambia Mbunge ajaye mambo ya kila kijiji na wazee gani anaweza kuwaendea mambo yasiende kombo ili kusudi aelewe na nitampa buku zima jinsi alivyonipa mimi Mzee Rashid Kawawa, namna ya kuwaendeleza wananchi wa Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa heshima na tahadhima naunga mkono tena hoja hii mia kwa mia na kwa herini katika Bunge hili kwa maana ya Ubunge wa kutoka Nachingwea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakutakia kheri katika kustaafu Ubunge.

Baada ya hapo nnaomba nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayehusika na Mazingira na Mambo ya Muungano Mheshimiwa Arcado Ntagazwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maelezo na ufafanuzi kidogo katika hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa lengo la kuisaidia Ofisi ya Makamu wa Rais, kutekeleza majukumu yake kwa utaratibu wetu tuliojiwekea wa kufanya kazi kama familia moja. Lakini tunaimrishwa kwa maana ya kutaka kuweka ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya katika utekelezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwatambue waliochangia humu Bungeni ambao ni Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. Hawa wamechangia kwa kuzungumza hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi wako 17 Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Jussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali tena, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na ndugu yangu Mheshimiwa Halimenshi Mayonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba michango yao kama nilivyosema ni ya kutuimarisha katika utendaji wetu wa kazi, katika kuwatumikia Watanzania wenzetu katika majukumu iliyokabidhiwa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu na sheria iliyotoa majukumu, kwa mfano yanahusiana na mazingira na masuala haya ya kupambana na umaskini.

Sasa nikiri kwamba pengine haitaniwia rahisi kuzungumzia kila mchango uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika muda tulionao. Lakini yatosha niseme kwamba miaka yote tumekuwa tukipokea michango hii na kuifanyia kazi na kurudisha hata majibu yetu kwa maandishi kwa Waheshimiwa Wabunge. Safari hii inaweza ikatuwia si vigumu kwa maana ya kutenda, lakini liko suala kwamba tarehe 29 Julai, 2005 Bunge litavunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitakachokifanya majibu ambayo tungewapelekea Wabunge kama tungekuwa tunaendelea, tutayatoa kama kawaida yetu yatawekwa katika maktaba kwa sababu pale ni hazina ya michango ya Waheshimiwa Wabunge. Lakini kama tunaweza tukatoa kabla ya uchaguzi tunazo anuani za Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukawatumia kwa njia hiyo. *(Makofi)*

Sasa napenda niwashukuru wote hao niliowataja na katika shukrani hizi kwa sababu asubuhi sikupata nafasi ya kutosha ningependa kwa kweli niwashukuru sana. Kwanza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ametutunza kusema kweli kama watoto wa familia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao hamkubahatika kufanya kazi na Mheshimiwa Makamu wa Rais, nawaombeni mniamini mia kwa mia. Sisi katika Ofisi yake ukiwa na jambo ukimwendea utajiona kweli uko mikononi mwa mlezi kama vile baba. Ni kiongozi, hana makuu, ni kiongozi ambaye yuko tayari kukusikiliza katika kila jambo na kukuelekeza. Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru pia Katibu Mkuu Mwandamizi Raphael Mollel, Mary Mushi na Mkurugenzi wa Maendeleo na Utumishi pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo mbalimbali katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana niseme na mimi binafsi na kaka yangu Mheshimiwa Waziri Edgar Maokola-Majogo na kama wanakumbuka nilipoteuliwa katika Ofisi hii niliwaambia wanikubalie kwamba sijui kitu. Lakini nitajitahidi kuwa mwanafunzi tena wa Shule ya chekechea ili nisiwaangushe kwa lugha ya kawaida katika yale ambayo wao wamebobea katika kuyajua.

Mimi nawashukuru sana, wamenifunza na nimejitahidi kujifunza na ninapotumwa kwenda katika Mikutano ya Kimataifa nina hakika siwaangushi hata kidogo. Sasa masuala ambayo nitapenda kuyazungumzia na pengine nitagusia mahsusi yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya Muungano tunazungumzia sana suala hili la kero za Muungano na pengine hata kulizunguzia suala hili, sisemi kwamba inakuwa kero lakini pengine tunazungumzia mambo ambayo pengine yanaelekea kutukatisha tamaa pale ambapo tunafanya mambo mazuri na ambayo tunapashwa kuwaeleza wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Sheria za Muungano *(Articles of Union),* unaona waasisi wetu kila walicholenga ni masula ya umoja wa wananchi wa nchi zilizokuwa Jamhuri ya watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika kwamba watu hawa asili yao ni wamoja, watu hawa wana udugu wa damu, watu hawa wana ushirikiano wa miaka nenda rudi kwa karne na karne na ukitaka kurudi katika historia ya wakati ule kipindi cha ovyo kile cha utumwa utaelewa ni kwa nini kuna udugu huu kwa Watanzania wa leo waliokuwa katika nchi huru mbili za Jamhuri ya watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nikisoma Sheria hii hasa misingi ya Muungano wetu ambayo inasema hivi, ninukuu kwa kiingereza na watu wa *Hansard* nitawapigieni *photocopy* kama kidogo kiingereza kitawapita pembeni: "*Whereas the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar, being mindful of the long association of the peoples of these lands, and of their ties of kinship and amity, and being desirous of furthering that association and strengthening of these ties and of furthering the unity of African peoples, have met and considered the union of the Republic of Tanganyika with the Peoples' Republic of Zanzibar."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi hiyo ya udugu, umoja na ushirikiano wa siku nyingi. Sasa tunapozungumza sana kuhusu matatizo, kero za Muungano pengine nikubaliane na Mheshimiwa mmoja aliyesema kwamba hapa pengine tunafanya kosa la ubinafsi. Kwa sababu umoja wa watu wetu hauwezi kuruhusu masuala haya ya kero na nikubaliane na hoja kwamba ukichukulia umoja wetu, udugu wetu na ushirikiano wa miaka nenda rudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna jambo linalotuzuia kuketi kitako kwa lugha ya Zanzibar na kujadili haya yanayosemwa na wakati mwingine kukuzwa kwamba ni kero za Muungano. Kwa hiyo, ninakubaliana kabisa kwamba haiko siri ya kutokaa kitako na kuzungumza yale yanayodaiwa kuwa ni kero za Muungano na tukiyazungumza tutaimrisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika hili nikubaliane kabisa na mchango wa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. Kwanza naipongeza Kambi ya Upinzani kwa maoni yao ya kuhitimisha kusema wanaunga hoja mkono, hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la Muungano Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ametuambia kwamba, kwa leo hayuko mtu ambaye ana azma ya kuuvunja Muungano na anapofanya hivyo au hata anapofikiria hivyo ajue kwamba anafanya kitendo cha uhaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa umoja wetu, kwa udugu wetu, kwa ushirikiano wetu wa miaka nenda rudi kweli tujadili masuala ya Muungano wetu, lakini kwa lengo la kuuboresha daima dumu. Sasa yako haya ambayo yamezungumzwa kwa mfano suala la mchango wa Serikali ya Muungano kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ile asilimia 4.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba huu ni utaratibu ambao uliwekwa kwa kipindi cha mpito. Tunaamini Tume ya Pamoja ya Fedha chini ya Uwenyekiti wa Mbunge wa Bumbuli, Mheshimiwa William Shellukindo. Kwa mujibu wa Sheria tuliyonayo watayaangalia kwa kina na kuyatolea maelezo na hata miongozo ili haya yanayosemwa kila wakati kero za Muungano, matatizo ya Muungano Tume hii ya pamoja itusaidie kuondokana na hali hiyo na tuweze kuufurahia na kujivunia Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri niliseme hili kwa hili lingine ambalo unalipata katika Katiba kwamba ule mfuko wa pamoja unachangiwa na Serikali mbili, Serikali ya Muungano na ukisoma Ibara ya 4 utaona kuna majukumu. Kuna Serikali ya Muungano yenye majukumu ya masuala ya Muungano na kuna Serikali ya Muungano sehemu yake inashughulikia masuala ya Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hizi Serikali mbili kwa uchambuzi huo zinatakiwa zichangie uendeshaji na kugharamia shughuli za Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujue mapema tunafahamu uchumi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ama Tanzania Bara ni ndogo. Kuna *dis-economies of small scale,* nchi ile ni ndogo kijiografia na uchumi wake ni mdogo vile vile. Sasa tukakaposema tuongeze kiwango tujue kwamba hata ule uwajibu wa kuchangia shughuli za Muungano nao utaongezeka. Hili ni vizuri likajulikana kwa sababu tusifikiri kwamba ni suala la kupokea tu, kuna haki na wajibu hili lieleweke mapema maana tusije tukawa tunaambizana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa maneno kwamba kwa mfano Kamati unayoiongoza wewe mwenyewe ni Kamati ya Maliasili na Mazingira na inashughulikia Wizara au Ofisi ya Makamu wa Rais inashughulikia masuala la Muungano, mazingira, kuondoa umaskini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na inasemwa kwamba haitamkwi suala la Muungano chini ya uongozi wa Kamati unayoisimamia. Lakini tukienda kwenye majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira wajibu wake kwa niaba ya Bunge zima ni Ofisi ya Makamu wa Rais.

Sasa huwezi kuondoa suala la mazingira kwa sababu Kamati inasimamia Ofisi nzima na majukumu yote ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hili kwa wale waliosema hata ukiangalia Kamati Maliasili na Mazingira, Muungano haumo, sasa ni kama kwa mfano Mwanasheria angesema Kamati yako Mheshimiwa Mwenyekiti kana kwamba haina tunachokiita *locus standi* unasimama wapi kuzungumzia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika masuala ya Muungano yamesemwa mengi lakini sidhani kama ninayo nafasi ya kuyazungumzia yote. Lakini nikubaliane pia na Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika mchango wake wa maandishi alizungumzia suala la elimu kwamba wananchi waelimishwe na hili amelirudia hata kwa upande wa masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama hatukujipa nafasi ya kuelewa mambo barabara basi tunaweza tukasema yale ambayo hayatusaidii katika kudumisha Muungano wetu na kuuelewa ipasavyo.

Sasa pengine niende kwenye masuala ya mazingira ya jumla ambayo najua yamezungumzwa kwa mfano Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, alisema mmezungumizia juu ya mipango ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, ambako ni kweli kabisa nimebahatika kufika *Mbamba Bay* nimelala pale na nimeona kwanza kwa mfano uharibifu wa mazingira katika Ziwa lile ambao umesababisha kutoweka kwa samaki mmoja anaitwa Mbasa, wanamfahamu wakazi wa kule.

Sasa niseme katika Mradi wa Hifadhi ya Mazingira katika Ziwa Victoria tulikuwa na tatizo mahsusi, magugu maji ambayo yaliharibu kabisa mfumo wa usafirishaji Ziwani na shughuli za uvuvi. Kwa hiyo, ikabidi tulishughulikie suala hili na katika kulishughulikia ndipo tukagundua kwamba hushughulikii mazingira ya Ziwa kusema kweli unaangalia raslimali iliyopo na shughuli za wananchi kujipatia riziki au kufanya shughuli za maendeleo na ni kutokana na uzoefu tulioupata kwa mafanikio makubwa kabisa tukabuni na Mradi wa Ziwa Tanganyika ambao wenyewe tumeanza na mkataba baina ya nchi zinazozunguka Ziwa lile na tulikuwa tumejipangia kwamba mradi huu ungeanza kufanya kazi na bado naamini utaanza kufanya kazi katika mwaka huu wa fedha wa 2005/2006.

Kwa hiyo, kutokana na uzoefu ule pia tulibuni mradi katika kutekeleza Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Nyasa. Tatizo tulilolipata ni kama tunavyosema juhudi zetu sisi

wenyewe bila kupata msaada, namshukuru Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, amesema misaada ni muhimu inachangia kutia nguvu na kasi mpya katika maendeleo yetu na kwa sababu tulitaka kushirikiana na nchi zinazozunguka Ziwa Nyasa wahisani wetu ikiwemo Benki ya Dunia walibaini kwamba moja ya nchi hizo ilikuwa haitoi kipaumbele kwa masuala ya mazingira kwa hiyo wakasema hawatakuwa tayari kuhisani au kufadhili Mradi na ndiyo tumesita hivi sasa tunatafuta namna ya kupata nani wa kujaza pengo ambalo tungepata fedha kutoka Benki ya Dunia. Kwa hiyo, ndiyo maelezo na ninadhani tulishawahi kujibu swali hapa kuhusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, yeye amesema anaunga mkono kabisa suala la Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria si kwa sababu anatoka kule lakini kwa sababu ni moja ya eneo linalotupa fursa ya kupambana na umaskini kwa wananchi wetu kwa raslimali alizotujalia Mwenyezi Mungu, maana lile Ziwa Mwenyezi Mungu alipoiumba dunia yetu akaliweka pale lilipo na sisi wengine tumezaliwa maeneo hayo hakuna aliyepeleka maombi kwamba tafadhali nizaliwe Kigoma au nizaliwe Kibondo. Lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu tunayo raslimali ile pale. Katika Hifadhi ya Mazingira tunacholenga ni raslimali ya kuwezesha wananchi wetu kujipatia riziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala moja ambalo nina hakika katika mchango wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri alikuwa analiulizia na ni moja ambalo linahusu miradi ya kupanda miti kwa wananchi wetu na ni kweli tumepokea miradi kadhaa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Niseme tu kwamba kwa sababu katika Ofisi ya Makamu wa Rais mara nyingi tunajikuta sisi wenyewe hatuna fedha hizo ingawa tunaziombea kibali kwa sababu zitapatikana kutoka kwa wahisani. Zisipopatikana ndipo unakuta sisi tunasuasua tu kutekeleza lakini kusema kweli tunakuta tunachewa kutekeleza litakiwalo kwa sababu hatuna fedha katika mfuko au katika Akaunti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini siku zote tunapenda kuwashirikisha wahisani katika juhudi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Edgar Maokola-Majogo, kaka yangu hapa ni kweli nchi yetu Waheshimiwa Wabunge kupitia uongozi madhubuti na thabiti wa Kiongozi wa Taifa letu Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. Nchi yetu sasa hivi tunaaminika na kusema kweli hata tunaheshimika sisi wengine tunaokwenda kwenye mikutano ya Kimataifa ukisimama na iko Bendera ya Tanzania unasikilizwa, si kwa sababu una kitu chochote lakini ni kwa sababu ya heshima na sifa ya Tanzania siku hizi ambayo tumejengewa na Viongozi wetu wa ngazi ya juu hasa hasa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa najiuliza na ninajiuliza kwa dhati kabisa sijui ilikuwaje nikachaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira Duniani. Nikijiuliza kwa dhati ya moyo wangu mimi nimezaliwa katika Kijiji kidogo sana kinaitwa Nyarugusu kule Wilayani Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanakijiji wa kawaida kabisa, hivi kama si Chama cha Mapinduzi na Uongozi wa Serikali ya Chama hicho kwa heshima tuliyopata katika nchi kupitia viongozi wetu hawa nani angemjua huyu mwanakijiji wa Nyarugusu anayeitwa Arcado Ntagazwa? Hayupo kweli, hayupo na ndiyo maana nakumbuka walivyoniuliza waandishi wa habari nilipokuwa narudi kutoka Korea mimi niliwaambia namshukuru Mwenyezi Mungu,nawashukuru wazazi wangu na pia ninakishukuru Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba hii imetupa pongezi Mheshimiwa Semindu Pawa, amesema sisi ni wale watoto wanaozaliwa kabla ya wakati wake kwa maana ya kwamba tunafanya mambo makubwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais, njiti.

Lakini haya yote ni kwa sababu viongozi wetu wa juu Mheshimiwa Rais, Makamu na Waziri Mkuu wametufundisha kuwa Viongozi Watumishi na tunapenda kujitahidi kwa uwezo wetu na kwa uwawezo wa Mwenyezi Mungu kuwatumikia Watanzania katika majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudie pale kwenye Muungano kwamba Koti sasa hivi linabana na alituasa Marehemu Baba wa Taifa kwamba ni vizuri kushona Vazi Jipya. Mimi nahisi na nakubali kwamba mchakato huu tulifanya kupitia *White Paper* miaka si mingi iliyopita. Watanzania kwa wingi wao walituambia tuendelee na Mfumo wa Muungano wenye Serikali mbili. Sasa kama hili koti linaendelea kubana sisi tumesema sisi ni watumishi wa watu mtakapofika wananchi watasema sisi mabosi wenu tunakata koti lishonwe upya. Bila shaka mchakato upo na sheria zetu zinaruhusu kufanya jambo hilo kwa hiyo sidhani kama tutafika mahali kwa kuwa koti linabana tuendelee kuvaa koti ambalo kila mmoja atatuona kwamba vazi tulilovaa kusema kweli halitusitiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie moja ambalo alilisema Mheshimiwa John Singo, kuhusu kongamano au mkutano unavyofanya wadau wa mazingira katika Wilaya za Same na Mwanga. Mimi napenda nimshukuru kwa kuwa walinishirikisha lakini cha kushukuru zaidi narudi kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Elimu, pale wananchi wa Wilaya hizo mbili kweli walipata elimu na kutambua kwamba bila Hifadhi ya Mazingira katika eneo la Wilaya za Same na Mwanga azma ya kupambana na umaskini na azma ya kujiletea maendeleo haitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulitolewa mfano wa chanzo kimoja cha maji katika miaka nilifanya hesabu za haraka haraka katika miaka 30 iliyopita kiwango cha maji yaliyokuwa yakipatikana kilikwisha kupungua kwa asilimia 75 yaani robo tatu. Sasa kwa maana hiyo ni kwamba ukichukulia miaka 40 kama mambo yataendelea hivi yalivyo ni kwamba chanzo kile cha maji kitakuwa hakina hata tone la maji kwa sababu yote yatakuwa yamekauka kutokana na uharibifu wa mazingira na bahati nzuri katika kulitambua tatizo hilo sheria yetu ya mazingira imezungumzia suala la Hifadhi ya Vyanzo vya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba shughuli yoyote isifanyike katika eneo la chanzo cha maji katika umbali wa mita 60 na wananchi wale wang'amua waziwazi

kabisa kwamba suala hili ni lazima lizingatiwe vinginevyo binadamu anachangia kutoweka kwake mwenyewe.

Kwa hiyo, nilishukuru kwa kunishirikisha na niling'amua waliwashirikisha wadau tangu viongozi wa dini mpaka tulipata kiongozi wa dini ya asili na yeye alikuwa ni mmoja kati ya wadau na walitoka pale na maazimio mazuri sana. Ninachoomba tu nimuombe Mheshimiwa Mbunge pengine ni vizuri na wao wakatuletea kwa maandishi wamefikia wapi ili na sisi tuchangie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu suala la Baraza Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Niseme tu kwamba ukisoma Sheria yetu ya Mazingira imetoa majukumu makubwa na imetoa mamlaka kwa Baraza hili katika kusimamia Hifadhi ya Mazingira katika nchi yetu. Ukianzia kwa mfano katika suala la migodi ni lazima kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kabla ya kuanza kuchimba madini yanayohusika na suala hilo linasimamiwa kikamilifu kwa sababu mwekezaji anatakiwa yeye mwenyewe atafute wataalamu waelekezaji wamwambie katika kuchimba madini katika eneo hili uzingaitie moja, mbili na tatu ili kuhifadhi mazingira. Anafikisha mpango ule katika  na Baraza linaendelea kufuatilia kama yale yaliyoandikwa ndivyo yanavyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kifupi ningependa niseme kwamba Sheria yetu ukiisoma vizuri na nashukuru sana wewe ulitusaidia sana katika Ofisi ya Makamu wa Rais kushughulikia, kupatikana na kufikia mahali sheria hii ikatungwa na Bunge hili Tukufu. Sheria iko barabarakatika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuna jambo nililisikia wakati fulani kuhusiana na vyura wa Kihansi na kwa sababu vyura hawa wako Tanzania lakini hawako mahali pengine duniani. Suala hili la kusema vyura hawa wametoweka ni vizuri tukaliweka vizuri, wale waliopelekwa Marekani, vyura ambao wamekufa ni wale wanaoitwa *Parent Stock,* unaweza ukawaita vyura , sijui utawaita wazazi au vipi. Vyura waanzilishiwa kizazi waliopelekwa kule Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri tukakumbuka, mimi nakumbuka nilipokuwa Wizara ya Ardhi,  Maliasili na Utalii kuna Mbunge mmoja alinipa elimu kwamba hawa samaki wanaitwa Makaji au *Shrimps* kwa kingereza miezi 18 wameshaishi na wanakufa kutokana na umri mkubwa. Sasa mpaka leo hii hakuna anayejua umri wa kuishi vyura hawa aina ya vyura wa Kihansi ni umri gani lakini wamekwisha kwenda kule Marekani zaidi ya miaka mitatu hivi leo lakini watoto wa vyura hao na ni watoto kweli maana vyura hao wanazaa watoto hawatagi mayai wanaendelea kuishi na mimi niliwaona baadhi yao *zoo* moja kule Detroit  katika jimbo la Michigan.

Kwa hiyo, vyura wale wapo lakini hapa kwetu wametoweka ingawa wamepatikana vyura wa aina nyingine sasa kwa sababu hatujui tabia na hulka zao inawezekana kuna mahali wamejichimbia watakuja kuonekana hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kusema katika muda niliokuwa nao sikuweza kujibu na sikuweza kutosheleza hoja za WaheshimiwaWabunge lakini tumezichukua zote tutaendelea kuzifanyia kazi kwa sababu Serikali ipo kuwe na uchaguzi au kusiwe na uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwatakia wote wale wanaokwenda kugombea kila la kheri, wananchi watupe dhamana yao turudi kuitumikia nchi yetu kupitia Bunge hili na *inshallah!* Mwenyezi Mungu atusaidie wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26 - Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration And General* ... ... ... ... ... ... 1,796,829,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ...2,593,750,900/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...88,134,100/=
Kifungu 2001 - *Union Secretariat* ... ... ... ... ... ... ... ...... ... ...24,155,485,400/=
Kifungu 3001 - *Poverty Eradication* ... ... ... ... ... ... ...... ... ... 1,916,576,600/=
Kifungu 4001 - *Non Government Organisations* ... ... ...... ...102,901,200/=
Kifungu 5001 - *Environment* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...1,076,707,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ...837,900,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Poverty and Eradication*... ... ... ... ... ... ... ...22,189,931,200/=

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kifungu kile kile

**MWENYEKITI:** Tumia *microphone* tafadhali.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Kifungu kidogo 6257, wakati nikichangia niliongelea kuhusu mashirika mengi ambayo yanarundikana mahali fulani fulani lakini mikoa mingine inaachwa hivi hivi. Sasa ningeomba Ofisi ya Makamu ya Rais ambayo ndiyo inayoratibu na kufuatilia mashirika haya kuhakikisha kuwa kama haya mashirika ambayo yanapeleka misaada katika maeneo fulani fulani inavyopendelea sasa mikoa ambayo inaachwa inapiga mihayo ifidiwe katika bajeti hii watenge fedha za kupeleka kusudi maendeleo yawe balance katika mikoa mingine.

Sasa ningeomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwa kweli hatuwezi kuwa waangaliaji tu na wengine wanaendelea. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza samahani kuwa Mheshimiwa Leonard Shango kwa kutokugusia hoja yake wakati ninajumuisha maana yake kulikuwa na mambo mengi kichwani mwangu hasa nilitaka niliteme lile la mwisho sasa atanisamehe na aniwie radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yasiyo ya Kiserikali kama mtakavyokumbuka wakati tunapitisha Sheria wale wanaoendesha *NGOs* walikataa sana ile Sheria kwa sababu ya nini. Kwa sababu chimbuko lake hasa ni wananchi wenyewe aidha, mmoja mmoja au kwa makundi, mmoja anaanzisha anawakusanya wenzake wanaanzisha Shirika lisilo la Kiserikali inaanzia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni katika kipindi kirefu kila wanapochangia Waheshimiwa Wabunge wametuambia hili la kusema mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa nini yanalundikana mijini. Mara nyingine unakuta wastaafu wameanzisha *NGO* si ajabu hata mimi ukasikia nimeanzisha *NGO* maana yake vya kufanya hakuna na unataka bado kuwahudumia wananchi kwa njia moja au nyingine. Kwa hiyo unakuta wengi wako mijini.Lakini tulisema pia kwamba sehemu mojawapo ya kazi yetu Ofisi ya Makamu wa Rais kwenye kitengo cha *NGOs* ni kuhamasisha na kushawishi wanaoandikisha *NGOs* siyo tu waziandikishe vijijini lakini wafikishe shughuli zao mpaka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siyo hilo tu, hata wakati tumeanzisha utaratibu wa kuandikisha tumesema humo tunaanza kuandikisha kutoka Wilayani ili kufanya *NGOs* mengine yaanzie huko huko Wilayani. Wanafanya kazi kwenye Wilaya wengine Kimkoa, Kiwilaya wanaandikisha Kiwilaya na Kimkoa wanaandikisha Mkoani na wale wa zaidi ya mkoa mmoja wanaandikisha Kitaifa kwa sababu hiyo hiyo kwamba viende kule mikoani. Kusema kwamba sasa sehemu isiyo na *NGO* Serikali ifidie wakati mashirika yenyewe ni yasiyo ya Kiserikali hata *concept* yenyewe inakuwa *defeated.* Kwa hiyo, tuhamasishe tuanzishe mashirika yasiyo ya Kiserikali katika maeneo yetu, Serikali haina sera ya kufidia maeneo yale ambayo hayana *NGOs.*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Nililokuwa naongelea ni kuwa Mashirika kama *TASAF* na *SELF* zijaribu kwenda *widely* katika mikoa ambayo haijafika kwa mfano Wilaya yangu ya Iramba wanaisikia tu lakini haijafika kule sasa Wilaya kama zile na nyingine katika nchi basi Serikali au Wizara au Ofisi ya Makamu wa Rais ielekeze kuwa kazi zao zifike pia katika Wilaya zile ambazo hawajafika. Nakushukuru.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Leonard Shango, kwa maelezo yake ya kutaka ufafanuzi. Nikianzia *TASAF* narudia kusema kwenye semina zetu mbili tumesema na leo nasisitiza tena kwamba awamu ya pili ya *TASAF* iliyozinduliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais imeelekezwa iende kutekeleza miradi hiyo nchi nzima Wilaya zote kupitia Halmashauri na kuna fedha zisizopungua dola za Marekani kama sikosei 174.5 kama nikikosea ushee ushee hivi tu. Bilioni 170 za fedha za Kitanzania zitakwenda kila Wilaya sasa nawashauri nendeni mkachacharike na wananchi wenu waibue miradi kutoka chini kwenda juu, wote watakaoibua miradi watapewa fedha hizo kwa formula ambayo imewekwa.Kuna percent kila Wilaya itapata halafu itafuatwa kutokana na wingi wa watu, kila Wilaya itafaidika na mradi huu. *(Makofi)*

Lakini hata hivyo tutazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba pale tutakapoona wanasinziasinzia tutawatikisatikisa kusema vipi ninyi huko vipi mbona hamuombi? Hiyo lazima tufanye na Mkurugenzi wa *TASAF* ananisikia hapa kwamba msisubiri tu wameibua wengine bwana sisi wepesiwepesi kufanya mambo harakaharaka hao tuwaendee kwamba kuna pesa ninyi hapa mbona hamjatekeleza, kuhamasishana maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hili lingine la kusema twende mikoani kwenye mambo ya *SELF* mwaka jana tumeongeza mikoa 8, tulianza na 6 tumekwenda mikoa 8. Nia yetu tutakwenda tena chini lakini tunakwenda hatua kwa hatua kwa hiyo tutazingatia ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge hususani maeneo yale ambayo yako chini kwa maana ya viwango vya umaskini viko chini sana ndiyo wanastahili vile vile watazamwe mapema zaidi. Lakini baada ye hatutakwenda kwa awamu tutakwenda kwa nchi nzima kwa hiyo namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake kwa sababu sisi Mawaziri tuko hapa Wataalamu wetu kuanzia Katibu Mkuu Mwandamizi na Wataalam wote Katibu Mkuu wote wako hapa tutazingatia hayo tutekeleze ipasavyo.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Environment* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...4,811,000,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge hili Tukufu imepitia Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo ikubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.27 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 21 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*